

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 18 Juni, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, Kikao cha Arobaini na Saba. Swali la kwanza linaelekezwa kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na litaulizwa na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi. Mheshimiwa Esther kwa niaba yake.

Na. 390

Kuinua Ajira kwa Vijana wa Kitanzania

MHE. JOSEPH M. MKUNDI (K.n.y. MHE. ESTER M. MMASI)
aliuliza:-

Serikali imeonesha nia madhubuti kupitia mikakati yake ya kuinua ajira kwa Watanzania.

Je, ni kwa namna gani Serikali imejipanga kuinua ajira kwa vijana kupitia makundi maalum kama vile vijana wa kidato cha nne, darasa la saba na waendesha bodaboda?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kukuza fursa za ajira kwa vijana kupitia makundi mbalimbali ya ngazi za elimu na waendesha bodaboda, Serikali imejipanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zote zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira, hususan kilimo na biashara, aidha, katika hili Serikali itajikita zaidi kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji wa viwanda vidogo, vyat kati na vikubwa ili kufikia lengo la asilimia 40 ya nguvu kazi nchini kuwa katika sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2020 kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

(ii) Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao unalenga kuwasaidia vijana kuweza kujajiri na kuwapa mikopo ya masharti nafuu na mafunzo ya ujasiriamali.

(iii) Ni kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Ujuzi nchini ambao umelenga kutoa mafunzo ya vitendo yatakayofanyika maeneo ya kazi ili kuwapa vijana wengi fursa za mafunzo Serikali imeanzisha programu maalum ya kutambua ujuzi uliopatikana nje ya mfumo usio rasmi na kurasimisha kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wale watakaobainika kuhitaji na kuwapa vyeti. Utaratibu huu unawapa fursa vijana wetu kuendelea na mafunzo rasmi na mfumo rasmi wa mafunzo na pia kutambulika na waajiri au watoa kazi.

(iv) Mwaka 2017 Serikali ilirekebisha Kanuni za Sheria ya Usafirishaji za mwaka 2010 kwa lengo la kuruhusu

bodaboda na bajaji kubeba abiria na kurasimisha ajira ya waendesha bodaboda na bajaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Azimio la Wakuu wa Mikoa la mwezi Novemba, 2014 kuhusu kuongeza fursa za ajira kwa vijana kwa kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za uzalishaji na biashara, lakini pia kutoa kipaumbele kwa kununua bidhaa na huduma zinazotolewa na vijana na kutoa mikopo ya masharti nafuu.

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa endelea.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, nishukuru vilevile kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa za Serikali za kuwezesha vijana katika maeneo mengi, lakini bado kuna Sekta ambayo inaa jiri vijana wengi sana kama vile sekta ya uvuvi na kilimo lakini hasa kwenye sekta ya uvuvi vijana wengi wameajiriwa maeneo haya lakini wanakutana na vikwazo vingi sana vinavyowafanya washindwe kufaidika na shughuli zao hizi za uvuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba vijana wanaojajiri na kuajiriwa kwenye sekta kwa mfano ya uvuvi wanaondolewa vikwazo wanatambuliwa na kuwezesha ili waweze kufanya shughuli hizi na kufaidika na shughuli hizi za uvuvi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Lakini, swali la pili kilimo ni sekta muhimu sana inayoweza kuwasaidia sehemu kubwa sana ya vijana, lakini bado sioni kama Serikali imefanya juhudhi za kutosha za kuweza kuwatambua vijana walio na mahitaji ya kuweza kujajiri kwenye sekta hii ya kilimo na kuwawezesha kwa kuwapa mtaji ili wafanye shughuli za Kilimo zenye ufanisi, nini mpango wa Serikali kutumia Kilimo kama sehemu kubwa inayoweza kuajiri vijana wengi kwenye nchi hii?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kutoka kwa Mbunge wa Ukerewe Mheshimiwa Naibu Waziri Mavunde tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA, AJIRA: Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza Serikali inatambua ya kwamba moja kati ya sekta ambayo inachangia katika kutoa nafasi za ajira ni pamoja na sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, mpango uliopo hivi sasa na ambaao tumeanza kuutekeleza ni kuendelea kuwaweka vijana wote wanaofanya shughuli za uvuvi katika ushirika na vikundi mbalimbali ili waweze kupata fursa kukopesheka kupitia Mifuko ya Mendeleo ya Vijana lakini vilevile Mifuko ya Uwezeshaji na hivi sasa tumeshafanya kazi hiyo katika baadhi ya Mikoa ikianzia Mkoa wa Geita kwenye Wilaya ya Chato, lakini vilevile na Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Pangani tumeanza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua na tupo katika mkakati wa kuhakikisha kwamba tutaishirikisha na Benki ya TADB ili waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu kilimo, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano na Wizara ya Kilimo tunatekeleza kwa pamoja mpango wa kuwashirikisha vijana kwenye kilimo ambaao una lengo la kuwafanya vijana hao kutumia fursa ya kilimo kama sehemu ya ajira.

Mheshimiwa Spika, mpaka ninapozungumza hivi sasa tayari mpango huu umeanza kutekelezwa na vijana wengi hivi sasa wameshaanza kubadili mtazamo na kukichukulia kilimo kama pia ni sehemu ya ajira tofauti na pale awali ambako kilimo ilikuwa ni *last resort*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mpango huu unatekelezwa kwa pamoja na tumeanza hivi sasa katika Mpango wa Kitalu Nyumba ambaao utashirikisha vijana 18,800 nchi nzima, lakini vilevile kampuni za vijana zinazofanya kilimo pia zimeanza kushiriki moja kwa moja katika kuhakikisha

kwamba wanaanza kutoa msukumo na mtazamo kwa vijana wengine wengi kuingia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatambua jambo hilo na Serikali tunaendelea kulifanyia kazi.

SPIKA: Tunaendelea na TAMISEMI, Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka uliza swali lako.

Na. 391

Uwezo Mdogo wa Halmashauri Kujiendesha

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA aliuliza:-

Halmashauri nyingi zina uwezo mdogo wa kujiendesha kwa kutumia mapato yake ya ndani.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha katika bajeti ili kuzisaidia Halmashauri kujenga hospitali na vituo vya afya badala ya kuziachia jukumu hilo Halmashauri pekee?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mkakati wa ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Halmashauri mbalimbali nichini. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 na mwaka 2018/2019 Serikali imejenga, imekarabati na kupanua vituo 352 ikiwa

hospitali tisa, vituo vya afya 304 na zahanati 39 vya kutolea huduma za afya nchini kwa gharama ya shilingi billioni 184.67.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetoea kiasi cha shilingi billioni 100.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa hospitali 67 za Halmashauri. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali imetenga kiasi cha shilingi billioni 10.4 kwa ajili ya ujenzi wa vituo 52 vya afya na shilingi billioni 46.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 27 za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha na kujenga vituo vya afya vya kutolea huduma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka swali la nyongeza tafadhalii.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa naangalia kwenye haya majibu ya Serikali naona wametenga pesa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali, lakini pamoja na vituo vya afya, lakini kwenye majibu haya sijaona pesa ambayo imetengwa kwa mwaka 2019/2020 kwa ajili ya maboma ambayo yako mengi sana sehemu mbalimbali ambayo wananchi wamejitelea nguvu zao kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo hasa ya zahanati, ujenzi wa zahanati.

Mheshimiwa Spika, sijui Serikali ina mpango gani wa kusaidia kukamilisha ujenzi wa maboma mbalimbali ambayo yamo katika sehemu mbalimbali za majimbo yetu? Swali la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Tabora Manispaa jengo la Halmashauri limechakaa sana mpaka linavuja,

sehemu nyingi zinavuja, lakini Halmashauri kwa mapato yake ya ndani imejitahidi kuligharamia jengo hilo na imelipa mpaka sasa hivi zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa mapato ya ndani na toka ujenzi umeanza mwaka 2014 Serikali imewahi kutoa shilingi milioni 450 tu katika kusaidia ujenzi wa jengo hilo. Sasa sijui Serikali ina mkakati gani wa kusaidia ujenzi wa jengo hilo ambalo ujenzi wake unafikia shilingi bilioni tano ambayo kwa mapato ya Halmashauri kama ya Tabora Mjini si rahisi kukamilisha, Serikali ina mkakati gani? (*Makofî*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo ya Wanyamwezi wa Tabora, Mheshimiwa Naibu Waziri Josephat Sinkamba Kandege tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, katika swali lake la mwanzo anauliza haoni fedha ambazo Serikali imetenga kwa ajili ya kumalizia maboma ambayo wananchi wametumia nguvu katika kuyajenga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, msingi wa majibu katika majibu yangu ya msingi yametokana na swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu katika swali lake la msingi ni kama vile hakuona jitihada ambazo zinafanywa na Serikali katika kuhakikisha ujenzi wa vituo vya afya, hospitali pamoja na zahanati na ndiyo maana katika majibu ambayo nimempa nimeonesha idadi ya fedha ambazo zimetolewa na Serikali na nia njema ya Serikali ambayo inaongozwa na CCM na sisi katika llani yetu tumeahidi pale ambapo wananchi wanatoa nguvu yao na Serikali tunapeleka mkono kusaidiana na wananchi ili kuhakikisha nguvu ya wananchi haipotei na yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge ni shuhuda nguvu kubwa ambayo inapelekwa na Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma za afya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika swali lake la pili kuhusiana na ujenzi pale Manispaa ya Tabora ambao unatakiwa ugharimu kama kiasi cha bilioni tano ni ukweli jengo limeanzishwa ni kubwa kweli na katika hali ya

kawaida kwa bajeti ya Serikali inavyotengwa si rahisi kwamba jengo hili litakamilika lote kwa mara moja na ndiyo maana tumekuwa tukiwashauri ni vizuri tukaanza upande ambao tunaweza tukaukamilisha ukaanza kutumika wakati ujenzi mwingine unaendelea kwa kadri bajeti itakavyokuwa inaruhusu. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Silinde swal la nyongeza.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, na mimi niulize swal dogo la nyongeza kwenye swal hili la msingi mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilitenga shilingi bilioni 251 kwa ajili ya kumalizia majengo ya zahanati, maboma pamoja na maboma ya shule za msingi, lakini fedha hizo katika mwaka huu hawakutoa kitu na mwaka wa fedha uliofuatia 2018/2019 ambao tupo Serikali ilitoa shilingi bilioni 69 kwa ajili ya shughuli kwa maana shilingi bilioni 39 kwenye majengo ya zahanati na shilingi bilioni 28 kwenye majengo ya shule za msingi.

Sasa nataka kujua *commitment* ya Serikali ya shilingi bilioni 184 zilizobaki za fedha za ndani kwenda kumalizia maboma hayo ya zahanati katika nchi zetu ikiwemo Jimbo la Mombasa? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swal hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jafo tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba ukiangalia katika kipindi cha karibuni Serikali imefanya investment kubwa sana katika maeneo hayo na hasa katika upande ule wa Maboma kuna takribani shilingi bilioni 38 kwanza zilitoka kwa ajili ya sekta ya afya awamu ya kwanza, lakini juzi juzi mwezi wa tatu hapa zilitoka karibuni shilingi bilioni 29.9 kwa ajili ya sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini, naomba nikuhakikishie kwamba mwezi wa nne hapa katikati tumetenga tena

karibuni shilingi bilioni 35.6 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba suala la sekta ya elimu kuhakikisha maboma mbalimbali yanatekelezaka.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo naomba nikutoe hofu Mheshimiwa Silinde kwamba Serikali ni nia yake kubwa kwamba kuhakikisha maeneo yote yenye changamoto yanaweza kufanyiwa kazi kwa lengo kubwa Watanzania wapate huduma vizuri. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante tunaendelea na Wizara hiyo hiyo swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata kwa niaba yake Mheshimiwa Mwambalaswa muulizie swali lake. (*Makof*)

Na. 392

**Serikali Kutengeneza Barabara ya Kibaya – Urughu,
Urughu – Mtekente - Ndago**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. MARTHA
M. MLATA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga vizuri barabara za Kibaya - Urughu, Urughu – Mtekente na Mtekente – Ndago zilizopo Wilayani Iramba ili kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa eneo hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Kandege tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara za Kibaya – Urughu, Urughu – Mtekente – Kisonga na Mtoa – Kisonga – Ndago

yenye urefu wa kilometra 61.46 zimekuwa zikifanyiwa matengenezo kwa nyakati tofauti ili kuhakikisha zinapitika nyakati zote.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 barabara ya Kibaya – Urughu ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa urefu wa kilometra 16 kwa gharama ya shilingi milioni 40.8 na pia barabara ya Mtoa – Kisonga – Ndago ilifanyiwa matengenezo ya muda maalum kwa urefu wa kilometra sita na makalвати matatu yaliјengwa. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 barabara ya Urughu – Mtekente – Kisonga ilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa urefu wa kilometra 12.5 kwa gharama ya shilingi milioni 53.3.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya shillingi milioni 188.8 zimetengwa kwa ajili ya kujenga *box culvert* kubwa la midomo miwili katika Mto Mtekente, kazi ya ujenzi imeanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2019. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 kuititia *TARURA* barabara ya Urughu – Mtekente – Kisonga imetengewa kiasi cha shilingi milioni 224.3 kwa ajili ya ujenzi wa *box culvert* kubwa katika Mto Kisonga na barabara ya Mtoa – Kisonga – Ndago imetengewa kiasi cha shilingi milioni 18 kwa ajili ujenzi wa kufanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa urefu wa kilometra sita.

SPIKA: Mheshimiwa Mwambalaswa uliza swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa Serikali kuvifanyia matengenezo barabara zote ambazo zimeulizwa kwenye swali hili, lakini kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019, barabara ya Kibaya Urughu imeharibika sana kwa sababu ya mvua, je, Serikali inasema nini kuhusu matengenezo ya barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, Swalii la pili barabara zilizopo katika Jimbo la Mheshimiwa Mlata Singida zinafanana sana na barabara za Wilaya ya Chunya, bahati mbaya kwa miaka miwili mfululizo huko Chunya, *TARURA* hawajafanya kazi yoyote kuzitengeneza barabara za vijiji, hasa hasa barabara ya kutoka Chunya kwenda Soweto; Isenyela kwenda Sangambi; Kiwanja kwenda Ifumbo; Chunya kwenda Mapogolo; Lupa kwenda Lualaje; Chunya kwenda Sangambi, lakini kubwa kuliko zote barabara ya kutoka Sangambi kwenda Chunya ni mahandaki haipitiki kabisa, je, Serikali inasema nini kuhusu matengenezo ya barabara hiyo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Spika, katika swalii lake la kwanza anaongelea eneo la Urughu ambalo barabara imeharibika kutokana na mvua nydingi ambazo zimenesha, ni ukweli usiopingika kwamba pale ambapo mvua zinanyesha nydingi na hasa katika barabara ambazo zinatengeneza kwa kiwango cha vumbi ni uhakika kwamba kunakuwa na uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukawasiliana na Mheshimiwa Mbunge ili tukajua ukubwa wa tatizo ili tuweze kutoa maelekezo kwa *TARURA* ili matengenezo ya dharura yaweze kufanyika ili barabara hii iendelee kupitika kipindi chote, wananchi waendeelee kupata huduma na kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, lakini anaongelea katika jimbo lake ambalo anasema linafanana sana na swalii la msingi na anaeleza kwamba katika jimbo lake *TARURA* hajafanya kazi yoyote kwa mwaka mzima. Hali kama hii hatujaipata pahali pengine popote, ni vizuri tukawasiliana na Mheshimiwa Mbunge tukajua hasa nini ambacho kimetokea hadi barabara isitengenezwe na hali bajeti imekuwa ikitengwa.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mwigulu Nchomba.

MHE. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibaya, Urughu - Mtekente - Mtowa na Sheluwi ni moja ya barabara inayobeba uchumi wa Iramba na katikati ya Mtekente na Mtowa pana daraja la kisasa sana limejengwa.

Je, kwa nini Wizara ya Ujenzi isiiipandishe barabara hii kufuatana na umuhimu wake ili iwe chini ya *TANROADSiweze* kujengwa kwa kisasa na iweze kusaidia wananchi hawa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli Waheshimiwa Wabunge watakulaliana na mimi kwamba tumekuwa na chombo hiki *TARURA* na dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba *TARURA* inafanya kazi nzuri na kweli nitumie nafasi hii niwapongeze *TARURA* kwa sababu wameanza vizuri maeneo mengi, wanafanya vizuri na kumekuwa na mchakato wa kuzitambua barabara zetu kwa nia dhabiti ya kuweza kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kupandisha barabara uko kisheria na kama saa nyngine itapendeza watumie nafasi hiyo kwa vikao walivyonavyo ili waweze kuleta mapendekezo na sisi kama Serikali tutazama kwa namna hiyo kwa mujibu wa taratibu zillizokuwepo ili kama itakidhi kupandishwa basi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atafanya hivyo. Lakini kimsingi ni kwamba *TARURA* ipo kwa ajili ya kuboresha barabara zetu na nifahamishe tu kwamba itaenda kujenga barabara zetu mpaka kiwango cha lami.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sokombi.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Spika, tatizo lililoko Iramba halina tofauti na tatizo lililoko katika Mkoa wa

Mara hasa barabara ya Musoma - Busekela ambayo ilitengewa kilometra 42 lakini cha ajabu barabara hii iliyojengwa ni kilometra tano tu. Ninachotaka kujua hizi kilometra 37 zitajengwa lini? Ahsante.

SPIKA: Lini zitajengwa? Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa kutambua umuhimu wa barabara hii anayozungumza Mheshimiwa Mbunge tumeanza kufanya ujenzi wa kilometra tano na hii tunazingatia kwamba yale maeneo ambayo ni korofi tunaanza kuyawekea lami na hivyo hivyo maeneo yote nchi nzima kwamba tunapokuwa na utaratibu wa kujenga barabara zetu yale maeneo ambayo tunaona kwamba ni muhimu tuyaboreshe tunaanza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza nimuombe Mheshimiwa Mbunge aridhike kwamba tumeanza kuchukua hatua nzuri ili kufanya ujenzi kwenye maeneo ambayo tunaona kwamba ilikuwa ni muhimu tuyaboeshe na tutaendelea kufanya hivyo. Tukipata fedha za kutosha tutakwenda kujenga barabara hii yote, kwa hiyo, uvute subira hatua ndio hivyo tumeanza kidogo lakini kadri tunavyopata fedha tutakwenda kuiboresha barabara hii na tutaendelea kuboresha maeneo yote ambayo yanaleta usumbu kwa wananchi wakati wanasubiri barabara ya lami yote ijengwe basi waweze kupita na kufanya shughuli zao za maendeleo, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mbaraka Kiwana Dau, tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii, Mbunge wa Mafia.

Na. 393

Watalii Walitembelea Kisiwa cha Mafia 2017/2018

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Je, ni watalii wangapi walitembelea Kisiwa cha Mafia kwa mwaka 2017/2018?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, tafadhalii

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kisiwa cha Mafia ni moja ya eneo la kimkakati katika uendelezaji wa utalii wa fukwe nchini. Katika miaka ya karibuni kisiwa hicho kimekuwa kikitembelewa kwa wingi na wageni mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi. Wageni hao wamekuwa wakivutiwa na vivutio mbalimbali vinavyopatikana katika kisiwa hicho ikiwemo papa potwe, magofu ya kale, utamaduni wa fukwe nzuri. Aidha, watalii wamekuwa wakivutiwa na michezo ya kwenye maji (*scuba diving, sport fishing and snorkelling*) na kuongelea na samaki aina ya papa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzuri wa Kisiwa cha Mafia idadi ya wattii wanaotembelea kisiwa hicho imeendelea kuongezeka ambapo katika mwaka 2017/2018 jumla ya watalii 5,412 walitembelea Kisiwa cha Mafia hususani katika Hifadhi yetu ya Bahari ya Hindi katika eneo la Kisiwa cha Mafia (*Marine Park and Reserve-Mafia*). Kati ya watalii Watanzania walikuwa 252 na wageni walikuwa 5,160. Idadi hii ya watalii walitembelea Mafia ni sawa na ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na watalii 4,817 walitembelea kisiwa hicho katika msimu wa mwaka 2016/2017. Katika kuhakikisha kuwa Kisiwa cha Mafia kinafikika kwa urahisi, Serikali inaendelea na mikakati ya kuboresha miundombinu ya kisiwa hicho ikiwa ni pamoja na kujenga meli na kuboresha maegesho ya meli katika Bandari ya Nyamisati na Mafia.

Mheshimiwa Spika, namsihi Mheshimiwa Mbunge aunganishe nguvu kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya

umma na binafsi wa Wilaya ili kuboresha miundombinu itakayosaidia kukuza sekta ya utalii katika Kisiwa cha Mafia kuktangaza zaidi ndani na nje ya nchi na kuhamasisha uwekezaji.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mafia Mbaraka Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri isipokuwa nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamoja na uzuri na vivutio vyote hivi vya utalii alivyovisema Mheshimiwa Naibu Waziri, Kisiwa cha Mafia hakijawahi kuonekana kwenye *channel* ya utalii inayoonyeshwa katika Azam. Sasa je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atawaelekeza wahusika wa vipindii hivyo waje kufanya *shooting* pale Mafia na vivutio vile viweze kuonekana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Serikali inajitahidi kuimarisha miundombinu ya kuingilita Mafia ili kuweza kupata watalii wengi zaidi. Tunaishukuru Serikali imetupatia boti ile ya *DMI* ambayo kwa sasa inamaliziwa matengenezo pale, lakini imekwama kupata kibali cha *TASAC* kutokana na matatizo ya hitilafu za kiufundi na kuna matatizo ya kibajeti ya Chuo cha *DMI*.

SPIKA: Swali Mheshimiwa?

MHE. MBARAKA K. DAU: Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano mtaweza kuwasiadua Chuo cha *DMI* matatizo yao ya kibajeti ili waweze ili waweze kulipia boti ile na iweze kuja Mafia?

SPIKA: Ahsante sana umeelewaka, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba lengo la kuanzishwa kwa *channel* ya utalii ni kuhakikisha kwamba inatangaza vivutio mbalimbali vilivyopo katika nchi yetu katika maeneo yote na maeneo hayo ni pamoja na Kisiwa cha Mafia. Lakini naomba nikiri kwamba *channel* hii imeanzishwa tu, haina muda mrefu na uandaaji wa vipindi hivi ni unahitaji gharama na pesa nyingi na nchi yetu ni kubwa, bado hatujamaliza kuandaa vipindi, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kisiwa hiki ni maeneo yetu ya kimkakati ambayo tumeyaweka kwa ajili ya kuhamasisha utalii na nimechukua pamoja na maombi yake lakini ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba watu wetu wanaoandaa vipindi kupitia *TBC* wanakwenda katika eneo hili kuvitambua na kuvirekodi vivutio vyote vya utalii na kuvitangaza.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na kwamba haijaonekana tutahakikisha kwamba tunatoa maelekezo kisiwa hiki kiweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, kwanza naomba nimshukuru kwa kuipongeza Serikali kuboresha miundombinu mbalimbali hasa uwanja wa ndege ambao Mheshimiwa Mbunge amesahau kusema kuna uwanja wa ndege bora kabisa pale Mafia na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba boti hii ambayo imekwama kwa masharti machache pale *DMI* nitashirikiana na wenzangu wa Wizara ya Uchukuzi kuhakikisha kwamba taratibu zinakamilishwa ili boti hii iweze kuanza kutoa huduma na kupeleka watalii katika Kisiwa cha Mafia, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Sware nimekuona.

MHE.DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kisiwa hichi cha Mafia ni eneo nyeti sana sio tu kwa ajili ya shughuli za utalii bali pia ni eneo ambalo linatulishia samaki, mazalia ya samaki katika

bahari yetu. Sasa kwa kuwa ni kisiwa kiko *strategic* Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa nini sasa isikae na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na TAMISEMI kuleta mkakati mahususi wa kuwezesha shughuli za wananchi katika maeneo haya ya Mafia ambao wako duni sana na *majority* ni wavuvi, wainuliwe kiuchumi na kuweza kuinua utalii pamoja na shughuli za uvuvi ili kuinua zaidi uchumi wetu kwa ujumla nchini?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Constantine Kanyasu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba maeneo ya Kisiwa hiki cha Mafia ni maeneo ambapo kwanza kuna visiwa vingi, lakini maeneo yenye wavuvi wengi, lakini ni maeneo ya mazalia ya samaki na baadhi ya maeneo haya ambayo nilmeyataja kwamba yako chini ya *marine park* ni maeneo yanayohifadhiwa kwa ajili ya mazalia ya samaki pia ndipo ambapo utalii wa kuzamia majini unafanyika na ndipo ambapo kuna akiba ya *under water cultural heritage* nyingi ambazo ziko maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu suala hili ni *cross cutting* linahitaji pengine kujadiliwa na wizara nyingi mbalimbali. Tumechukua wazo lake lakini nimhakikishie kwamba mpaka wavuvi na wananchi katika maeneo hayo wanaandaliwa vizuri ili kuhakikisha kwamba wanafaidika na uwepo wa shuguli za uvuvi pia na uwepo wa shughuli za utalii katika maeneo hayo.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Jerome Bwanausi uliza swali lako.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uwepo wa mamba pia ni sehemu ya kivutio kwa watalii lakini kutokana na ongezeko

kubwa sana mazalio ya mamba katika Mto Ruvuma na kuleta athari kubwa sana kwa wananchi.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja kwenye Jimbo langu kuona athari kubwa zinazojitokeza na kutafuta changamoto za kutatua tatizo hilo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo kuhusu utalii wa mamba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba limekuwepo ongezeko kubwa sana la mamba katika maeneo yetu mengi mamba, boko na wanyama wengine ambao hawatumiki moja kwa moja sana na kuhamasisha utalii na katika eneo hili la Mto Ruvuma ambalo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akisema wamesababisha shughuli za uvuvi na shughuli za matumizi ya maji ya kawaida ya Mto Ruvuma kushindikana.

Mheshimiwa Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyomjibu hivi karibuni kwenye swali lake la msingi kwanza tulielekezwa watu wetu wa *TAWA* kuhakikisha kwamba wanapeleka visima vya maji karibu katika vijiji ambavyo viko karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pili, tuliwaagiza watu wetu wa *TAWIR*/kufanya utafiti na kutueleza mamba waliopo wamezidi kwa kiasi gani ili tuweze kuweka mkakati wa kuwavuna, lakini nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kwenda katika eneo hilo kwenda kuangalia hali halisi na kuzungumza na wananchi.

SPIKA: Tunaelekea Wizara ya Nishati Waheshimiwa Wabunge, swali linaulizwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer Mbunge wa Monduli.

Na. 394

Ahadi ya Umeme wa REA Katika Jimbo la Monduli

MHE. JULIUS K. LAIZER aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* kama ilivyoahidi katika vijiji vya Munjere, Baraka, Mbaasha, Lepurko, Mti Mmoja, Arkatan, Arkaria, Mfereji, Ndonyonaado, Mswakini, Naitolia, Emurua, Lashaine, Orkenswa, Engaaroji, Oldonyolengai na Naalarami?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Shule ya Sekondari Oldonyolengai ambayo laini imefika tangu mwaka 2015 lakini mpaka sasa umeme haujawaka?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Subira Hamis Mgusu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) imedhamiria kufikisha ueme katika vijiji vyote visivyo na umeme nchini ifikapo mwezi Juni 2021. Kuligana na mpango wa kupeleka umeme katika vijiji 64 Wilayani Monduli vijiji 16 vilishapatiwa umeme vikiwemo vijiji vya Arkatani na Mti Mmoja ni mionganoni mwa vijiji vya Wilaya ya Monduli vilivyopata umeme kupitia awamu ya pili ya mradi wa kusambaza umeme Vijiji (REA II). Aidha, vijiji vya Arkaria, Lepurko na Mbaasha vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 48.75 na njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4

yenye urefu wa kilometra 40 na ufungaji wa transfoma 20. Jumla ya wateja wa awali 720 wataunganishiwa umeme na gharama za mradi ni shilingi bilioni tatu. Mradi unatarajija kukamilika mwezi Juni, 2020.

Vijiji vingine vya Munjere, Baraka Mfereji, Ndonyonaado, Mswakini, Naitolia, Emurua, Lashaine, Orkenswa, Engaaroji na Naalarami vitapata umeme kupitia *REA* /// mzunguko wa pili utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

(b) Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Oldonyolengai iliyopo Kata ya Engaruka imeshapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* /// mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa Wilayani Monduli.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Monduli.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na kwa kweli nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri kwa sababu katika Wilaya ya Monduli vijiji vilivyokuwa vimepatiwa umeme peke yake vilikuwa 16 na sasa karibu vijiji vyote 64 vitaingizwa kwenye awamu ya tatu. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tatizo kubwa la *REA* katika maeneo mengi ni kwamba umeme unafika kwenye kijiji lakini vitongoji na maeneo mengi ya wananchi umeme ule haufiki.

Je, nini mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo umeme haujafikia japo inaonekana kijiji kimefikiwa umeme unaweza kupelekwa kwa wananchi kuliko kuwa na umeme ambao umefika kijijini lakini wananchi hawajapata umeme?

Mheshimiwa Spika, swali la pili katika Kata ya Engaruka katika Shule ya Oldonyolengai tayari laini kubwa imefika ni kazi ya kuunganisha tu katika shule ya msingi Engaruka Juu

na katika zahanati ya Oldonyolengai. Je, nini kauli ya Serikali kwa mkandarasi aliyoko *site* ili aweze kuunganisha umeme katika maeneo hayo?

SPIKA: Majibu wa maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Julius na kwa niaba yake napokea pongezi zake kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Mkoa wa Arusha na maeneo mbalimbali na pia nimpongeze Mheshimiwa Julius kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya katika jimbo lake la Monduli.

Mheshimiwa Spika, kama alivyouliza na nakiri ndani ya Bunge lako kweli miradi hii ya umeme inayoendelea *REA* awamu ya tatu au na *REA* awamu mbalimbali kazi yake ya msingi ya kwanza ni kufikisha miundombinu ya umeme mkubwa katika baadhi ya maeneo kwenye vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo na ndio maana Serikali yetu ya Awamu ya Tano imebuni mradi wa ujazilizi awamu ya kwanza ambao ulifanyika katika mikoa 8 na tumepata mafanikio makubwa wateja takribani 30 wamepatiwa umeme katika vijiji 305. Mpango unaoendelea sasa hivi ni Ujazilizi Awamu ya Pili A kwenye mikoa tisa ikiwemo Mkoa wa Arusha pia Mkoa wa Mwanza, manispaa za llemtela na Nyamagana na maeneo mbalimbali. Sambamba na hilo katika mradi huu wa *REA* wa Ujazilizi Awamu ya Pili takribani Bunge lako tukufu limetupitishia pesa shilingi billioni 169 ambayo inaenda kuwezesha wateja wa awali 60,000 kuunganishiwa umeme.

Kwa hiyo, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa bajeti imeshapita tunawaahidi kwamba tutaendelea kuismamia ili vitongoji vyote viendelee kuunganishwa lakini kwa kweli kazi kubwa kwanza ni kufikisha umeme katika maeneo ya makao makuu ya vijiji kasha usambazaji ni jambo endelevu. Pia naomba niseme taarifa ya ziada tumeielekeza

TANESCO wamebaini maeneo 754 ambayo yamepitiwa na miundombinu ya umeme mkubwa na pale kazi kubwa itakuwa ni kuweka transfoma na kushusha huo umeme na kwa kuwa tumeamua *TANESCO*, *REA* yote ishambulie na ndio maana Serikali imefanya maamuzi ya makusudi ya kisera kufanya kwamba bei ya kuunganishia umeme 27,000.

Mheshimiwa Spika, naomba nikutaarifu na Bunge lako juzi tulikuwa na mukutano mkubwa na tutaanza kuzindua wateja wanaounganishwa kwa bei shilingi 27,000 na tunaanza Wilaya ya Kondoa wameshaunganishwa wananchi 500 baada ya uamuzi wa Serikali. Kwa hiyo, niwatoe hofu wananchi wote na vitongoji ambavyo hawajaguswa.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili, ameelezea masuala ya kwa kuwa laini kubwa imefika katika Kata ya Engaruka, ameuliza; Serikali inatoa maelekezo gani kwa mkandarasi ambaye ni *NIPO Group* aliyeko katika Mkoa wa Arusha. Juzi mukutano wetu baina ya *REA* na *TANESCO* tumeendelea kutoa msisitizo umuhimu wa kuunganisha taasisi za umma katika miradi inayoendelea.

Kwa kuwa *TANESCO* tumeipa mamlaka sasa na wao kuendelea kusambaza umeme vijijiini kwa bei ya shilingi 27,000 na kwa kuwa imetenga shilingi bilioni 40 na Bunge mmeidhinisha ni wazi maeneo haya ya taasisi za umma yatafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *REA* na *TANESCO* wataendelea kushambulia maeneo mbalimbali ili kukamilisha na watanzania wapate fursa ya kutumia umeme kwa bei nafuu ikiwa ni azma ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano. Ahsante sana.

SPIKA: Kwa majibu hayo Waheshimiwa hakuna haja ya maswali ya nyongeza, tunaendelea. (*Kicheko*)

Mmeambiwa *REA* na *TANESCO* wanashambulia kwa mpigo, ondoeni hofu. Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa Kusini uliza swalii lako.

Na. 395

Kushamiri kwa Uvubi Haramu - Kilwa

MHE. SELEMANI S. BUNGARA aliuliza:-

Uvubi haramu unazidi kushamiri siku hadi siku hasa kwenye maeneo ya Songosongo, Somanga, Njianne, Kivinje hadi Pwani ya Bushungi. Aidha, maeneo haya kuna bomba la gesi linapita na hivyo kujenga hofu ya uwezekano wa mlipuko pamoja na uharibifu wa mazingira kwenye maeneo tajwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti kukabiliana na tishio hilo sugu?

(b) Kwa kuwa wanaofanya hujuma hizo wamejiandaa kwa kuwa na boti maalum katika kuendesha huduma hizo; je, Serikali haioni haja ya kuleta boti za doria zenyet uwezo wa hali ya juu ili kulinda bahari na bomba la gesi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvubi, majibu tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvubi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na uvubi haramu, Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuanzisha vituo vya doria kwenye maziwa makubwa, mwambao wa Bahari ya Hindi na mipaka ya nchi. Imeanzisha Kikosi Kazi cha Kitaifa (*Multi Agency Task Team*), ambacho kinafanya kazi ya kudhibiti uhalifu wa mazingira ikiwemo kudhibiti uvubi haramu hususan matumizi ya mabomu katika shughuli za uvubi. Kufanya opereshini za mara kwa mara mfano Operesheni Jodari kwenye Ukanda wa Pwani na

Operesheni Sangara, Ziwa Victoria, kuanzisha na kuimarisha vikundi vyatya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi (*BMU*) pamoja na kufanya maboresho ya Sheria na Kanuni za Uvuvi ili kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi hapa nchini. Juhudi hizi zimezaa matunda hususan katika Ukanda wa Pwani ambapo uvuvi wa kutumia mabomu kwa maana ya milipuko umepungua kwa takribani asilimia 99.

Mheshimiwa Spika, Serikali itendelea kupambana na tatizo la uvuvi haramu hususan wa mabomu kwa kuhakikisha vituo vyatya doria vinapatiwa vitendea kazi ikiwemo boti za kisasa ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi na miundombinu ya gesi kwa faidi ya kizazi cha sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuiunga mkono Serikali yao kwa kukemea na kupiga vita uvuvi harama katika maeneo yao.

SPIKA: Mheshimiwa Said Bungara swali la nyongeza tafadhali.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu swali langu vizuri kabisa na nakiri kabisa kwamba asilimia 99 ya walipuaji wa mabomu umefikia. Juhudi hizi nakumbuka Mheshimiwa Naibu Waziri alivyokuwa Mbunge, alivyokuwa Mkuu wa Wilaya kule Kilwa tulishirikiana na mimi kutembea Wilaya ya Kilwa nzima kuelimisha ulinzi shirikishi wa *BMU* na matokeo yake *BMU* ndiyo imesababisha kupungua kwa milipuko hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudihizo kuna viongozi wa Wilaya ya Kilwa, Diwani wa Kata ya Kivinje na *DAS* wa Wilaya ya Kilwa wanawafuatalia sana hawa viongozi wa *BMU* na kufikia hatua ya kuwashtaki kwa kutekeleza jambo hili la kusimamia *BMU* kwa uhakika na wakafkishwa mahakamani, lakini Mwenyezi Mungu wakashinda kesi.

SPIKA: Uliza swali lako sasa Mheshimiwa Bungara.

MHE. SULEMAN S. BUNGARA: Je, hauoni hawa viongozi wa Wilaya ya Kilwa wanawakatisha tamaa wananchi wa Kilwa? Moja hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili katika Operesheni Jodari wananchi wa Kilwa walichomewa moto nyavu zao nyingi sana, lakini kwa mimi ninavyoona kwamba walionewa kwa sababu kwa mujibu wa kitabu cha...

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, bado swali langu.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, swalilangu la pili bado.

SPIKA: Tayari tayari tayari.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, nakuomba, nimeulizaje?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, nimeulizaji?

SPIKA: Tayari tayari. (*Kicheko*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, hili la pili nimeulizaji? (*Kicheko*)

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa

Selemani Said Bungara maarufu kama Bwege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Bungara kwa pongezi alizozitoa kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi pale alipotoa ushuhuda wa namna ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa ya usimamizi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia mabomu, shukrani kwa kuwa muungwana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Bungara analalamika kuwa kuna viongozi wa Serikali wanakatisha tamaa wananchi na akamtaja Diwani mahiri kabisa wa Kata ya Kivinje Mheshimiwa Jafar Arobaini na *DASwa Kilwa*.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nijibu maswali haya kwa kusema kuwa nina mfahamu vyema Mheshimiwa Diwani Jafar Arobaini, ni mtu makini, na mtu mchapa kazi, mtu hodari, mzalendo, nina hakika kuwa hawezi kuwa kinyume na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo yeye ni Diwani wake. Kama itathibitishika ya kuwa wako viongozi wa *BMU* ambao wamefanya vitendo kinyume au yuko kiongozi yejote wa Serikali aliyetenda kinyume sisi kama Wizara na Serikali kwa ujumla tuko tayari kwa hatua zetu za kinidhamu, kuchukua hatua na kufanya kazi mambo haya.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili anasema juu ya nyavi zilizochomwa pale Kilwa, nyavi hazikuchomwa Kilwa peke yake; nyavi zimechomwa kote katika nchi maeneo ambayo yameonekana nyavi zile ziko kinyume cha sheria. Tumefanya hivyo katika eneo la bahari, tumefanya hivyo na tutaendela kufanya hivyo endapo tu watu watatumia nyavi zisizokuwa halali kwa ajili ya kulinda rasilimali za Taifa letu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, tunaendelea na Katiba na Sheria swali muhimu sana la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi. Mheshimiwa Silafu tafadhali.

Na. 396

Mirathi kwa Wagane na Wajane

MHE. SILAFU J. MAUFI aliuliza:-

Mgane anapobaki na watoto hundi zinazolipwa kama kuna malipo huandikwa kwa jina lake, lakini kwa wajane huwa ni tofauti, anapewa masharti ya kulipiwa mahakamani na awe na muhtasari wa kikao cha upande wa mwanaume na ndipo malipo yafanyike kwa mgao maalum.

(a) Je, kwa nini mjane asiandikwe jina lake kwenye hundi na asimame na watoto wake kwa kupewa haki hiyo?

(b) Je, Serikali haloni kama inamnyanya mjane?

(c) Kama ni sheria; je, Serikali haionti kwamba ni wakati wa kuiangalia upya sheria hiyo?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silafu. Mheshimiwa Waziri Katiba na Sheria majibu kwa swali hili muhimu sana la wajane na wagane.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: *TWPG* tusikilizane, swali lenu hili.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala ya mirathi yanasisi mamiwa na Sheria ya Mirathi, Sura ya 352. Sheria hii inatoa utaratibu mzima unaohusu masuala yote ya mirathi, wosia, kufungua

mashauri ya mirathi, usimamizi, pingamizi la msimamizi au msimamizi anapofariki au asipotendewa haki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, sheria za nchi zinatambua kuwa mirathi na usimamizi wake unaweza kuongozwa na Sheria ya Kiislam au Sheria ya India ya mwaka 1885 kwa wasiokuwa waislamu. Matumizi ya sheria hizi yanaangalia maisha ya marehemu, dini na namna marehemu alivyozikwa. Pia sheria hizi zinaeleza namna mali itakavyopaswa kugaiwa kwa wanufaika huku ikainisha kila mnufaika kwa kiwango anachopata.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inajali na kutambua kuwa binadamu wote ni sawa na hii imeelezwa katika Ibara ya 12(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara ya 13(2) ya Katiba inatoa marufuku kwa sheria yoyote kuweka shauri lolote lile la kibaguzi katika matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo hakuna sheria yoyote inayompa mgane haki zaidi mjane au kwa namna yoyote kuonesha ubaguzi. Hata hivyo, utaratibu unaofanyika unatamka msimamizi wa mirathi kuwasilisha mchanganuo wa malipo na hundi huandikwa kwa wanufaika wote pasipo kujali jinsia zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na sheria nzuri, kumekuwa na uelewa mdogo mionganoni mwa baadhi ya wananchi kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazohusu masuala ya mirathi. Wizara yangu kupitia *RITA* na wadau mbalimbali imekuwa ikitoa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu mirathi na maendeleo na kubuni mbinu zitakazosaidia ili elimu ya mirathi iwafikie wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote tushirikiane katika kuchangia jitihada za Serikali katika kufikisha elimu ya mirathi kwa wananchi wetu katika maeneo yetu yanayotuhusu, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali Serikali imesema hakuna ubaguzi wowote.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa majibu mazuri katika swali langu namba 396, lakini kutoakana na mfumo dume tulionao katika nchi yetu ya Tanzania, hizo sheria kihalisia hazitekelezeki ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba elimu hajjawafikia wananchi wetu na hususan akina mama wenzangu ndiyo wanaonyanyasika sana na sheria hizi, inapofika wakati wa mirathi mama anakosa kupata haki iliyokuwa sahihi. Ifahamike wazi ya kwamba Wizara inasema inapitia *RITA*, hiyo *RITA* huenda ikawa iko Dar es Salaam, lakini katika Mkoa wa Rukwa na Mikoa mingine *RITA* hiyo haipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuuliza swali langu; je, Wizara au Serikali ipo tayari kuweka mkakati maalum wa kutoa mafunzo endelevu na hasa kwa kina mama kuelewa haki zao katika kuhakikisha kwamba wanatimiziwa haki zao? Kwa sababu wanahitaji uwakilishi wa sisi Wabunge ni dhahiri kusema ya kwamba... (*Makofi*)

SPIKA: Sasa swali.

MHE. SILAFU J. MAUFI: ...hata Wabunge elimu hiyo hawana; je, wako tayari Serikali kutoa mafunzo hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wanawake hawa wajane wamekuwa ni wengi, wanaume wagane ni wachache kwa sababu mwanaume mgane ni wa dakika mbili baada ya muda anaweka mke mwingine ndani, kwa hiyo, anakuwa siyo mgane tena, lakini mjane anaendelea kuwa mjane. (*Makofi*)

Kwa kuwa wako wengi na wako katika makundi mbalimbali; je, Serikali inaona mkakati gani wa kuwawekea mpango wa kuwawezesha kimkopo ili kina mama hawa

waweze kujendeleza na kuhudumia familia zao? Naomba majibu hayo. (*Makofi*)

SPIKA: Hili ndiyo swalii la siku hili, kwa siku ya leo ndiyo swalii hilo. Mheshimiwa Waziri semina kwa Wabunge Wanawake, lakini ni kweli wagane ni wachache kuliko wajane? (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Ndiyo!

SPIKA: Majibu Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, mimi naungana mkono na mama, kwa kweli katika utekelezaji wa sheria hizi hasa za mirathi akina mama wamekuwa siyo tu wanasumbuliwa, lakini wanabaguliwa. Tatizo hili linajionesha kadri tunavyokuwa mbali na mijji hasa kwa akina mama walioko vijijini. Ni kweli kwamba katika mfumo dume, zile mali mara nyingi ziko chini ya mwanaume na wanawake inapokuja kwenye mirathi wanawekwa pemberi au ndugu wa yule aliyefariki mwanaume wanamnyanyasa yule mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaona umuhimu na ninakubaliana na wewe kwamba *RITA* ipewe jukumu kubwa la kuelimisha wananchi wote kwa ujumla, naomba mashirika mbalimbali ya akina mama tushirikiane katika kueneza elimu hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nakubaliana kwamba mbali na elimu hizi za vipeperushi au machapisho kuna haja ya kuwa na mkakati maalum, mkakati ambao hata Wizara yangu, Majaji, Hakimu watakuwa wanaelezwa na kushirikiana na utawala kwa ujumla katika Mikoa na katika Wilaya. Pendelezo hili na jinsi liliyoungawa mkono hapa nitalipa kipaumbele katika Wizara yangu, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge swalii hili ni muhimu sana kwa *TWPG*. Hebu kwa mikutano mitatu ili yobaki ninyi Wabunge Wanawake wote m-sponsor

(mdhamini) muswada fulani wa kwenu wenyewe, rekebiseni haya mambo, msisubiri Serikali peke yake. Tumieni njia mbalimbali zilizoko katika kanuni zetu, hebu fanyeni jambo moja la wanawake, kwa mfano iwe ni marufuku katika nchi yetu mama na familia kufukuzwa katika nyumba ya familia. Kwa mfano tu au mambo haya ya mirathi wanahangaika kweli, wanateseka na ninyi ndiyo Wabunge wao. Katika miaka mitano mme-sponsor nini cha kubadilisha hali yao au itaisha hivi hivi tu! Viti Maalum, tufanye kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Saed Kubenea.

Na. 397

**Wanasheria Wote wa Kwenye Mashirika ya Umma
Kuwa Chini ya AG**

MHE. SAED A. KUBNEA aliuliza:-

Serikali ilitangaza kuwa wanasheria wote walioko kwenye mashirika ya umma watafanya kazi chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi na kuwapa ufanisi kwenye ufuatiliaji wa kesi zinazofunguliwa dhidi ya Serikali.

(a) Je, utekelezaji wa agizo la Serikali kuhusu mawakili binafsi kutosimamia kesi za Serikali limefikia wapo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichoookolewa tangu mashirika ya Serikali yaache kutumia mawakili wa nje?

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali yaliyofanywa kuitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2018 yaliyopitishwa na Bunge lako tukufu, yaliwezesha kufanya wanasheria wote katika utumishi wa umma kuwa chini ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Mabadiliko hayo yalitokana na Tangazo la Serikali Na. 50/2010 lilitambua kuwepo kwa Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali ambayo amepewa jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya madai ambayo Serikali inashtaki au inashtakiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kuitia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali tayari imeshatoa maelekezo kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali kuwasilisha mashauri yote ya madai dhidi ya Serikali katika Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali kwa ajili ya uratibu, usimamizi na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezeshaji wa Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali kwa sasa mashauri yote ya madai dhidi ya Serikali yanasmamiwa na ofisi hii isipokuwa kama itaonekana kuwepo kwa ulazima wa kuhusisha mawakili binafsi. Hii hutokea iwapo mashauri husika yamefunguliwa katika mahakama za nchi za nje zisizokuwa za Kimataifa ambazo kwa baadhi ya nchi sheria zake za ndani na taaluma ya uwakili haziruhusu mawakili wa nchi nyingine kufanya shughuli za uwakili hasa uwakilishi mahakamani ndani ya nchi husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, inapotokea hitaji la kutumia mawakili binafsi, Mwanasheria Mkoo wa Serikali hulazimika kutoa kibali cha Serikali cha kuajiri Wakili kutoka ndani ya nchi hiyo itakayoshirikiana na Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali katika kusimamia uendeshaji wa shauri husika.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali kumesaidia kupunguza gharama zilizokuwa zinalipwa na wakili binafsi ambazo kwa tathmini ilifanyika uendeshaji wa kila shauri moja hapa nchini zilikuwa hazipungui shilingi 5,000,000 na kwa upandea mashauri

yaliyofunguliwa nje ya nchi gharama za kumlipa wakili kwa kila shauri ilikuwa hazipungui dola za Marekani 300,000 mpaka 2,500,000 kwa kila shauri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti 2019/2020 kwa mwaka 2018/2019 Serikali iliooka kiasi cha shilingi 9,018,957,011 ambazo zingelipwa kwa mawakili binafsi. Ninapenda kulithibitishia Bunge kuwa Serikali itaendelea kuokoa fedha nyingi zaidi ambazo zitasaidia kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea na kazi ya ukusanyaji wa mashauri yote ya madai kutoka kwa Wizara na Taasisi zote za umma/Serikali. Zoezi hili litakapokamiliika litasaidia kufanya tathmini ya kina na kupata thamani halisi ya fedha zilizookolewa na Serikali kuititia maboresho haya mapya. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kubenea tafadhali.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri yenye tija.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa baadhi ya mashirika ya umma yanaendelea kutumia mawakili binafsi katika kuendesha kesi am bazo imeshtakiwa na wadai. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mashirika ya umma na taasisi zake zinazoendelea kutumia mawakili binafsi katika kuendesha kesi za umma?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa moja ya malengo ya kubadilisha kuagiza kesi binafsi, kesi zilizoshtakiwa Serikali zisimamiwe na mawakili wa Serikali ni kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi. Sasa gharama za kuendesha kesi nchi za nje zimekuwa kubwa sana na sababu moja inayosababisha Serikali ishtakiwe nje ni pamoja na kuvunja mikataba kiholela.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inalipa wadai wote, wakandarasi wote ambao wamei-supply Serikali kwenye mikataba ya Kimataifa ili kuiondoa Serikali na mzigo mkubwa wa madeni na kushtakiwa nchi za nje? (*Makofii*)

SPIKA: Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Majibu ya maswali hayo tafadhali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kubenea.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, baadhi ya Mashirika ya Umma kuendelea kutumia mawakili binafsi hii inawezekana ni kwamba wakati maelekezo haya ya kesi zote kusimamiwa na Wakili Mkuu wa Serikali yanatolewa yale mashirika yalikuwa tayari yameshawa-*engage* wale *lawyers*, lakini kwa vyovyyote vile kwa sasahivi wanafanya kazi pamoja na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuanzia pale lilipotolewa lile agizo kwamba kesi zote za haya mashirika ya umma zisimamiwe na Wakili Mkuu wa Serikali hakutakuwa na kesi yoyote ambayo itasimamiwa tena na Mawakili binafsi isipokuwa katika mazingira ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaeleza. Kama iko kesi nje ya nchi na iko katika mahakama ambayo kuna taratibu ambazo haziwezi zikawaruhusu wanasheria wetu kusimama katika zile mahakama basi tutapata mawakili binafsi wa kusimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii la pili ambalo linagusa kesi mbalimbali zilizoko na zinazotokana na kuvunjwa kwa mikataba na kadhalika, nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa hivi tunao umakini mkubwa sana tunapoingia hii mikataba kiasi kwamba hatutaingia katika mazingira ya kuweza kushtakiwa kwa sababu ya kuvunja mikataba.

Kwa hiyo sasa hivi tunazingatia mambo yote ya muhimu, maslahi ya nchi na kadhalika na kuhakikisha kwamba mikataba yetu inategengenezwa vizuri kabisa kiasi

kwamba hatutakuwa na matatizo ya kesi hizi mbalimbali. Na kwa kesi ambazo ziko tayari kwa kiasi kikubwa tumeingia katika majadiliano na mashauriano tuone namna gani tunaweza tukazimaliza kesi hizo kwa njia ya mashauriano badala ya kuendelea na njia ya mahakama. Naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana, kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge, maswali mawili yaliyobaki tutayapanga katika wakati mwengine. Sasa niendelee na matangazo.

Wageni wetu katika Jukwaa la Spika ni pamoja na vijana kutoka Shule ya Msingi ya Wisuzaje, Kata ya Mtanana wakiongozwa na Diwani Mussa Chiwanga. Wanafunzi 40 na walimu watano, wale wa Wisuzaje, karibuni sana watoto wangu. (*Makofi*)

Lakini pia yuko Mheshimiwa Kuwayawaya S. Kuwayawaya aliyekuwa Mbunge wa Chilonwa kwa miaka mingi. Karibu sana Mheshimiwa Kuwayawaya, hujatutembelea muda mrefu sana. Ninyi ndiyo Wabunge ambaao mliweka misingi mikubwa katika Bunge hili, tunashukuru sana kwamba leo umepata fursa ya kuwa pamoja na sisi. Lakini mavazi yake yeye hupendeza siku zote, huwa ni mavazi mazuri sana. Karibu sana Mheshimiwa Kuwayawaya. (*Makofi*)

Wako wageni wa Mheshimiwa Nabu Spika kutoka Jijini Dar es Salaam ambaao ni *Managing Director* wa *Zumbe One Tanzania Limited* Ndugu Stanley Bendera, karibu sana, yuko *Director* wa *Zumbe One Arbogast Chiwembo*, karibu sana, yuko *Financial Manager Zumbe*, Suzana Urio, ahsante na *Katibu wa Vijana wa CCM* wa Wilaya ya Chamwino, karibu sana. (*Makofi*)

Wageni 11 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto kutoka Marekani ambaao ni ndugu Dannica Leigh, *those from the US, one after the other I will be mentioning your names get seated*. Dannica Leigh, David Scott, Thomas David, Levi

James, Mira Kathleen, Isaac Waterlmoreira. Wameongozwa na wenyiji wao ambai ni Josia Kizindo, Rachel Johnson, Azgard Steven na Godbless Kisanga, karibuni sana. (*Makof!*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni mgeni wa Mheshimiwa Selemani Jaffo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni mwalimu kutoka Bagamoyo Ndugu Timotheo Kasmiri. Karibu mwalimu popote pale ulipo. (*Makof!*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mwita Waitara, Naibu Waziri, TAMISEMI Ndugu Philemon Lameck, karibu sana. (*Makof!*)

Wageni 68 wa Mheshimiwa Mussa Mbarouk ambaao ni walimu na wanafunzi kutoka shule ya *Indian Ocean English Medium* ya Jijini Tanga, karibuni sana kutoka *Tanga Indian Ocean*. (*Makof!*)

Wageni 20 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Waziri wa Kilimo ambaao ni Makatibu Wenezi wa CCM Kata kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Ndugu Stephano Simbeye. Wenezi, karibu sana kutoka Vwawa. (*Makof!*)

Wageni 23 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga pia ambaao ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi *Top Layer* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalimu Iman Mwaipaja. *Top layer*, karibuni sana watotow etu. (*Makof!*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Allan Kiula kutoka Mkalama ambaye ni Katibu wa CCM wa Mkalama Ndugu Salum Shack na Diwani wa Kata ya Mkalama Mheshimiwa Florence Misayi, karibuni sana. (*Makof!*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambaao ni viongozi wa CCM wa Kata ya Mgandu Wilaya ya Manyoni, Mkoani Singida wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Mgandu Ndugu Lameck Mwamkamba, karibuni wale wa kutoka Mgandu. (*Makof!*)

Wageni 57 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaao ni Maaskofu, Mapadri na *Mediators* wa Dodoma na nje ya

nchi. Wageni wale wa Mheshimiwa Anna Lupembe karibuni sana Mababa Askofu, Wachungaji na wageni wote kutoka ndani nan je ya nchi. Basi msisahau kuwa mnatuweka katika maombi. Ahsanteni na karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 49 wa Mheshimiwa Lolesia Lukwimba ambao ni kwaya ya *Kingdom* na *DCC* kutoka Kanisa la *Winning Faith* la Kisasa, Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana, kwaya mmependeza kweli kweli. Eneo hili la *gospel*/hili Tanzania tuko juu sana, hata nchi jirani zote ukienda unakuta nyimbo za *gospel* za Tanzania zipo, iwe Nairobi, Kampala, Kigali, Bujumbura mpaka Kinshasa kule, Zambia pia ziko. Hongereni sana. (*Makofi*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mafinga wakiongozwa na Ndugu Kisina Nelson, *UDOM* Mafinga, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa *Engineer Gerson Lwenge* ambao ni Kwaya ya Tumaini ya KKKT Illembula kutoka Wanging'ombe Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Mchungaji wa Usharika wa Illembula, Mchungaji Geofrey Mtweve. Illembula, karibuni sana. Mmesafiri kutoka mbali karibuni sana Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni viongozi wa Chama cha Mawakala wa Forodha Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Edward Uri. Ahsante karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Kemilembe Lwota ambao ni jamaa zake kutoka Mkoa wa Mbeya Ndugu Leonard Bashosho na Ndugu Monica Bashoho, karibuni sana wale wa kutoka Mbeya. (*Makofi*)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanawake 50 ambao ni wajasirimali na wanafunzi 20 toka Shule ya Msingi ya Upendo *Friends* ya Jijini Arusha. *Upendo*

Friends karibuni sana kutoka Arusha. Mmependeza kweli kweli Upendo. Karibuni sana, kweli mnatoka Arusha ninyi. (*Makofii*)

Ndugu Godfrey Gunda na Ndugu Clemencia Gunda karibuni sana pia popote pale mlipo. (*Makofii*)

Matangazo mengine ni pamoja na tangazo kwa ajili ya ibada la Mheshimiwa Anna Lupembe, anawaomba wote Wabunge na watumishi kuhudhuria katika eneo la *basement* leo siku ya Jumanne tarehe 18 ambapo kutakuwa na ibada saa 7.00 mchana na kama mnavyoona kwaya zimekuja ziko na nguvu kubwa. Ni vizuri kufika pale kuona umahiri wao. (*Makofii*)

Katibu wa Bunge anawatangazia wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane hapa mara tu tutakapoahirisha shughuli za Bunge saa saba. Kamati ya Uongozi muhimu sana tukutane saa saba kamili mchana. Kama Mwenyekiti hayupo, mkamu tafadhali ufile. Saa saba tukimaliza tu hapa. La Kamati ya Uongozi nimeshawaeleza.

Waheshimiwa Wabunge, niwasemee kidogo tu *TWPG* kuhusu yale mambo ya choo bora kwa kila jimbo na mchango wake. Nawaomba sana muwe na subira katika jambo hili, si jepesi kihivyo, nimeona watu wanapiga piga maneno mengi, linahitaji busara kubwa namna ya kuliendea na likipelekwa tu hovsky hovyo litatuletea matatizo makubwa.

Kwa hiyo, ningeomba badala ya kuwa mnarusha maneno na nini kuwa na subira kidogo, hakuna nia mbaya katika jambo hili, linahitaji tafakuri ya ndani kidogo namna ya kuliendeza. Kuna sababu nydingi ambazo zingine siwezi kuzielezea hapa, njia mojawapo ambayo inapendekezwa na watu wengi ni kwamba zile fedha zipitishiwe kwenye akaunti za Wabunge, lakini nina hakika baadhi ya Wabunge zikiingizwa hizo hela zitakatwa kwenye madeni, benki watachukua hazitafika hata huko shulenii. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tukianza mjadala huo hapa yaani hatutaumaliza, yaani hilo nina uhakika. Mkitaka semeni,

tutawaambia tutumbukize lakini matokeo yake itakuwa *disaster*. Mimi ndiyo natunza ma-file najua kuna watu ukitumbukiza shida. Kwa hiyo lazima kuwa na umakini kwa hiyo tuwe na uvumilivu kidogo. Hakuna anayefanya makusudi katika jambo hilo hata kidogo. Natafuta njia mbalimbali ambazo zitakuwa ni bora zaidi kuona namna gani ya kutekeleza jambo hili. Sio rahisi, inatakiwa kukaa na kufikiri vizuri. (*Makofi*)

Kama ambavyo tumekuwa tukisema kwamba vijana wetu wa *Taifa Stars* tayari wapo kule Cairo, Misri kwa ajili ya AFCON na tulikwishesha hapa kwamba Wabunge ambao wangependa kwenda wajiandikishe na kutakuwa na uchangiaji. Kwa hiyo awamu ya kwanza tutakuwa na Wabunge kama 48 hivi ambao watakwenda, ni idadi nzuri na kubwa. Tumejitahidi sana kuititia ofisi yangu kujaribu kupunguza machungu ya uchangiaji kiasi ambacho kwa kweli *trip* hii imekuwa ni *very fair*. Kwa mtu ambaye hukujandikisha kwa kweli ni wewe mwenyewe tu hukutaka. Lakini tumejitahidi sana, yale machungu hayatakuwa makubwa kiasi hicho, tume *converse* vya kutosha na kwa hiyo watasafiri vizuri, tutahakikisha wanapata hoteli *five star* wakiwa kule na kutakuwa na awamu mbili, awamu ya kwanza na ya pili na tumeshafunga dirisha jamani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wewe ukishajitahidi wamemalizika ndiyo hao na wale wa *trip* ya kwanza safari hii nitalongoza mimi mwenyewe nitakayeondoka usiku wa leo kuelekea huko, tutawapelekea salamu zenu Waheshimiwa na tutawapa moyo sana vijana, tunajua mechili zile ni ngumu, lakini ni hamasa kubwa kwa Watanzania kuona kwamba timu yetu baada ya miaka yote karibu 40 inafikia kiwango kile cha kuweza kucheza michezo ile. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tumeona Bunge tuchukue jukumu kwakweli la kuongoza hamasa na kuhakikisha kwamba vijana wanapocheza wanajua viongozi wao pia wamesafiri umbali wote huu kwenda kule na hatutarajji kushindwa, kwa kweli. Tunachoomba kwenu ni kuendelea kuiombea timu yetu na tumehakikisha kwamba Pierre tunaenda naye. Kwa hiyo,

tunaenda naye Pierre, ili kuhakikisha *Taifa Stars* inakuwa juu.
(*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, kama kuna chochote katika wale wanaokwenda *AFCON*, tunaweza kuwasiliana mchana baada ya matangazo kama kuna chochote, lakini kila kitu kiko, kila jambo liko vizuri, kila kitu kiko sawasawa. Ubalozi wetu wako vizuri, tutapokelewa, tutafika hoteli, tutapelekwa uwanjani, tutarudishwa kutoka uwanjani, tutapata *tour* kwenda kwenye *pyramids*, kwenye *museums*, tutakwenda *Suez Canal*/kufanya *boat* crues kwenye *Suez Canal*. Kwa kweli ni *trip* ambayo Waheshimiwa ambaye hakutaka kwenda, basi, bahati mbaya lakini ni *opportunity* chache, watakaporudi watakwambieni. (*Kicheko*)

Mwisho kabisa kwenye meza yangu hapa ni kuhusu uchangiaji wa bajeti, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mimi ningekuombeni Waheshimiwa, kila mmoja wetu apate nafasi ya kuichangia bajeti. Kila mmoja wetu, kadri inavyowezekana, jipange vizuri, pitia yale ma-*books*, ndiyo maana tupo hapa, sisi ni wawakilishi wa wananchi. Unapokuwa mwakilishi wa wenzako, halafu mambo mazito yanawekwa mbele yako, halafu unanyamaza, sijui kama unawatendea haki wale ambao umewawakilisha na moja ya mambo muhimu ni Bajeti ya Taifa, bajeti ya Serikali. Maana haya ni mapato na matumizi kwa mwaka mzima unaokuja, sasa je wananchi wako wanasema nini kuhusu jambo hili. Jimbo lako, wewe mwenyewe kama Mbunge unashauri nini, Serikali ielekee wapi, ifanye nini. (*Makofi*)

Baada ya hotuba nzuri sana ya Waziri wa Fedha, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge, usinyamaze, pata nafasi, tuleteeni majina kuititia *Chief Whips* wenu, kila mmoja apate na tumetenga siku za kutosha kabisa, kila mtu ambaye atajiandikisha kwa maana ya kuzungumza humu tutampa nafasi. Kwa hiyo, tujitahidi natoa wito kwenu Waheshimiwa Wabunge tutumie fursa hii vizuri, tuchangie kwa uzuri tu kwa maana ya kushauri na Waziri wa Fedha, Naibu wake na timu nzima inayohusiana na masuala yetu ya mipango, uchumi, fedha, iko hapa Dodoma wakati wote huu kwa ajili ya

kuchukuamawazo ya Wabunge ambayo ndiyo mawazo ya wananchi wa Tanzania.

Basi naomba sasa tuendelee, unapopata dakika zako kama kawaida, ukienda moja kwa moja inakuwa nzuri zaidi ili uweze kuokoa muda zaidi. Kwa orodha niliyonayo hapa leo, atatuanzishia Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Saddiq Murad atafuatia.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mapendekazo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii kuchangia hotuba ya bajeti kwa mwaka 2019/2020. Mimi napenda kuanza kwa kusema kwamba duniani kote maendeleo ya nchi hayategemei kodi peke yake na ninalisema hili kwa sababu wimbo humu ndani sasa hivi imekuwa ni kodi, kodi, kodi, taratibu za kikodi, sasa leo mimi nitazungumza zaidi kwenye kushauri. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, kodi ni moja ya kitu ambacho kinasaidia maendeleo, lakini kodi asilimia kubwa ya nchi nyingi inatumie kwenye kulipa mishahara na *recurrent budget* kwa maana hizi *OCs*, matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, dunia ya sasa kama unataka kuendelea, kuna njia kubwa mbili tu za kufanya; jambo la kwanza ni *Foreign Direct Investment* na jambo la pili ni *Private Public Partnerships*. Hayo ndiyo mambo makubwa ambayo yanaweza kukutoa kwenye kasi ile ambayo dunia inaitaka ya sasa.

Mheshimiwa Spika, leo tumepitia hotuba ya Wizara ya Fedha na kwenye hotuba ya Wizara ya Fedha na baadhi

ya hotuba zilizotangulia, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imemeanisha baadhi ya miradi ambayo bado haitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, wameelezea Mradi wa *LNG* wakati wa Nishati na Madini kwamba uko kwenye *negotiation*, wameelezea mradi, kwa mfano mradi ambao mwingine umekufa wa Bandari ya Bagamoyo, kuna Mradi wa Liganga na Mchuchuma, kuna Mradi wa *SGR* na kuna Mradi wa *Stiegler's Gorge*. Miradi hii ingetumia mfumo wa *FDI* na *PPP*, hebu fikiri leo uchumi wa Tanzania, tumekuwa katika *level gani*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *LNG* dola bilioni 30, unazungumzia triliuni 70 za kitanzania; Bandari ya Bagamoyo, endapo tungeingia mkataba vizuri kabisa, dola bilioni 10, sawasawa na triliuni 24, Liganga na Mchuchuma - dola bilioni tatu, sawa na triliuni saba, *SGR* triliuni 17 yaani ukimaliza *phase nzima* na *Stiegler's Gorge* triliuni sita. Yaani unazungumzia uchumi ungeongezeka kwa wakati mmoja kwa triliuni 124. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo pato letu la Taifa ni triliuni 125, fikiria hizi fedha zingeingia ndani ya uchumi wetu, triliuni 124 kwa wakati mmoja, nakuhakikisha leo Serikali ya awamu ya tano ingekuwa *ime-double GDP* ya Taifa letu, lakini tatizo liko wapi, watakwambia mikataba mibovu na *weakness* ambayo tumekuwa tukiifanya kila siku kwenye miradi mikubwa kama hii, yaani wewe ukigundua kifungu kibovu na mkataba wote huutaki, wakati utaratibu wa dunia nzima, kama kuna mahali pana shida, unakwenda una *renegotiate*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa hebu angalia *trickle down effect* kwenye masuala kama haya, leo ajira zingeingia bwerere kila mahali, kwa sababu kila mtu angepata ajira kwenye maeneo hayo kwa mfumo huo kwa hizo fedha ambazo karibu triliuni 124 zingeingia ndani. Viwanda vingekuwepo vingi nautolea mfano, Bandari ya Bagamoyo peke yake, ilikuwa tu siyo bandari, *the whole project* ilikuwa na viwanda zaidi ya 1,000 pale. Sasa haya yote yanegkuwa yanafanyika kwa wakati mmoja, leo maendeleo yote yanegbadilika. Sasa sisi tunatumia fedha za ndani na wakati

mwingine tunakopa kwenye mabenki ya kibiashara ku-*finance* miradi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na mfano mzuri, *SGR* tunakopa kwenye mkopo wa kibiashara, *Stiegler's* vilevile, tunakopa vilevile humo ndani, tutaanza kulipa kabla hii miradi haij-mature!

Mheshimiwa Spika, na ninayasema haya kwa sababu moja tu, *SGR* awamu ya kwanza, Dar es Salaam - Morogoro, mpaka sasa umetekelezeka kwa asilimia 48. Bado hatujafika Morogoro, 48% tutakuja kumaliza mwaka gani na tunakwenda kwenye uchaguzi mwakani. Morogoro - Makutupora mpaka sasa umetekelezeka kwa asilimia saba tu, bado asilimia 93! Kwa mwendo huu Rais Magufuli anaweza kuondoka madarakani miradi hii haijakamilikka bado. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, *Stiegler's Gorge* mpaka sasa hivi mradi ni kwamba upo tu kwenye *ma-study*, wametoa bilioni 700, haujaanza ku-mature na tunahitaji umeme ambao ile reli itakapokamiliika inatakiwa ianze kutumia ule umeme. Sasa haya yote ni kwamba tunakwenda lakini tunakwenda *in a slow, very slow* yaani mwendo wa konokono. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni vizuri na Mheshimiwa Rais, nakwambia anataka kusikia maneno kama haya, hataki kusikia vitu vingine. Sasa kinachotokea ni nini, Bunge tunashauri, lakini haya mambo hayamfikii!

Mheshimiwa Spika, na mimi kuna kitu kilinishangaza sana, siku ile Mheshimiwa Rais wakati anazungumza na wafanyabiashara, nikawa najiuliza swalii, hivi yale yaliyozungumzwa na wafanyabaishara, humu ndani Bungeni hatujawahi kuyasema? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na kama humu ndani hatujawahi kusema, basi sisi wote hatustahili kuwa Wabunge. Kama hatujawahi kuyasema maana yake hatustahili kuwa

Wabunge na kama tumeyasema, hayafiki, tafsri yake ni kwamba kuna watu ni washauri wabovu kabisa wa Mheshimiwa Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na hii ninaisema kwa sababu moja, mwaka 2006 nikiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale Rais Thabo Mbeki wakati ule alikuja pale, akafanya mdahalo Nkrumah, sasa pale Nkrumah alituambia hivi, kazi ya Urais inaweza kuwa ngumu kama una washauri wabovu na inaweza kuwa rahisi kama una washauri wazuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na ukisikia huko mtaani, unamsikia Rais Magufuli analalamika, Urais mgumu, Urais mgumu! Kumbe jibu ambalo Mbeki alituambia pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2006 ndiyo leo naliona kwamba amezungukwa na washauri wabovu, ndiyo maana anaona kazi ngumu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo Rais anakutana na wafugaji, Rais anakutana na wafanyabiashara, Rais anakutana na wachimba madini wadogo, Rais ata..., yaani Rais anafanya kila kitu mwenyewe! Bunge tunafanya kazi gani? Hasa hayo ndiyo maswali ambayo yanamnyima... (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimelisema hili kwa sababu mwaka jana kwa mfano Kamati ya Bajeti tulikuja hapa na mapendekezo 11, Serikali ilikataa mapendekezo yote ndani ya Bunge hili! Baada ya miezi mitatu mambo hayajaenda vizuri, mchuzi wa zabibu, katikati ya mwaka wa fedha tukaletewa sheria ya mabadiliko hapa, Rais kule alishapigwa *fix*, katikati ya mwaka wa fedha tumekuja kubadilisha mapendekezo, mwaka huu wameleta mengine kama matatu, bado kama manne hivi. Sasa haya yote, ndiyo matokeo ya watu kumshauri vibaya Mheshimiwa Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na Rais anapaswa kushauriwa kwamba unajua na Mheshimiwa Mpango hili unajua, haya mambo ndiyo Rais anakiwa aelimishwe *beyond reasonable doubt!* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia, mimi kila siku, siku moja nilizungumzia Rwanda, nimesoma mfumo wa Rwanda. Rwanda Rais Kagame, kabla hajafanya jambo, anaruhusu watu wafanye *study analysis*, wanakwenda zaidi ya mara tatu, yaani watu wanasoma mfumo sawasawa. Sasa *study* ya kwanza, *study* ya pili, *study* ya tatu, wanajiondoa na wasiwasi wa kutekeleza mambo, baada ya hapo, wanakwenda kutekeleza wakishakuwa wameondoa *doubts* zote katika ule mkataba. Sasa leo Tanzania, nikawa najiuliza hii mikataba tunayoikimbia, ina maana sisi hatuna hata wasomi/wanasheria wanaoweza kuandika mikataba vizuri! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ee, tunakaa na watu ambao wanafikiri tu kodi ndiyo inaweza kuleta maendeleo nchi hii, fedha za ndani ndiyo zinaweza kuleta maendeleo nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, yaani, *with this*, namna, hata ukiwapa miaka 100 hakuna chochote watakachokifanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa *we have to think in a different way* na haya mamabo mmpelekeeni Mheshimiwa Rais aweze kuyafanya kazi, kinyume na hapa, tutakwenda tu, tutabidi tu kwamba Bunge basi limalize kazi yake, awe anafanya mwenyewe pale lkulu awe anaita sijui viongozi wa dini, asikilize maoni yao, na haya mengi tunayoyasema hapa!

Mheshimiwa Spika, waambie watu wako waache kuchujachuja sana haya mambo, yaani wanayakata sana, watu wanataka kusikia huko, taarifa haziji kama zilivyo, kwa hiyo, matokeo yake ni nini, lazima watu muwe na uwezo wa kusikiliza *both sides*, mambo mazuri na mambo mabaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili niliamua niliseme kwa sababu ndiyo namna pekee ambayo tunaweza tukatoka hapa tulipo, tukaenda mbele zaidi, lakini kitu kingine tulizungumzia kuhusu kilimo. Mimi nimejaribu kusoma, Tanzania

sasa hivi tunataka uchumi wa viwanda, lakini hatuwekezi kwenye kilimo! Jana mimi nimejaribu kupitia kwenye mitandao, kwenye kusoma *journals*nyingi, nchi zote zilizokuwa kiviwanda, kwenye *first generation* ya *agriculture revolution*, *second generation* ya *agriculture revolution* na *third generation* ambayo ilikuwa ni ya China, wote kabla ya kwenda kwenye viwanda, waliwekeza kwenye kilimo. Kilimo kilipozidi, ndipo wakaenda kwenye viwanda. Sisi tumekwenda kwenye sera ya viwanda wakati hatuna malighafi na ndiyo maana mnaona, sera ya viwanda haitekelezeki! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wewe mwenyewe unajiliza, leo, hivi unaenda kuanzisha kiwanda, wakati huna pamba ya kutosha, unakwenda kuanzisha kiwanda wakati tumbaku yenye imeshuka kutoka uzalishaji wa tani milioni 150 mpaka tani 350,000. Pamba yenye imeshuka, korosho imeshuka, tunaanzisha kiwanda kwa malighafi ipi? Za kuagiza kutoka nje ya nje ya nchi! Kasome *First Agriculture Revolution*, kasome *Agrarian Economy*, kasome *The Green Economy* ya China, wote watakwambia *causative* ya viwanda, *causative* ya mabadiliko ya viwanda ilitokana na kilimo kikubwa na cha kisasa, ndiyo wakaenda katika uchumi wa viwanda. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Murad atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi. Mheshimiwa Saddiq!

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi asubuhi ya leo, naomba nianze na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu yao yote kwa kutuletea bajeti nzuri sana, sana, sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais amethubutu, leo tunazungumzia Tanzania ya viwanda kwa vitendo na mimi ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, nasema sera inatekelezeka! Wanaosema sera haitekelezeki, waje

kwenye kamati yangu. Twende Kibaha tukaangalie viwanda vipyta vilivyojengwa, twende maeneo yote tukaangalie viwanda vilivyoshamili, njooni tuangalie wawekezaji wanavoinga Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sera ya viwanda inatekelezeka kwa vitendo na Mheshimiwa Rais tumemshauri kama Kamati, akae na wadau azungumze nao, amekuwa msikivu, amekaa na wafanyabiashara, amekaa na wadau na amewasikiliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, ni Rais wa mfano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanaozungumza maneno ya pemberi wameishiwa hoja, Mwenyekiti wa kamati ndiyo mimi. Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda ndiyo mimi, ukweli naujua mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amefanya mambo ambayo tumemshauri sisi, zile tozo zote zilitakuwa ni kero, leo tozo 54 zimeondoka, siyo jambo dogo. Hilo ni jambo kubwa na la mfano na la kuigwa na la kupongezwa na ametekeleza llani ya chama chake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika hili tunakupongezza, tuko na wewe, kanyaga twende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Bashungwa, nimpongeze Ndugu Mhede, karibuni katika mchakato huu tusaidiane tufanye kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kidogo muda unakwenda, nizungumzie suala la *TRA*. *TRA* kuna utaratibu ambao unasababisha wafanyabiashara na Watanzania wapate shida. Shida namba moja ni zile fomu za *TIN*, fomu zile zinaandikwa kwa kiingereza, wale wafanyabaishara wanapata shida kuzijaza, fomu zile zina urasimu, matokeo yake kuna vishoka wamekaa nje kwenye Ofisi za *TRA*, wanachukua zile fomu wanawajazia watu na vishoka wale

wanawa-charge Watanzania shilingi 10,000 hadi shilingi 20,000; *TRA* tubadilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, fomu zile zimepitwa na wakati, wakati fomu zile zinaandaliwa nchi ilikuwa haina Vitambulisho vya Taifa, sasa hivi tuna vitambulisho vya Taifa vina kila kitu ndani, anuani zote zimo ndani, kile kitambulisho kinatosha kabisa kutengeneza fomu ambayo ni *very simple* na fomu hizohizo zina matatizo upande wa *BRELA*, nawaomba *TRA* waliangalie hili, fomu zilizopo zinaleta urasimu na vishoka tunawapa muda wa kutafuta fedha nje ya utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze kwa upande wa *TRA* ni suala la kodi. Tumezunguza hizi kodi nyingi sana, sasa tunaomba wakasimamie ukadiriaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lipo kwenye *assessment*, pale kwenye *assessment* ndiyo kuna matatizo, *DG* mpya tuna matumaini na wewe, ulikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda nakufahamu uwezo wako. Nenda kaibadilishe *TRA*. *TRA* ikibadilika uchumi wa nchi utakua, *TRA* ikiwa rafiki wa wafanyabishara, tutasonga mbele kwa kasi kubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kidogo suala la fedha za kigeni, niongee na Gavana kama yupo. Hatua zinazochukuliwa na Serikali tunaziunga mkono, lakini naomba ifahamike, biashara za Dubai, China na nchi nyingine duniani, biashara kubwa hizi zimetawaliwa na suala la kulipa fedha taslimu. Unapokwenda Dubai kununua mzigo, ukinunua mzigo wa dola laki moja, wale wafanyabiashara wanataka *cash* dola laki moja. Sasa je, utaratibu wa kupeleka *cash* dola laki moja ukoje? *BOT* watusaidie namna bora ya kuhakikisha biashara zinarudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kariakoo imepotea katika ramani ya biashara. Tulikuwa tuna Kariakoo ya Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda na Congo, leo Kariakoo ile imepotea

kwenye mtandao haipo na sababu ya kupotea ile Kariakoo zipo nyingi ikiwemo suala la namna ya kupeleka fedha za kigeni Dubai, China na nchi nyingine, lakini leo kwa ruhusa yako Kamati ya Bajeti tulikwenda Uganda na mimi nilikwenda. Unafika Uganda unawauliza wafanyabiashara wa Uganda mbona siku hizi hamji Dar es Salaam kuchukua mzigo wanakwambia sasa hivi wa Dar es Salaam wanakuja kwetu, wa Malawi wanakuja kwetu, wa Rwanda wanakuja kwetu. Hayo ndiyo majibu tuliyopewa Uganda na wale bahari hawana, Bandari hawana. *BOT* tujulize kuna nini hapo, *TRA* tujulize kuna nini. Kwa nini tumelipoteza soko ambalo lilikuwepo Dar es Salaam, soko la Kariakoo. Bidhaa zile zilikuwa zinapatikana pale zina *grade* zake. Ukinunua mzigo kule Dubai, China kuna *light weight*, kuna *heavy weight* sasa zile biashara zilizokuwa zinafanyika *TRA* wao hawajui *light*, hawajui *heavy*, hawajui nini, wao ni kodi, kodi, kodi matokeo yake tumeua mtandao wa biashara, tumewakatisha tamaa wafanya biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, leo tunatakiwa tufungue milango ya Kariakoo, leo tunatakiwa tujulize tumekosea wapi, tumekwama wapi. Mheshimiwa Dkt. Mpango tukae tusaidiane tufanye mawazo ya pamoja, tuzungumze hili tuna ushahidi, tuna nia ya kusaidia eneo hili lirudi katika mtandao wa biashara katika nchi zote za maziwa ambayo yametuzunguka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie Mfuko wa Mazingira; Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kulikuwa na Mfuko wa Mazingira ulikuwa una kazi nzuri ya kufanyakazi ya mazingira kwenye Nchi yetu. Mfuko huu mwaka jana 2018/2019 ultengewa bajeti ya shilingi milioni 500 fedha zile hazikutoka. Dkt. Mpango alivyokuja kwenye Kamati ya Uongozi na Bajeti akaahidi 2019/2020 zile milioni 500 zitawekwa. Nashangaa, naona zile milioni 500 hazipo na ule mfuko hauna hata senti moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni mwanamazingira, Mfuko wa Mazingira hauna senti hata moja maana yake una zero na mfuko haupo. Nimuombe Dkt. Mpango rudisha kauli yako,

zile milioni 500 ni ndogo mno tuanze na hizo. Tukipata shilingi milioni 500 tunaanza hapo. Hilo ni la Mfuko wa Mazingira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende Mvomero; Mvomero tuna barabara ya lami inayoanzia Magole-Turiani-Mziha-Handeni-Korogwe. Barabara ile iliwekwa na Serikali makusudi ni barabara mbadala kwa ajili ya barabara ya Chalinze-Segera. Kilometra 48 zimeshaweka lami Turiani-Magole bado Turiani-Mziha-Handeni. Mwaka huu niipongeze Serikali wameweka bilioni moja katika barabara hiyo, naomba sasa barabara hiyo itangazwe, mradi ule uanze ili barabara ile ifunguke. Wenzetu wa Handeni-Korogwe waliashaweka lami kwenye barabara yao.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la mazao ya biashara; kule kwangu wanalima miwa, Kagera kule wanalima kahawa, Mwanza wanalima pamba, eneo hili tuna shida. Eneo hili tuna shida, nimpongeze Waziri amezungumzia kahawa na wanasema katika hotuba yake kwamba watalinda kahawa lakini mimi napata shida kidogo; hotuba ya kiingereza ya Waziri inazungumzia *roasted coffee*. Wale watu wa Kagera wanataka *instant coffee* inayokuja kutoka nchi za nje ndiyo ushuru wake upandishwe kwa sababu viwanda vilivyopo Tanzania vya *instant coffee* endiyo vinapata ushindani mkubwa. Sasa kwenye hotuba yake amezungumzia kahawa, hotuba ya kiswahili amezungumzia kahawa, lakini kwenye hotuba ya kiingereza amezungumzia *roasted coffee*.

SPIKA: Ahsante Mwenyekiti.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwiliima na Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti iliyosomwa na Waziri Dkt. Mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii kwa kutuletea hotuba nzuri inayoonesha muelekeo mzuri wa nchi yetu kiuchumi na kazi kubwa inayofanywa na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hotuba hii imezingatia mambo mengi ambayo tumekuwa tunashauri, mambo mengi ambayo yamekuwa yanaleta kero kwenye jamii hotuba hii imezingatia kwa hiyo kwa moyo wa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi kubwa sana ya kuandaa hotuba hili nzuri. Jukumu letu sasa nikushauri maeneo machache ambayo tunafikiri yanatakiwa yafanyiwe marekebisho au yaongezwe kwa ajili ya kuboresha kile kilichowasilishwa kwetu. Kwangu mimi nitajikita kwenye maeneo makuu mawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, uchumi wetu unaonesha kupanda na kwa mujibu wa takwimu hizi, uchumi wetu sasa umekuwa kwa asilimia saba na asilimia saba hizi zimetokana na sekta mbalimbali za kiuchumi ambazo zimekuwa zinafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika sekta zilizofanya vizuri ni sekta ya kilimo ambayo kwa ukuaji wake ni sekta ya nne kwa kukua, lakini kwenye eneo hili, sekta hii ya kilimo kama inavyoonekana imekua kwa asilimia 5.3 na tunatambua sekta ya kilimo ni sekta inayojumuisha watu wengi, inaajiri watu wengi na kama tutaiwekea mkazo inaweza kuongeza kwa kiwango kikubwa sana ukuaji wa uchumi wetu kama Taifa na kwenye eneo hili la kilimo likijumuisha uvuvi, mifugo na kilimo chenyewe bado hatujawekeza sana kwenye sekta hii ya kilimo. Kwa mfano, tukiangalia kwenye sekta hi, tukijumuisha uvuvi, mifugo na kilimo chenyewe kwa ujumla wake aukiangalia sehemu ya uvuvi ndiyo imechangia

sehemu kubwa sana karibu asilimia tisa, lakini eneo hili la uvuvi ambalo linaajiri watu wengi sana bado kuna vikwazo vingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tumeona kwa mujibu wa hotuba kuna maeneo mengi hasa kwenye eneo la uvuvi ambako tozo nyingi zimeondolewa, lakini bado kwenye sekta ya uvuvi yenye we bado kuna tozo nyingi sana ambazo zinawafanya wanaoshiriki kwenye shughuli za uvuvi wasiweze kufanya vizuri sana na kuchangia pato la Taifa. Kwa hiyo, bado ni muhimu sana Serikali iliangularie hili. Niombe Mheshimiwa Mpango uangarie namna gani tunaweza tukaifanya sekta ya uvuvi ikachangia sehemu kubwa sana ya pato letu na tukiangularia kwa mfano kwenye mazao ya kilimo, kwenye bidhaa tulizouza nje kutoka bilioni 790 mwaka huu tumeuza zaidi ya trillioni moja ya mazao, lakini tunaweza tukafanya vizuri zaidi kama tutaboresha sekta ya uvuvi na wakafanya kazi vizuri, bila vikwazo vingi na tukaweza kuuza mazao mengi nje.

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri niombe sekta ya uvuvi vilevile iangaliwe, tozo wanazokutana nazo wavuvi ni nyingi sana ziweze kuangaliwa kama zilivyopunguzwa kwenye eneo la mifugo, sekta ya uvuvi vilevile zipunguzwe kwa sababu kama tunavyo jua vijana wengi wanaajiriwa kupitia sekta hii ya uvuvi kwahiyio kakam tozo hizi zitapungua wataweza kujiajiri, watafanya shughuli zao lakini uzalishaji utakuwa mkubwa zaidi na kuwezesha Taifa letu kuweza kuuza kwa ukubwa snaa mazoa ya uvuvi nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini niongelee eneo la kilimo; kwa mujibu wa tafiti mbalimbali, kilimo kinaajiri zaidi ya nusu ya wananchi wa Tanzania na sehemu kubwa tunayouza nje yanatokana na kilimo. Tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda, bila kuboresha eneo la kilimo hatutaweza kufikia kwa ufanisi kwenye uchumi wa viwanda, kwa hiyo, ni lazima tuwekeze wka kiwango kikubwa sana na kwa dhati kwenye kilimo hasa kilimo cha kisasa, kilimo cha umwagiliaji. Bahati mbaya sana tuna eneo zuri sana, eneo kubwa tukilinganisha na mataifa mengine yanayotuzunguka. Juzi tumemuona Mheshimiwa Rais amefanya ziara nje, watu wengi sana

wanaotuzunguka wanahitaji chakula kutoka nchini kwetu. Sawa, tunaweza tukawapelekea chakula, lakini tuna uwezo wa kuzalisha zaidi na zaidi tukaweza kuza chakula kingi sana na tukaipatia nchi yetu pesa za kutosha sana za kigeni, lakini kilimo tunachokifanya bado ni kilimo cha kawaida sana cha mazoea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachowea kushauri ni muhimu tuangalie, tuangalie *comparatively* maeneo tuliyonayo. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa inalimwa pamba, Nyanda za Juu Kusini wanalima mahindi, kuna eneo wanalima mpunga, tunaweza tukatenga kwa mfano, eneo la Kilombero ihawa *hub* ya kuzalisha mazao kwa mfano ya mpunga, eneo la Nyanda za Juu Kusini ikawa eneo maalum kwa ajili ya kuzalisha mahindi, eneo la Kanda ya Ziwa ikawa eneo maalum kwa ajili ya kuzalisha pamba, Serikali ikaangalia ni watu gani ambao wanaweza wakatusaidia kuzalisha mazao haya, tukawekeza kwenye maeneo haya tukiamini kwamba namba kadhaa ya watu Serikali ichukue jukumu la kuwawezesha kimkakati na kuweka malengo kwamba watu hawa Serikali inawawezesha wazalishe kiasi fulani cha mazao ili sasa mazao haya na wati huo Serikali ikiwaandalia masoko waweze kuzalisha mazao haya na vilevile wakiwa na uhakika wa masoko yao. Tukifanya hivyo kwa miaka miwili, mwaka mmoja, miaka mitatu tunaweza tukawa na uzalishaji mkubwa sana wa mazao mbalimbali ya kimkakati na Taifa letu likaweza kuuza mazao mengi nje na kuweza kuisaidia Nchi yetu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tuynatambua kwamba kupanda kwa uchumi wetu kumechangiwa ana *stabilization* ya bei ya mazao ya chakula lakini vilevile *inflation rate* kuwa *stable*, lakini yote haya yanawezekana tu kama tunaweza kuwa na chakula cha kujitoseheleza ndiyo tunaweza tukafikia hapa.

Kwa hiyo ningeomba sana Serikali iangalie na hasa Mheshimiwa Waziri tuone namna gani tunaweza tukafanya kilimo cha kimkakati badala ya kulima kilimo cha kawaida tu kila mmoja analima jinsi anavyojisikia hatutaweza kufikia malengo yale tunayoyataraja.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo lingine ambalo nilitaka nichangie...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Joseph bahati mbaya ni kengele ya pili.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mbunge wa Ukerewe. Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel. Mheshimiwa Hasna! Hayupo? Mheshimiwa Ruth Mollel utafuatiwa na Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ili yoko mezani hapo. Naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani moja kwa moja, *100 percent.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mtaalam wa rasilimali watu na kwa vile ni mtaalam wa rasilimali watu, *interest* yangu kubwa san imekua kwenye upande wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza mara ya mwisho kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu watumishi, ninaendelea kusisitiza kwamba katika awamu hii watumishi wamesahuliwa kabisa. Wamesahauliwa kwa sabbau katika maslahi yao, *increment* zao za mwaka hawapewi, vilevile hata ile nyongeza ya Mei mwaka juzi imepita, mwaka jana imepita na mwaka huu imepitira bila nyongeza yoyote ya mshahara wakati tunajua kwamba hali ya uchumi imekuwa ni ngumu, vitu vimepanda bei, kama nilivyo sema na sasa nasema kwa mfano, kibaba cha unga cha kilo tano ulikuwa unanunua kwa shilingi 2,000 sasa unaunua kwa shilingi 6,000 na mshahara wa mtumishi umebakie pale pale.

Kwa hiyo, ninazidi kusisitiza kwamba watumishi wa umma kwanza ndiyo walipa kodi wazuri, kwa sababu wao wanalipa *pay as you earn*, wanapopokea mshahara wanalipa kodi ambayo hawawezi hata waka-forge, kwa hiyo, wanailipa kodi stahiki. Kwa mfano, mwaka huu tunategemea *pay as you earn* itakuwa *1.0 trillion* tofauti na mwaka jana ambayo ilikuwa bilioni 998; kwa hiyo, tunaona jinsi ambavyo watumishi wa umma wanachangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya nchi yetu, lakini hatuoni ni kwa jinsi gani na wenyewe sasa wanasaidiwa kufanya maisha yao yawe rahisi kwa sababu wanachangia *67 percent* ya kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeangalia bajeti Mheshimiwa Waziri ametenga kama shilingi triliuni saba kwa ajili ya mishahara, kwa hiyo hii itakuwa ni mishahara hakuna hata nyongeza ya mishahara kwa ajili ya watumishi. Sasa mimi ninasikitika sana kwasababu watumishi ndiyo *engine* ya Serikali, leo watumishi wakiweka mgomo hapatatosha hapa, hakuna kitu kitaendelea, nchi yote itazizima, itasimama. Ni kwa nini Serikali ya Awamu ya Tano haioni umuhimu wa watumishi na kufanya maisha yao yawe rahisi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini sasa kwenye hii *pay as you earn* Serikali ya awamu ya Tano ionictheshe huruma, ionictheshe interest ya watumishi kwa kuwapunguzia kodi ya *pay as you earn?* Naomba Mheshimiwa Mpango atakapokuja atuambie ni jinsi gani sasa waonyeshe *good will* kwa ajili ya watumishi ambao wanaitumikia nchi hii na kuindhesa Serikali yenye kwa kuwapunguzia kodi ya *pay as you earn.*

Mheshimiwa Spika, nakuja tena kwenye suala la watumishi; watumishi wanaidai Serikali karibu shilingi bilioni 61 hii ni walimu pamoja na watumishi wengine. Wanadai nyongeza za mshahara, wanadai pesa za likizo, wengine *per diem*, Serikali ikikudai itakukata mshahara, ukichelewa kulipa kodi ya ardhi utalipa *interest*, lakini inakuaje Serikali watumishi wanawadai pesa zote hizo watawapa *interest* kiasi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni jambo la kusikitisha na mimi ninayo mapendekezo ambayo naishauri Serikali ili kuepuka hii adha ya malimbikizo kila siku ya madai ya watumishi miaka nenda miaka rudi, ni muhimu sasa katika pesa zile ambazo ni shilingi bilioni 666 ambazo zimetengwa kwaajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa basi Serikali ihakikishe hayo madeni yanalipwa, hilo moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili; Serikali ifanye kazi ya ziada kuangalia ni mifumo ipi na taratibu zipi zinazofanya malimbikizo ya madeni na kuna namna ya kufanya. Namma ni kuangalia mfumo wenyewe unavyokwenda. Tunao wataalam wa kuchambua *systems*, tunaita *process analysis*. Tutafute watu wa *process analysis* watufanyie waone ni kitu gani kinachofanya haya madeni kila siku yanalimbikizwa katika Serikali na kufanya ulipaji unakuwa mgumu. Inakuwa ni rahisi kama nyongeza ya mshahara inachukua *process* mara moja unalipa pesa kidogo kuliko kuwa na malimbikizo kila mwaka inakuwa ni vigumu sana kulipa.

Kwa hiyo, nashauri watafutwe wataalam kama hatunao pale utumishi kwenye Ofisi ya *Management Services* tulete watu kutoka nje watusaidie kufanya uchambuzi wa huu mfumo ambao unaleta malimbikizo ya madeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja pia kubwa ambalo mimi naliona; tatizo kubwa ambalo Serikali inatakiwa kulifanyia kazi ni mfumo wa usimamizi na ukaguzi. Kila mara tunakuwa kama tunastushwa ni kwa sababu hatuna mfumo wa usimamizi na ukaguzi endelevu ambao utaweza kugundua matatizo haraka na kuyashughulikia haraka.

Mheshimiwa Spika, mimi pia napendekeza kwamba uwepo mfumo wa uwajibikaji, kwa watendaji, watendaji wanaohamisha watumishi wakijua hawana bajeti ya kuwalipa wawajibishwe, watumishi wanaoweka taarifa *fake* kwenye mtandao wawajibishwe na tutakapokuwa na huo mfumo wa kuwajibisha basi tutajenga mfumo ambao ni mwenye *integrity*, ambao unaweza kufanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia ninakwenda kwenye suala la Ubalozi, Balozi zetu hali ya Balozi zetu ni mbaya sana nikiangalia Balozi ya Brussels ambayo jengo sasa karibu litakuwa *condemned* na inahitajika *Euro 300,000* kuweza kulikarabati lile jengo liweze kukaa vizuri, basi katika pesa zile zilizotengwa *priority* ipewe lile jengo la Brussels ambalo linakutaka kuwa *condemned*.

Vilevile sisi kama Watanzania tunayo sifa duniani, lakini kama ikiwa tuna viwanja ambavyo tumepewa miaka nenda miaka rudi kujenga Balozi na hatujengi. Tuna kiwanja pale London kimeota magugu kinataka kuwa *condemned* kile kiwanja, ni kwa nini Serikali haiwezi kutumia mfumo wa *mortgage financing* kuweza kujenga Ubalozi wetu pale ukafanya hata biashara ukaweka na maduka na nini na ile pesa ambayo inalipwa kila mwaka. Kila mwaka zinalipwa billioni 21 kwa ajili ya kulipa pango, kwa nini tusifanye *mortgage financing* na hizo pango zikatumika kulipia madeni ya benki. Mimi sijaelewa ni kwa nini, tuna kiwanja Oman miaka nenda miaka rudi. Tunaomba tutumie *mortgage financing*, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Mollel. Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi na mimi niseme maneno machache katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza naunga mkono hoja, cha pili natoa pongezi kwa Wizara kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji na naposema watendaji namaanisha wataalam, hili suala la wataalam nasisitiza kwa sababu wakati mwingine tulikuwa tukichangia humu bila kuzingatia utaalam wa watu ndio maana tunakuwa tumekazana kukosoa. Lakini pia nipongeze Wizara kwa kufuta tozo 54 hii ni historia, watu wengi walitarajia labda vinywaji vitapanda bei na nini lakini sasa naona Mheshimiwa Dkt. Mpango amewapiga chenga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia ile *tax amnestyna* kutolewa kwa *extension* nitoe pongezi na nisisitize tu kwamba Wizara iongeze juhudzi za kufuatili hasa hiyo kodi iweze kupatikana. Lakini pia suala la biashara miezi sita, watu wanaoandikishwa *TIN* kupata ule msamaha kwa miezi sita ni jambo kubwa sana, isipokuwa katika kuchangia hapa nimesikia kuna kitu kinaitwa bajeti hewa. Sasa nilijaribu kujiuliza bajeti hewa ni kitu gani, lakini bajeti hiyo ikashushwa hadi triliioni 29.

Mheshimiwa Spika, kwa kumbukumbu waliosoma ile sura ya bajeti tuliona kwamba viro vyanzo vimewekwa vyanzo hivyo ndio vinakwenda kwenye shilingi triliioni 33 na baadhi ya vyanzo hivyo ni kodi na mapato ambayo tutakutana nayo ambayo sio ya kikodi lakini kuna mikopo ya ndani na nje na kuna misaada, sana sana ninachowea kusisitiza ni kwamba Wizara sasa ifanye *close monitoring* iweze kufuatilia hivi vyanzo hivi viweze ku- *perform* hilo ndio jambo kubwa, kwa sababu kila siku bajeti inakuwa kulingana na mahitaji na kuna *commitment* zinaongezeka kulingana na mahitaji, kwa hiyo hatuwezi kuwa tunarudi nyuma tunasonga mbele. Pia tutambue kwamba katikati huwa kuna *mid review* ambayo huwa inafanyika kuangalia hivi vyanzo vina *perform* vipi, kwa hiyo ni mambo ya kitaalam ndio maana nilisisitiza suala la wataalam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu mimi nikalizungumza kwa sababu nina uzoefu nalo kidogo ni suala zima la *clearing and forwarding*. Suala la kwanza ni kujiuliza kwa nini tulianzisha *clearing and forwarding* na wanatambuliwa na nani, ndio maana wengine waliochangia wakasema kuna *WCO* inawatambua, *East African Custom Management Act* ya mwaka 2004 inatambua jambo hilo, kwa hiyo jambo hilo ni kubwa sana, lakini pia tuangalia historia ya *TRA* zilikuwa taasisi tatu zikaunganishwa ndipo ikatoka *TRA* walikuwa wanafanya kazi vipi na kulikuwa na mapungufu yapi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunakwenda ni suala la *IT system*, kwa hiyo hawa watu wa *clearing* wanatumia mtandao, kwa maana hiyo ni lazima tuangalia hawa watu

tunaosema kila mtu a- *clear* mzigo wake tutamuwekea huo mtandao kwenye simu. Lakini kuna vibali kutoka kwenye taasisi mbalimbali hivyo vibali watavipata kwa utaratibu upi. Kwa hiyo jambo hili tusije tukaliendea kwa pupa lazima liwe na uratibu mzuri na liangaliwe kwa karibu na lengo kubwa Serikali iweze kupata mapato yake, kunaweza kuwekwa *exceptional*/labda kwenye *loose cargo* au mtu amekuja na *television* yake moja *airport* jambo hilo linatakiwa liangaliwe lakini suala la kumbukumbu ni muhimu sana pamoja na kodi suala la kumbukumbu ni muhimu sana. Kwa hiyo jambo likiangaliwa kwa ujumla wake wamezungumza mambo ya ajira, lakini mimi nilikuwa naangalia *modality* ambayo tutakwenda kuitumia ni *modality* ipi kwa sababu hatutaki *ku-frustrate* suala zima la ukusanyaji wa mapato. Hilo ni jambo muhimu, tunaomba Mheshimiwa Waziri uweze kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la kodi ya mafuta; ukurasa wa 60 wa kitabu wanasema kutoa ushuru wa forodha wa asilimia 25 kwenye mafuta ghafi. Mwaka jana tuliongeza kodi hapa, lakini mafuta yameendelea kuja na hakukuwa na upungufu wa mafuta/hakuna *impact* yoyote ya ile hatua iliyochukuliwa na Bunge ya mwaka jana na ziko sababu mbalimbali. mimi baadae nitaleta mapendekezo lakini nilikuwa nafikiri na ninaona hiyo itakuwa ni busara kwenye mafuta ambayo ni ghafi asilimia 25 au dola 250 kwa tani. Pia kwenye mafuta ambayo yako *processed* asilimia 35 au dola 300 *whichever is higher* maana yake kunakushuka wanapokuja ku-declare wanasema bei ya mafuta kwenye soko la dunia imeshuka.

Mheshimiwa Spika, mimi nilijaribu kuangalia takwimu mbalimbali nikaona zile bei kweli zinaonekana zinashuka. Kwa hiyo kama bei hizo zinaonekana zinashuka sisi tunapoteza kipato, kwa hiyo wakiweka ile *tag* ya dola 250 kwa tani au ukiweka *tag* ya dola 300 ina maana Serikali itapata mapato yake. Lakini pia tumezungumza hii sababu hili jambo ni muhimu sana kwa sababu huku tulisema ukurasa wa 62 nanukuu walisema; "ongezeko la ushuru wa forodha

linatarajiwa kuhamasisha uchakataji wa mbegu za mafuta hapa nchini na kuongeza ajira viwandani na mashambani." Sasa kama hilo ndio lengo na tunataka tuongeze uzalishaji wa mbegu hapa ndani na uchakataji lazima tuweke ile *tag* ili kuweza kuhamasisha huku lakini pia ziko *measures* Wizara ya Kilimo inabidi kuchukua ili kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo jambo hili nilipenda kulizungumzia liweze kunufaisha viwanda vyana ndani lakini pia liweze kunufaisha wakulima kwa ujumla wake. Sasa hivi bei ya mashudu nikitoka hapo kuna mbezi ya mashudu kwa mkulima ni shilingi 200 lakini bei hiyo imeshuka kutoka shilingi 400,300 mpaka imefika shilingi 200, kwa nini kwa sababu ya ada na tozo zingine ambazo hazikuzungumziwa kwenye tozo zilizofutwa. Kwa hiyo ningeomba kama ningeomba kabisa ile tozo ya shillingi 20,000 kwa tani iweze kufutwa itakuwa ni hatua kubwa sana. (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Allan malizia.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba Wizara waangalie ili waongeze juhudzi za *formalization* ya *informal sector* kwa sababu huko ndio tutakusanya kodi watu wawekwe kwenye mfumo wa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Allan Kiula. Mheshimiwa Nape Nnauye atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Lubeleje ajiandae.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye mapendekezo haya ya bajeti. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri

na Naibu Waziri na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayofanya, najua wanapitia kwenye mawimbi wakati mwininge, lakini ndio kazi zenyewe zilivyo, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia niipongeze Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti nadhani wamefanya kazi nzuri sana ukipitia *report* yao wameweka mambo mengi ya msingi ambayo wameyashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upande wa Serikali nipongeze uamuzi wa kufuta tozo mbalimbali mlizozifuta, ninaamini nydingi zitasaidia kurahisisha ufanyaji wa biashara katika nchi yetu, nadhani hili jambo ni zuri na ni jambo la kutiwa moyo. Sasa tuende mbele zaidi tukaangalie zile tozo ambazo zina *positive impact* kwa wafanyabiashara na *impact* yake ni kubwa zaidi, hizi ziko nydingi ziko 54; lakini nydingi ni ndogondogo sana na pengine madhara yake yanaweza yasioneokane sana kwa hiyo tuende zaidi ya hapo tulipoenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru sana Serikali kwa kukubali pendekezo la kufuta tozo kwenye visima vile, visima vya watu binafsi nadhani uamuzi huu ulikuwa mzuri, ninaishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mtama, lakini na kwa niaba ya watumiaji wa visima kwa sababu nadhani hii ilikuwa ni kero kubwa, Serikali imekubali, imelifuta naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini sasa Mheshimiwa Waziri nadhani tuende mbali kidogo Kamati ya Bajeti imependekeza msamaha wa kodi kwenye ongezeko la thamani kwenye mitambo ya kuchimba visima vya maji. Kwa hiyo, pamoja na kufuta tozo lakini nadhani sasa fikrieni kwa sababu Mheshimiwa Waziri magonjwa mengi nchini hapa chanzo chake ni maji, lakini mitambo hii ikifutwa kodi, mitambo hii itatumika kuchimba visima, lakini pia itatusaidia kwenye kilimo kwenye kuchimba malambo. Kwa hiyo, ninaunga mkono pendekezo la Kamati ya Kudumu ya Bunge kwamba pamoja na kufuta tozo kwenye visima basi tuende

mbali tufute pia VATkwenye mitambo ya kuchimbia visima.
(Makofii)

Mheshimiwa Spika, ninaunga pia mkono pendekexo la Kamati ya Kudumu ya Bunge wamezungumzia kwa kina mgawanyo wa bajeti yetu. Bajeti yetu kwa sehemu kubwa na Kamati imeeleza, imepeleka fedha nyingi kwenye maeneo ya ujenzi na miradi mikubwa tuliyonayo, sio jambo baya kuwekeza kwenye hii miradi. Lakini sekta ambazo zinahusishwa watu wengi katika nchi yetu ni sekta ya kilimo ndio inahusisha watu wengi sana, karibu asilimia 70 ya Watanzania wanajihuisha na kilimo, lakini kinazalisha ajira kwa asilimia 65, asilimia 85 karibia ya bidhaa tunazouza nje zinatokana na kilimo, lakini inachangia Pato la Taifa kwa asilimia 29 na kwa asilimia zaidi ya 100 chakula cha nchi hii kinategemea kilimo. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ndiyo sekta ambayo ikiguswa inagusa maisha ya watu wengi na tungeweza kupambana na umaskini wa watu wetu kwa kiwango kikubwa. Ukiangalia mtiririko wa bajeti mwaka 2016/2017 kwa bajeti ya maendeleo tulitenga asilimia 1.38 ndio tukapeleka kilimo; asilimia 1.38, sekta ambayo ndio inabeba watu wengi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 tukatenga asilimia 1.25, mwaka 2018/2019 tukatenga asilimia 0.81 na huu ni utengaji sio upelekaji wa fedha, mwaka 2019/2020 tukatenga asilimia 1.17 ya fedha za maendeleo. Sasa hili ndilo eneo kubwa na kupanga ni kuchagua, kama tunataka kushughulika na umaskini wa watu wetu, tunataka kushughulika na watu walio wengi mimi nilidhani vipaumbele vyetu na mgao wetu eneo kubwa la fedha zingeenda huko. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama tumeshindwa kutenga fedha nyingi na upelekaji wa fedha kwenye sekta hiyo ambayo inagusa watu wengi unasuasua, mimi nilidhani ule utaratibu tulioanza nao mwaka 2016/2017 wa kufuta tozo nyingi kwenye eneo la kilimo ili itusaidie tungeendelea nao ingesaidia *inge-replace* hili ambalo tumeshindwa kulifanya

la kutenga fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo. Lakini safari hii tume-*deal* na tozo kwenye biashara, kwenye kilimo tumefumba macho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka tulikuwa tunatenga fedha hapa kwa ajili ya pembejeo, kuna wakati tulifikia mpaka bilioni 200 tumeziondoa, pembejeo hakuna hazipatikani, viwanda vya kutengeneza havipo sasa na bado tozo bado ziko nyingi, pendekezo langu ni kwamba tuende tukazipunguze.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili; wigo wa wawalipa kodi kwa muda sasa imekuwa tukizungumza, kuna takwimu sina hakika kama bado ni hizo hizo kwamba inategemewa walipa kodi wako kama bilioni 14 wanaolipa ni milioni 2.5, kwa hiyo mzigo wa wawalipa kodi wengi ambao walitakiwa kulipa unabebwa na asilimia ndogo sana ya Watanzania. Sasa Mheshimiwa Waziri mimi nilidhani tunganeza hata kama ni kidogo kuupanua huu wigo wa wawalipa kodi tungakuwa tumepeiga hatua fulani na wigo ungepanuka, nimemsikia mama yangu pale akizungumza hoja ya wafanyakazi, tunajua mshahara kidogo hatujapandisha maisha yao yanaendelea kuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, mimi nilidhani tungakuwa tumepanua wigo wa walipa kodi tungeweza kushughulika kupunguza kodi hasa kwa wafanyakazi na hasa wafanyakazi wa chini. Ukichukua takwimu leo wafanyakazi wote nilisikia mama alizisema pale karibu shilingi bilioni 971 zinategemewa kutokea kwenye *pay as you an* ya wafanyakazi wa Serikali. Lakini wako wale wa chini kabisa walimu ambao ni wengi na ndio wanateseka tunategemea shilingi bilioni 194 tungezikata hata kwa asilimia 50 ambayo unapata shilingi bilioni 97, hizi tukazipeleka kwenye chanzo kingine ambacho tumekibuni huu mzigo ungepungua kutoka kwa wafanyakazi na hasa walimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nadhani tungelianza hii hatua tulipo-*introduce* vitambulisho vile vya kitaifa lengo moja wapo ilikuwa ni ku-*formalize* sekta zetu lakini kwa kiasi

gani tumeitumia imetusaidia kwa kiasi gani tusipotanua wigo wa wawalipa kodi tutaendelea kuwabebesha watu wachache mzigo mkubwa wa wawalipa kodi na kwa sababu mzigo unakuwa mkubwa wana-*tendency* ya kujitahidi kukwepa kwa sababu mzigo ni mkubwa sana. Kodi nzuri ni ile ambayo inalipika na inalipika kwa wakati, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nilikuwa napendekeza hebu tuenze basi tutoke hapa tulipo tuongeze wigo wa wawalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa nilizosisoma hapa inaonesha kwamba sekta ya sanaa na burudani imekua kwa kiwango kikubwa, lakini ukweli sekta hii inakua kwa kudra. Sheria, kanuni na taratibu tulizonazo zinazosimamia sekta hii zimepitwa na wakati sana. Sasa lazima ifikie mahali Serikali twende tujikite tuzibadilishe sheria na taratibu zinazosimamia sekta hii ambayo tunakubaliana kwamba inakua kwa kiwango kikubwa basi iendane na wakati, kwa sababu sheria tulizonazo zimepitwa na wakati na hazisaidii ukuaji wa hii sekta. Kwa hiyo mapendekezo yangu moja, tuangalie mgawanyo wa fedha tunaupeleka wapi kule ambako wapo watu wengi nadhani ndiko ambako tulipaswa kupeleka fedha nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni vizuri tukaangalia namna ya kupanua wigo wa wawalipa kodi tusibaki na namba ile tunacheza nayo unarudisha, unajumlisha, unatoa mzigo unakuwa mkubwa sana. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana malizia.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye. Sasa kama nilivyotaja Mheshimiwa Jitu Soni ndio anafuata, Mheshimiwa George Lubeleje ajiandae.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana awali ya yote naomba nichukue fursa hii kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kuniwezesha kuchangia. Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao nzima kwa kazi kubwa na nzuri sana wanayofanya na niwapongeze kwamba bajeti ya awamu hii imeleta matumaini makubwa ni bajeti moja katika bajeti ya hii miaka minne ambayo ni ya mfano kabisa, imelenga kila sekta, lakini imelenga hasa kwa kuwezesha viwanda vya ndani na ukuaji wa uchumi wa ndani kukua kwa kasi kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru kwa kuanza kutekeleza suala lile la *blueprint* kwa kuondoa tozo angalau 54, ni mwanzo tu lakini ninaamini kwamba sasa mtakuja na ile sheria Bungeni ya kuweza kuifanya *blueprint* yote iweze kutekelezwa ili viwanda/biashara ya ndani iweze kukua na tuweze kuzalisha bidhaa na tuweze kushindana kwa bidhaa zinazotoka nje lakini pia bidhaa zetu ziweze kwenda nje kushindana katika masoko mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nishukuru kwamba mmeweza kuendeleza msamaha wa kodi kwa muda wa miezi sita mingine kwa wale ambao ilikuwa bado hawajalipa. Niwapongeze mmeweza pia kupandisha ile *threshold* ya VAT kutoka milioni 40 kwenda mpaka milioni 100 lakini pia wale ambao walikuwa chini ya/waliotakiwa kupeleka mahesabu baada ya milioni 20, sasa ni milioni 100.

Mheshimiwa Spika, ningeomba kwenye orodha hiyo kama inawezekana makampuni ambayo ni *limited*, ambayo hayapo kwenye mfumo huu, ambayo yapo chini ya milioni 100 ni watu wamependa *formalize* biashara zao lakini bado biashara zao zipo chini ya milioni 100 na wao pia waendelee kupata msamaha huo ili pawe na usawa. Mtu anaye-*formalize* asiadhibiwe na lengo kubwa ni kutoa sekta isiyo rasmi kuwa rasmi. Kwa hiyo, pangekuwa na vivutio zaidi kwa sekta ambayo watu wamejirasmisha basi wao wapate vivutio zaidi ili wengi waondoke huko kwenye sekta isiyo rasmi na kurudi kwenye sekta ambayo ni rasmi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze kwa kushusha kodi ambayo haijasemwa na watu wengi, mmeshusha vile viwango vya kodi kwenye *presumptive tax* kutoka 150,000 kwenda laki tatu na kitu, kwa hiyo kodi zimeshuka. Kwa hiyo, wafanyabiashara wengi sasa wataweza kulipa zile kodi na hawatafungiwa biashara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine kwamba tunaomba mkija sasa wakati wa *Finance Bill* tuweke utaratibu wa kuwa na *one stop center* badala mtu kutafuta leseni na vibali maeneo mbalimbali kama ilivyo kwenye *TIC* kwa wale wanaojisajili *TIC* wale wa nje, sasa na sisi wa ndani kupitia Afisa Biashara wa Mkoa na Wilaya, tukienda tukilipa sehemu moja, tozo na ada zote ulipie sehemu moja unaachana nao mpaka mwakani, sasa huko Serikali ijue kwa sababu yote inaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, wajue namna ya kugawanya hizo tozo na ada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado nasisitiza *blueprint* usipoitekeleza bado hatutakuwa tunaweza kushindana kwa bidhaa zetu kwenda nje wala humu ndani, lakini ni hatua moja nzuri mmeanza nayo, niwapongeze lakini naomba hiyo sheria ije mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni muhimu, mnakusanya fedha vizuri lakini bado matumizi mabaya yapo kwa mfano *GPSA*, *TEMESA* lakini pia *TBA*, hayo ni maeneo ambayo haya mabilioni mnayokusanya wanaenda kuyatumia vibaya, ni kichaka ambacho kimejificha ambapo kwa mfano *TEMESA* ukipeleka magari ya Halmashauri kutengeneza pale ni kero kubwa, unaweza kutengeneza kwa nusu ya bei na kwa viwango vilevile tukiwa tunatengeneza nje hivyohivyo katika majengo ya Serikali na nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo muichunguze *TEMESA* na *GPSA* hiyo Sheria ya Manunuzi wanapanga watu wakuwa-supply 10 kwa mfano kwa mwaka mzima. Iwe ni wazi *GPSA* ibaki ku-regulate kwamba kama *BOT* wanaangalia bei za *foreign exchange* na nini ni ngapi, *GPSA* ibaki ku-regulate bei, lakini iwe wazi kwa mtu yejote, saa yejote tenda

ikitolewa waweze kujaza ndiyo mtaona manufaa, *value for money* itapatikana. Kwa hiyo, *GPSA, TEMESA, TBA* muwaondoe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu lingine, undeni *Tanzania Regulatory Authority, upper stream, lower stream* ili wote wawe chini ya taasisi moja na wao wote waweze kufanya ndiyo mtawezza kuondoa kodi, tozo, ada na ushuru mbalimbali nyingi, lakini pia wafanyabiashara wengi wanaomba kwamba hizi *regulatory bodies* badala ya kwenda kupiga faini za ajabu ya kwanza watoe onyo na kuwaambia rekebisha, ya pili iwe ni onyo kali zaidi na ya tatu ndiyo iwe faini, siyo mara ya kwanza anakuja anakufungia biashara anakutoza faini za ajabu, hapo ndiyo tutaona lengo lao kuu ni kufanikisha watu wafuate sheria na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu lingine ni kama Kamati ya Bajeti ilivyopendekeza na siku zote tunapendekeza suala la kuondoa kodi kwenye mitambo ya maji na mitambo ya kuvuna maji ya mabwawa na malambo. Hii itasaidia watu wengi zaidi kuwekeza kwenye sekta binafsi badala ya kutegemea Serikali ifanye mambo yote haya kwenye umwagiliaji, maji ya kunywa, maji ya mifugo na mabwawa ya samaki na bado tukitengeneza hayo mabwawa, athari tunayopata ni uharibifu wa yale maji ya mafuriko kuharibu miundombinu itakuwa haipo, kwa hiyo mkiondoa.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwa wale ambao wanapata msamaha ni makampuni makubwa na miradi ya Serikali, lakini mtu binafsi hapati hiyo. Hasa upande wa kilimo hatuwezi kupata kwa sababu bidhaa zetu hazipo *vitable*, kwa hiyo *vital on deferment* kwenye *capital goods* sisi hatupati. Kwa hiyo, nivizuri mkatuondolea ili watu wengi binafsi pia waweze kuleta mitambo ya maji na tuweze kusaidiana na Serikali kuboresha huduma ya maji kwa pande zote.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine tunawashukuru na tunawapongeza mmeweza kuondoa kodi kwenye vifaa au mashine za kuchonga vito, *lapidary* na za kutengenezea

jewellery. Tunaomba sasa mfike hatua ya pili kwa sababu hatua ya kwanza mmeondoa *duties*, mngeondo na VAT kabisa ili sasa zile mashine ziwe za bei nafuu na Watanzania wengi watakaopata mafunzo pale *Gem Center* pale Arusha basi waweze kupata hizi mashine kwa bei nafuu zaidi. Kwa hiyo, mngeweza katuondolea kodi kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru kwamba mmeondoa kodi kwenye *refrigerated trucks* kwa ajili ya *horticulture*, lakini tunaomba mngetanua wigo zaidi ili uweze kuhusisha pia sekta ya maziwa, nyama na samaki kwa sababu bidhaa hizo mkiweza kuondoa kodi, wale wavuvi hawatahitaji kuuza samaki wao wanapovua, wanaweza kuzi-*refrigerate* kwa bei nafuu kwenye *containers* ambazo zitakuwa *refrigerated* za ushirika na hata wale wa kuku badala ya kuuza kuku kwa haraka kwa bei ya chini, wanaweza kuwa-*process* na kuwaweka kwenye *fridge* wauze taratibu ili mkulima aweze kufaidi moja kwa moja. Kwa hiyo, pamoja na kuwa mmesaidia Sekta ya *horticulture* mngetanua wigo kwenda kwenye maziwa, samaki na lakini pia kwa upande wa nyama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni ombi la kuondoa kodi kwenye *solar waterpumps* itasaidia sekta ya maji kwa upande wote lakini pia ukileta kama umwagiliaji, kodi hizo hazilipiwi lakini ukileta hivihivi bila kutaja umwagiliaji ina kodi. Kwa hiyo, inaleta usumbufo mkubwa, mngeziondoa ili sekta nzima ya maji iweze kupata...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Ahsante, nashukuru na naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze la kwanza kwa kuishukuru Serikali, tangu nimeingia Bungeni mwaka 1990 naiomba Serikali ijenge barabara ya kutoka Mpwapwa kwenda Kongwa mpaka Mbande kwa kiwango cha lami, sasa baada ya miaka 25 naishukuru sana Serikali mwaka huu imekubali kujenga barabara ya lami kutoka Mpwapwa kwenda Kongwa mpaka Mbande. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kusikiliza kilo cha wananchi wa Mpwapwa cha muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, jukumu/kazi yetu sisi Wabunge tupo hapa kuitisha Bajeti ya Serikali na mimi nina hakika bajeti hii itapitishwa bila kupinga, nina hakika kabisa tutapitisha bajeti, lakini Mheshimiwa Waziri, tunapitisha bajeti lakini jambo la kushangaza kwa sababu mikoa inapangiwa bajeti yake na Halmashauri inapangiwa bajeti yake, lakini jambo la kushangaza hizi fedha zote ambazo zinatengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazifiki zote, kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano, katika Mkoa wa Dodoma mwaka 2017/2018 tulitengewa shilingi bilioni 35 lakini mkoa ulipewa shilingi bilioni 15, asilimia 43 tu na mwaka 2018/2019 tumetengewa karibu shilingi bilioni 46, tumepewa shilingi bilioni 30. Sasa na ndiyo maana miradi mingi inakwama, mikoa mingi.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri mimi nipo kwenye Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na ndiyo tunachambua bajeti ya mikoa yote, bajeti ya Serikali. Hakuna mkoa ambao fedha zinazopitishwa na Bunge mkoa unapata zaidi ya asilimia 60. Sasa tutatekelezaje hii miradi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama fedha zote hazifiki basi angalau Mheshimiwa Waziri uwe unatueleza kwamba fedha hazikwenda zote kwa sababu moja, mbili, tatu; kama kuna majanga yametokea, milipuko ya magonjwa imetokea au kama kuna jambo lolote. Lakini kama hutuelezi na wananchi kule wanahoji, mmeahidi kuchimba visima vyta maji, havichimbwi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna miradi inayoendelea Wilaya za Mpwapwa na Kongwa, Jimbo la Kibwakwe, lakini miradi inachukua muda mrefu kukamilika kwa sababu fedha hazipelekwi na wakandarasi hawalipwi. Kwa hiyo, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, fedha ambazo zinapitishwa hapa kwa ajili ya miradi ya maendeleo mikoani na Halmashauri zipelekwe zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna miradi kwa mfano ya vituo vyta afya na zahanati, mwaka jana mlilitahidi katika Jimbo la Mpwapwa nilipata fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Mima, nashukuru. Lakini mwaka huu Jimbo la Mpwapwa sikutengewa fedha kujenga hata kituo kimoja cha afya na mimi nimeombwa kituo cha afya ambacho kimeanza kujengwa sasa miaka kumi, Kituo cha Afya Mbori.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mbori ni muhimu, kituo hiki kikikamilika watakaohudumiwa pale ni wananchi wa Chamkoroma, Tubugwe, Mseta, Matomondo, Mlembule, Mpeta, Godegode na Kimagai. Hiki kituo kitahudumia watu wengi. Sasa kama sikupata fedha ya kujenga kile Kituo cha Afya cha Mbori na Kituo cha Afya cha Belege, nitafanyaje? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana kituo hiki tupewe fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni barabara; nimezungumzia barabara ya lami kutoka Mpwapwa kwenda Kongwa – Mbande lakini kuna barabara kwa mfano barabara ya kwenda Mima kutoka Mpwapwa – Gulwe-Belege – Chitemo – Mima unakwenda Igoji I, Igoji II, Isalaza pale mpaka Seruka. Mheshimiwa Spika wewe umekaa Mima,

unaifahamu sana hii barabara; hii barabara ni muhimu. barabara hii kuna kata nane zinahudumia barabara hii, barabara hii haipitiki, inapitika kwa shida. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati hii barabara ya kutoka Mpwapwa kwenda Mima mpaka Seruka. Hii *light grading* haitatusaidia, tunataka *heavy grading* barabara ilimwe, ishindiliwe, ijengwe na mifereji ili iweze kuhudumia wananchi wa maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji; katika Jimbo la Mpwapwa na Jimbo la Kongwa kuna miradi mingi ya umwagiliaji, lakini miradi hii sasa kuta zote zimebomoka, kwa hiyo miradi hii haifanyi kazi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Wizara ya Kilimo ifanye ukarabati wa miundombini hii skimu za umwagiliaji ili wananchi kwa mfano wa Kata za Matomondo, Chamkoroma, Tubugwe kule pamoja na Lumuma na Malolo, hizi skimu za umwagiliaji zitasaidia sana. Kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wetu katika Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa ili kuondokana na tatizo la njaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono asilimia mia moja, asante. (*Makof*)

SPIKA: Tunakushukuru sana Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Seneta. Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nianze kwa maneno ya mshairi yafuatayo na naomba Waheshimiwa Mawaziri wanisikie namna gani mshairi huyu aliiasa nafsi. Alisema; huku giza lajikita nafsi yangu inuka, inuka uje nakuita nafsi yangu itika, sikuiti kwa kukuteta nafsi yangu isijeshituka. Akasema, nakuita uje na zibo nafsi yangu isijeziuba, kama hakiyo ni robo, nafsi yangu kilo epuka, siwe na matobotobo nafsi yangu utaaibika, nakuita uje na fungo nafsi yangu isijefunguka, umeumbwa

kwa udongo nafsi yangu utaondoka, basi uache maringo nafsi yangu juu tauka. Unijie na stara nafsi yangu umesitirika, uje ukitia idhara nafsi yangu utaumbuka, maisha ni msafara nafsi yangu unakumbuka, usinijie na hasira nafsi yangu utaathirika, usinije na papara nafsi yangu utanichoka, bali uje na subira nafsi yangu utatukuka, kama waja na kiburi nafsi yangu bora geuka, kwangu uje na hadhari nafsi yangu utasalimika, yadhahiri ama siri nafsi yangu yameandikwa. Haya basi, anasema haya kuwa msikivu nafsi yangu semezeki, dunia mti mkavu mara waweza kung'oka, huwabwaga wenye nguvu nafsi yangu utanusurika...

SPIKA: Mheshimiwa Yussuf bajeti sasa.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nimeanza maneno haya kusudi madaktari wetu hawa wa uchumi wanisikie. Kwa muda wa miaka mitatu mfululizo tulikuwa tunaionesha Serikali namna gani uchumi wetu unaanguka, namna gani tunapata hasara, namna gani maisha ya Watanzania yanakuwa magumu lakini kiburi, dharau na jeuri kikawa ndiyo kimewatawala madaktari wetu hawa wa uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tulisema mfumo wao wa kodi zilizopitiliza kiasi zinaua biashara, tukasema binafsi nimesimama kwa *microphone*hi na kitu hiki nilichokaa mwaka jana nikawaambia zaidi ya hoteli 56 pale Kariakoo zimefungwa na majumba yamebadilishwa matumizi. Kwa hiyo, hakuna wageni wanaoingia, mabasi yaliyokuwa yanaleta wageni wale hayana kazi, wafanyakazi waliokuwa pale hawana ajira, *porters* waliokuwa wakifunga mizigo hawana, *restaurant* zile hazifanyi kazi, wakawa hapa wanakuja na maneno ya kwamba wao wamejidhatiti na wapo vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka mitatu Mwenyezi Mungu ameleta rehema zake, Rais ameona kwamba nchi inadidimia, amekutana na wafanyakabiashara tulikuwa tukiyaeleza sisi kwa muda wa miaka mitatu, lipi ambalo

wafanyabiashara hawakumweleza Mheshimiwa Rais?
(Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wajitathmini madaktari hawa wana haki ya kuwepo pale kama ni waungwana, kama ni waungwana wajiuzulu kwa sababu kila kitu tuliwaeleza na tukawashauri na wakaleta dharau kwamba wao wamejipanga katika uchumi. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, jana mchangiaji mmoja amesema kwamba miradi hii tunayofanya mikubwa ni mizuri na inatakiwa ifanywe; well, ndivyo, lakini katika uchumi wetu huu? Niliwapa mfano kwa sababu wameleta mtaalam wao mmoja hapa akatupa semina anatupa mifano kutoka Wizara yao hiyo ya Biashara anatupa mifano tunamuuliza maswali anakwepa. Tukawaeleza namna gani Sweden/nchi za Scandinavia zinakuza uchumi wao tukawaeleza Waheshimiwa Mwenyezi Mungu mkubwa, juzi kuna shirika moja hili la mawasiliano limempa Rais shilingi bilioni tatu, Airtel wamempa Rais shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Spika, sasa tuchukulie mashirika yote ya simu yafanye vile, tuwe na viwanda 20 vifanye vile, tuwe na makampuni ya kilimo na wachimba madini wafanye vile, ndiyo Sweden inavyoendesha uchumi wake. Ile bajeti yao yote ni zile *donations* zinazotokana na wafanyabiashara na zinatokana kwa sababu wameweka mazingira sawa/wezeshi na uwazi katika biashara zao. Kwa hiyo, mfanyakibashara hana hofu ya kufanya biashara yake, anafanya biashara, inapofika mwisho wa mwaka anafanya hesabu anaichangia Serikali yake. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, sasa fedha ile inatosha wao kwa bajeti yao na *surplus* ile ndiyo wanatusaidia sisi katika nchi zetu. Kwa hiyo, ile *income* inayotokana na makusanyo ya Serikali ndiyo wanakuja kwenye miradi yao mikubwa kama ya kwetu hii ya *Stiegler's* au *SGR* na ndege. Sasa sisi tunaichukua bajeti ndogo tunayokusanya ambayo haitoshelezi tunaiingiza kwenye miradi mikubwa, unawakuta

Watanzania leo wana-suffer katika maisha ni kwa sababu ya mipango yenu mibaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na tulikuwa tukiwashauri humu ikawa hapa Mheshimiwa Dkt. Ashatu anakuja hapa anatushikia kiuno anakwambia Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imejidhatiti, hatuna hofu, tutakwenda hivi na hivi. Leo baada ya miaka mitatu kwa nini mnaramba matapishi yenu? Kilekile tulichokuwa tunakieleza mnakikataa leo mnakirudia, kwa nini mnaramba matapishi yenu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wataalam hawa ndio kweli wanamshauri vibaya Rais na wanatupeleka kubaya...

SPIKA: Mheshimiwa Yussuf, mimi naona unalaumu lakini husemi *concretely* ni maeneo gani, ni kitu gani, yaani unapiga lawama za jumla tu.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nimesema, nilisema mwaka jana hapa kodi ya kontena moja milioni 40 pale bandarini inatuulia biashara yetu na wafanyabiashara wanachukua kontena hilo hilo, linapita *as a transit* likifika Uganda wanalipa milioni kumi biashara ile ile inarudi, haya mashati na vitenge tunavyouziwa hapo nje na mashuka vinatoka Uganda, vinapita hapo, niliyasema hayo. Jeuri na kebehi ikaja hapa hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuwashauri tena wachumi wetu hawa, wapi tutapata fedha ili kuokoa hapa tulipo. Kuvunja ni mara moja, lakini kujenga inakuchukua muda mrefu, wametuulia uchumi kwa muda wa miaka mitatu, si kazi rahisi kuujenga uchumi. Nilisema huwezi kuona maendeleo ya Taifa kiuchumi kwa miaka mitano au kumi, siyo rahisi, nilisema. Kwa sababu kama Taifa kujenga uchumi ni kitu kimoja kinahitaji mipango na muda mrefu, nilisema hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nawaonesha; la kwanza, Mheshimiwa Mattar siku zote anapiga kelele kuhusu uvuvi wa bahari kuu. Meli moja ya uvuvi kwa utafiti uliofanywa inaweza

ikaingizia Serikali yetu dola milioni 65 kwa mwaka. Hayo yanazungumzwa tu, hayajafanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tutaimarisha utalii katika ukanda wa bahari huu, utalii wa fukwe, tukafanya *diving*, *snorkeling*, *fishing*, utalii wa historia, utalii wa kiutamaduni, pato la utalii, *GDP* ya Taifa inaweza kutoka asilimia 17 hadi asilimia 40 kwa muda mfupi sana. Kinachohitajika hapa katika utalii ni *triangle*, vitu vitatu tu; waweke pamoja jamii, iweke pamoja wawekezaji (*serious investors*), ikae na Serikali waweke mfumo ili sheria zisigongane, *serious investors* waje wawekeze tuta-*boost* uchumi wetu. Tunawaeleza hilo la pili tunapiga kelele mwaka wa tatu, bado hakuna mkakati wowote wa utalii uliopangwa katika ukanda wa bahari kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, biashara ni lazima uweke mazingira wezeshi, uweke mazingira ya uwazi. Mtanzania awe ana uwezo wa kujua nakwenda kuchukua simu hii China, nainunua shilingi ngapi, ntailipia kodi shilingi ngapi awe anaweza kufanya kulekule...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Yussuf, malizia.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, mimi nimewashauri na wakiwa tayari ntawashauri wataalam wao waliosoma Amerika wametudanganya na tuliwauliza maswali wakajibu, tutawapa mifano ya nchi mbalimbali. Sisi hatukusoma, na Mheshimiwa Marehemu Karume alituambia tumesoma hatukujua, tumejifunza tumetambua. Tukienda huko kwa wenzetu tunajifunza kwa nini waendelee sisi tukwame; kwa nini, tunajifunza hayo mambo. Kwa hiyo tunapowashauri Waheshimiwa tunaomba muwe wasikivu. Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu na mimi pia nichangie Bajeti Kuu ya Serikali yaani mapato na matumizi kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi sana kwa Wizara hii, hasa kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Kijaji na Katibu Mkuu - Ndugu Doto James, na wengine wote wataalam wa Wizara hii ambaao wamekaa na kuandaa bajeti hii ambayo kwa kweli imekidhi viwango, lakini pia imekidhi matakwa ya wananchi wa Tanzania na vilevile itatuvusha hapa tulipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeshuhudia upande wa pili kule wanaongea mambo mengi sana. Jana mtu mmoja alijikita katika kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango na mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Ashatu hawafai na waondolewe katika nafasi hizo. Lakini hiyo ni dalili ya rangi mbili waliyonayo hawa wenzetu, wamesema sana, lakini mimi nashuhudia kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango na wenzake, timu hii ndiyo bora kabisa katika utawala wa Tanzania, na ninawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile wenzetu hawa kwanza wanasema bajeti hii imepangwa vibaya na Mheshimiwa Dkt. Mpango hafai, lakini ukikutana nao kule nje wanaungana na wananchi ambaao wanasema bajeti hii ni nzuri sana. Kwa hiyo, wao wanashindwa kujifaragua peke yao wanajiunga na wananchi ambaao wanasema bajeti hii ni nzuri na hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango na hasa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alimteua Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake kufanya kazi hii ngumu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sungura mdogo hatuwezi kumgawa watu wote sawasawa akatuenea na

kushiba, lakini tukubali kwamba kazi hii siyo rahisi, mtu yejote akivaa viatu vya Mheshimiwa Dkt. Mpango na mwenzake Mheshimiwa Dkt. Ashatu, atapata tatizo hili ambalo tunalipata kwamba hela hii haitoshi na kinachopatikana tunakigawa sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye kuchangia bajeti hii na nianze na umuhimu wa sekta binafsi hapa nchini. Sekta binafsi nchini hapa ndiyo inayojenga vitega uchumi vikubwa, kwa mfano barabara na hivi karibuni viwanja vya ndege, na mfano *Terminal III* ambayo inakusudiwa kuingiza hela nyingi sana kutokana na ndege zitakazotua pale, watalii na abiria ambao watalipia gharama za kiwanja hicho. Na mimi ni--*declare interest* kwamba katika *local content* ya kiwanja hicho, Kampuni ya Ulinzi na Usalama iliyofunga mitambo pale ni *SSTL Group* ambayo ni kampuni yangu.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi pia inajenga vitega uchumi vingine kwa mfano reli inayojengwa na Yapi Merkezi ni kampuni binafsi, lakini vilevile umeme wa Rufiji unajengwa na sekta binafsi; lakini pia umeme wa *REA* nchini hapa unajengwa na sekta binafsi. Kwa hiyo sekta binafsi hii ina miradi mingine kadhaa. Namuomba Mheshimiwa Dkt. Mpango aipe umuhimu wake kama uti wa mgongo kama ambavyo katika nchi nyingine imepewa. Sisi hapa uti wa mgongo huu wa sekta binafsi umepinda na hauna nguvu yoyote na sasa unalegealegea sana. Mheshimiwa Dkt. Mpango, uimarishe sekta binafsi ya ulinzi ili iweze kuchangia barabara katika kukuza uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana tumelisema sana na ni--*declare* pia mimi ni mwajiri vilevile ni suala la *SDL*. Mheshimiwa Dkt. Mpango hili tumelisema sana. Sisi tunashindwa kufanya biashara hapa kwa sababu ya kitu kinachoitwa *ease of doing business*; asilimia 4.5 ni kubwa kuliko *SDLs* zote duniani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapa Afrika Mashariki ni Kenya tu wana-*charge* sekta ya utalii asilimia 1.2, kwengine kote Uganda hakuna, Rwanda hakuna, Burundi hakuna, kote na

dunia nzima Tanzania ina-*charge* asilimia 4.5, ni kubwa sana. Tunaomba utakapokuja kufanya majumuisho yako, hebu fikiria upunguze hata kidogo. Tumetoka mbali, tulikuwa na asilimia sita, lakini tunakuomba uipunguze taratibu, hatusemi mara moja, lakini fikiria hata kupunguza kiasi kidogo, sisi waajiri na wafanyabiashara tutafurahi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili limeletwa pia Serikalini, katika mambo ambayo Mheshimiwa Rais alitaka yaletwe *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)* na waajiri tumekuletea hili suala la *SDL*, lipunguzwe hata kidogo. Tafadhalii utakapokuja kufanya majumuisho yako tupunguzie *SDL* kutoka asilimia nne kwa kiasi chochote kile ambacho utaona kwamba hakitaumiza bajeti.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la *VETA*; *VETA* ilipobuniwa ilikuwa katika Wizara ya Kazi na madhumuni yake ni kufundisha wafanyakazi *skills*. Lakini sasa *VETA* imehamishiwa kwenye Wizara ya Elimu ambayo inafundisha elimu. Sisi waajiri ambao tunachangia mfuko huo kwa zaidi ya shilingi bilioni tisa kwa mwezi tunaona kama zile hela zinapotea. Lakini pia imekuwa inachukua watoto badala ya wafanyakazi ambao walikusudiwa kwenda kuongeza ubunifu na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la *REA*; *REA* hii haiendi vizuri kwenye jimbo langu. Mimi nina vijiji 87, katika *REA* III(i) nilipewa vijiji 18 mpaka leo hii vijiji vitatu tu, Mheshimiwa Dkt. Kalemani vijiji vitatu tu ndiyo vimewashwa katika 18, asilimia 16, basi na muda unakwenda. Lakini mbaya zaidi hata nyumbani kwa Mbunge umeme hakuna, nimesema, nisemeje sasa ili mnielewe?

Mheshimiwa Spika, lipo suala la mwihsso ambalo pia namuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango alifikirie kupunguza matumizi. Balozi zetu kule nje tunapanga nyumba na nyumba hizi ni ghali sana. Asilimia zaidi ya 60 ya matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje inakwenda kupanga majengo na tunadaiwa hatupeleki hela kule, tujenge majengo yetu kwa njia ya *mortgage*. Tukianza kujenga majengo kwa muda

wa miaka kumi kwa mkopo na tuna-*mortgage* majumba yaleyale, baada ya miaka kumi tutakuwa na nyumba zetu.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri hapa Tanzania, Mabalozi wangapi wamepanga? Wamejenga nyumba zao na sisi tuone mbali, Mheshimiwa Dkt. Mpango, punguza matumizi ya Wizara ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kujenga nyumba zetu. Mimi nilikwenda kuangalia kiwanja ambacho tulipewa Muscat, kwa gharama yangu, nimefika kule Muscat jiwe la msingi limewekwa na Mheshimiwa Dkt. Kikwete. Leo huu mwaka wa ngapi tangu Mheshimiwa Dkt. Kikwete aondoche. Mpaka tunaona aibu tumekwenda kuondoa kile kibao limekuwa pori.

Mheshimiwa Spika, lakin pia tulipopewa kiwanja cha Kenya tulibadilisha kiwanja cha Kenya Ubalozi hapa, wenzetu wamejenga Ubalozi wa Kenya wanafanya matengenezo ya kawaida. Sisi kile kiwanja cha kwetu Kenya mara kitakiwe kuuzwa, Mzanzibari mmoja akaenda kukichukua akapeleka mahakamani; kwa nini tusijenge nyumba zetu kwa mkopo kutumia *mortgage system*? Jambo hili litatusaidia sana kuondoa madeni yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie bajeti hii. Naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige. Mheshimiwa Hussein Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Kalanga Laizer.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Jambo la kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kutufikisha kutimiza wajibu wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuonesha katika bajeti ya mwaka huu dhamira ya kuanza safari ya kufanya *reforms* katika mambo ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na

Wabunge na Watanzania kwa muda mrefu. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana, hasa suala la kutengeneza *demarcation* ya *line* katи ya *TBS* na *TFDA* katika hatua ya awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Profesa Kabudi kwa namna walivyo-*handle* suala la Airtel na kupelekea Serikali kupata 49% *share*. Wameli-*handle* jambo hili *in a civilized and professional way*. Nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri, na niiombe Serikali kwa ujumla wake; tunapo-*handle* masuala ya *private sector* *this is the best way* ya ku-*handle* wawekezaji wa ndani ama wa nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nisisitize tumepata *share* asilimia 49 katika Airtel. Ombi langu, kwa kuwa tunakuwa sehemu ya bodi, tunakuwa sehemu ya *management*, ikija *obligation* ya *investment* kwa sababu kwa takwimu, Airtel *is not making profit*, ikija suala la *investment* na *Telecom Sector* inabadilika kila siku hakikisheni mnawekeza kama wadau wengine waliokuwa *partners* katika *business*, *this is very important*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu kuhusu Airtel; Serikali ina *TTCL*, nimemsikia Mtendaji Mkuu wa *TTCL* akisema siku moja kwamba utakapokwenda maeneo ambayo hakuna mtandao wa *TTCL* unaweza ukafanya *roaming* kwa kutumia Tigo, *it is wrong in business*. Sisi tutakuwa tunalipa sana kumlipa Tigo kwa sababu tunatumia *infrastructure* yake. Ninawashauri, ingieni makubaliano na Airtel ambayo mna 49% kama Serikali ili tutakapokuwa maeneo ambapo *TTCL* haipo itumie *infrastructure* ya Airtel kufanya mawasiliano kwa sababu itakuwa ni *within the circle* ambako ninyi mna-stake.

Mheshimiwa Spika, nitoe maoni yangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Nimesoma hotuba ya Waziri, nimesoma hotuba za Wizara tatu ambazo tunazitarajia kuwa ndiyo *input* kuweza ku-*attain* malengo yaliyoko katika hotuba ya Waziri; nimesoma hotuba ya Wizara ya Wizara ya Kilimo, nimesoma hotuba ya Wizara ya Mifugo, nimesoma hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nape ameongelea Sekta ya Kilimo, nataka tu *on record* ukichukua *total development budget*/tuliyotenga mwaka huu ya shilingi trillioni 12, uka-*compare* na kile ambacho tumekitenga katika sekta ya kilimo na mifugo ambazo kwa ujumla wake zinachangia zaidi ya asilimia 30 ya *GDP*yetu. Fedha tulizotenga kwa ujumla ni shilingi bilioni 161 wakati *development budget* ni shilingi trillioni karibu 13. Hii ni sawasawa na asilimia 1.3; hatuwezi kupiga hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hoja yangu ni nini; nimesoma *monetary statement*, hii hapa ya *BOT* na ninaomba ninukuu maneno; *BOT* wanasesma; *global economy* itashuka kutoka 3.6 kwenda 3.3 kwa sababu ya *trade war* iliyopo kati ya China na Marekani. Sasa sisi kwenye *global economy who are our trading partners and what are we selling?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunauza mazao ya kilimo na ninaomba niyasome hapa; zao la tumbaku, limeshuka kutoka *1.2 million kgs tuna-project* mwaka huu 2018/2019 tutakuwa na tani 50,000 ndiyo tutakayoenda kuuza kwenye soko la dunia. Korosho mwaka 2016/2017 ilikuwa tani 265,000; mwaka 2018/2019 tani 224,000; mkonge kutoka tani 36,000 sasa tuna-*project* tani 15,000; chai kutoka tani 26,000 tunakwenda tani 19,000; sukari kutoka tani 330,000 tunakwenda tani 327,000; pareto kutoka tani 2,150 tunakwenda tani 1,800. Zao pekee ambalo tuna-*project* *ku-grow* ni zao la kahawa kutoka tani 48,000 kwenda tani 61,000; pamba na yenyewe tunajua kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa nini ninachotaka kusema Mheshimiwa Waziri wa Fedha umempa *Commissioner General* wa *TRA target* ya kukusanya *1.7 trillion shillings*. Mheshimiwa Waziri *Commissioner General*/hawezikukusanya na huyo utamtumbua. Nasema haya *in very good faith* kwa sababu ili tukusanye kodi ni lazima tuzalishe, ili tukusanye kodi ni lazima tufanye biashara. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni nini; ukienda kwenye *lending*, kutoka mwaka 2016 mpaka mwaka wa

fedha 2018/2019 sekta ya kilimo uwekezaji wa mikopo umeshuka kutoka asilimia 11 mpaka -4; sekta ya *manufacturing* kutoka asilimia 20 mpaka 17; sekta ya *transport* kutoka asilimia 27 mpaka asilimia 4; *building* kutoka asilimia 9 mpaka -2; *trade* kutoka 2.2 mpaka -2.1; *hotel and transportation* kutoka asilimia 7 *lending* kushuka mpaka -1.6%.

Mheshimiwa Spika, nini kitakachotokea; *excise duty* zitashuka, *VAT* zitashuka, *consumption taxes* zote zitashuka na Mheshimiwa Rais wakati anaongea na wewe Mheshimiwa Waziri na wataalam wakati anaongea na wafanyabiashara, alisema kodi za ndani zinashuka na kodi za ndani ni zipi; kodi za ndani ni *VAT on consumption* za ndani; kodi za ndani ni *PAYE*, kodi za ndani ni *excise duty*, hizi zote ziko *related* na biashara. Kama hatutafanya *proper harmonization* na *regulation* kwenye biashara hatuvezi kutoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, sasa hatua ya kwanza ninayokuomba na ninajua hii utakumbana na matatizo Serikalini, fanya maamuzi yafuatayo; muite Waziri wa Viwanda na Biashara, kaa naye, muombe mfanye mabadiliko makubwa. Tuna sheria hapa; tuna Sheria ya *CARMATEC*, tuna Sheria ya *TIRDO*, tuna Sheria ya *EPZA*, tuna Sheria ya *TanTrade*, tuna Sheria ya *TEMDO*; hizi taasisi zina-*contradict* zenyewe. Fanyeni *harmonization*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili; mtu yejote anapotaka kusajili biashara hatua ya kwanza anayofanya ni kwenda sehemu inatwa *BRELA*, *BRELA* ni kifupi cha *Business Registration and Licensing Agency*. Ushauri wangu, chukueni Sheria ya *BRELA*, hizi taasisi zote ziwekeni mle ndani, anzisheni kitu kinachoitwa *Business Registration Licensing and Regulatory Authority*. Ili mtu anapoingia kusajili biashara, kuchukua leseni, anakutana na kila kitu mle ndani, akitoka anakwenda kufanya biashara yake. Uta-reduce *bureaucracy*, uta-reduce *cost of business*. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Bashe una akili wewe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, la pili angalia kitu hiki Mheshimiwa Mpango *GDP contribution*, sekta iliongoza kukua ambayo ni ya sanaa inachangia 0.3% hii ndiyo imekua, imeongoza kukua katika uchumi wetu, sekta inayokua ambayo inachangia asilimia kubwa ya *GDP*, sekta ya kilimo imekuwa kutoka 3.7% kwenda 5% *marginal growth is less than population growth*, hamuwezi ku-break through.

Ushauri wangu tuhakikishe tuwe na mpango na mimi hili linanisikitisha, ukisoma mpango wa maendeleo huwa hapa tulioipitisha hauna *smart objective*, tunapozungumzia *smart objective* ni lazima ziwe *measurable*, unazalisha pamba kutoka tani 200,000 kwenda ngapi? Unazalisha tumbaku kutoka tani moja kwenda ngapi? Unazalisha kahawa kutoka wapi kwenda ngapi? Usipofanya namna hii hamuwezi kujipima, hatuwezi kujipima...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, namalizia kwa neno moja, naomba niseme hivi yupo hapa tulikuwa *handsome boy* Wazirage aliasisi *cotton to clothes*, ule mpango umeishia barabarani, aliasisi mpango wa *leather to leather product* umeishia barabarani, aliasisi mpango wa mbegu za kunde, mazao ya mbegu za kunde mpango umeishia barabarani. Mheshimiwa Waziri tunawaomba tulifanya mabadiliko mwaka 1967 kwenda kwenye uchumi wa kuhodhi wa Serikali, tukafungua masoko 1990s kwenda 2000 umefika wakati wa kupitia mfumo mzima wa Serikali, badilisha Sheria ya *Income Tax*, badilisha Sheria ya *VAT*, badilisha *Tax Administration Act*, usipofanya namna hii hauwezi kufikia malengo tuliojiwekea ni lazima tuwe *production oriented* / *kuliko tax oriented* kwenye uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ombi moja kwa heshima yako na kwa kiti chako, Waziri umetangaza hapa wafanyabiashara

wasikamatwe, Nzega kwangu imetua *tax force* wiki iliyopita na kamji kale kadogo, wamekamata wafanyabiashara saa hizi wako polisi zaidi ya wiki, pale Wizarani kwako Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti niseme Waziri amekuwa mwalimu na dada yangu Ashatu mwalimu, wanajua kwenye maendeleo kuna-*primitive way of wealth accumulation*, nchi hii huko nyuma watu walipiga dili niwaombe hebu kale kaofisi namba 43 pale Hazina, Dar es Salaam ambako kamekuwa-*connected* na TAKUKURU ambako wafanyabiashara wanapiga foleni mpaka leo kuhojiwa mambo ya mwaka 2008, 2009, 2010.

Nikuombe Rais Magufuli ni *man of decision* mpelekee, toeni *amnesty*, watu waliowahi kupiga *deal* jamani Mheshimiwa Mpango hawezi kufukuzwa hata siku moja kwa wizi hata siku moja / *can bet*. Lakini huko nyuma watu walipiga *deal*, na *deal*/ zote zillanzia Serikaliini, leo wanaosuffer ni wafanyabiashara, wanauzwa mali zao kulipa madeni ya miaka ya nyuma, tutawaumiza, wasameheni tangazeni *amnesty*, atakayeiba kuanzia leo mumshughulikie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono, ninachokiomba Serikali fanyeni *harmonization* mipango na bajeti havionani, ahsante. (*Makof*)

SPIKA:ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe. Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti asubuhi ya leo na mimi nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutupa nafasi ya kujadili bajeti ya nchi yetu katika mwaka wa fedha huu tunaoanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi naungana na waliotangulia kuipongeza Wizara kwa ujumla wake na Serikali kwa juhudni ambazo wameendelea kuzifanya katika kusaidia uchumi wa Taifa yetu. Lakini nianze kwa maneno machache ya wachangiaji wa asubuhi wanassema Serikali yetu, Rais wetu

amekosa washauri wazuri ndiyo maana uchumi wetu hauendi vizuri na maneno mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi kwamba katika muda wa miaka karibu miwili Bunge hili limekuwa likiishauri Serikali mambo mengi ya msingi na Serikali imeyasikia na imeyafanya kazi. Serikali hii ina wataalamu na washauri wazuri ndiyo maana leo tunajivunia gawio la Airtel kwa historia ya nchi yetu na kupata hisa hiyo ambayo Serikali imepata. Hao ndiyo washauri, Rais hafanyi kazi peke yake Serikali hii ndiyo ushauri wao ndiyo umesababisha sasa hivi Serikali inapokea gawio katika mashirika ya Serikali ambayo yalikuwa yakijiedhesha kwa hasara. Kwa nini tusitambue michango ya watumishi wetu wanaosaidia nchi.

Mheshimiwa Spika, Rais kazi yake ni kusimamia, lakini wako watumishi wetu wanaofanyakazi kumshauri Rais na mambo mengi yamefanyika kwa kipindi hiki ndiyo maana tunajenga reli ndiyo maana tumefufua Shirika la Ndege ambalo limekufa kwa zaidi ya miaka 20. Ukitsemakuna washauri wazuri nadhani hatuitendei haki nchi yetu ndiyo maana hata kodi ambazo tulikuwa tumezilalamikia zimefutwa na Serikali hii kwasababu ya ushauri wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini baya zaidi wako wanaohoji kwa nini Rais amekutana na watumishi sijui watu gani wafanyabiashara, Rais huyu ni Rais wa Watanzania wanyonge wa Taifa hili, anayo haki na wajibu wa kufanya alichokifanya na wote tumpongeze ni historia katika nchi Rais kuja kuongea na watu wachache na wa chini kabisa huyu Rais ni wa mfano ndiyo maana ye ye anachojali ni watu wake, amepigwiwa kura kama Wabunge hapa lazima akutane na wapiga kura wake wakati wote tumpongeze Rais ambaye ameona ikulu ni sehemu ya Watanzania na siyo sehemu yake peke yake, halafu watu mnakuja hapa mnahoji eti kwa nini Rais amekutana na wafanyabiashara, huyu ni Rais wa mfano, ni Rais wa wanyonge, ni Rais anayeeonesha kwa vitendo kwamba anajali maslahi ya Watanzania bila kujali hadhi yao ya kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hii lazima tujifunze kujifunza kwake ni Wabunge wangapi wanakutana hata na wapiga kura wakitongoji, Rais huyu amekutana na wafanyabiashara wa kila Wilaya historia hiyo, amekutana na Makatibu Tarafa historia hiyo na wafanyabiashara wa madini historia hiyo ndiyo Rais tunayemtafsiri kama Rais wa wanyonge wa Taifa hili tumpongeze, tumtie moyo na anafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme maeneo machache kushauri katika bajeti tunazungumza habari katika kitabu cha Waziri ukurasa wa 31; Waziri anasema hivi; katika kuendeleza azma ya kujenga uchumi wa viwanda katika mwaka 2019/2020 Serikali itajikita kuvutia uwekezaji zaidi kwenye viwanda viliviyotumia malighafi zinazopatikana nchini kama vile mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, misitu na madini.

Mheshimiwa Spika, nataka nimuulize Waziri kiasi gani mmetenga? Kwa sababu kuzungumza ni jambo moja na lakini kuwekeza katika maeneo hayo ni jambo lingine na Mheshimiwa Waziri lazima tujifunze kwamba Serikali haiwezi kuwapa wananchi mmoja mmoja fedha kwa ajili ya kujenga kilimo, kwa ajili ya kuwekeza katika mifugo, lakini lazima Serikali itengeneze miundombinu na mazingira wezeshi ili Watanzania wanaoweza kuwekeza wawekeze katika maeneo hayo. Ni kweli mnazungumza maneno ya kuwezesha kilimo lakini kiasi gani ambayo Serikali imetenga kwa ajili ya mazingira wezeshi katika sekta ya kilimo, katika mazao yale ya kibashara ikiwepo pamba na mazao mengine kama chai, kahawa na mengine kama hayo, kama hatuwekezi katika maeneo hayo hatuwezi kwenda.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nishauri Serikali katika eneo hili, moja ya tatizo kubwa linaloikabili sekta ya kilimo kwenye nchi yetu ni mambo makubwa matatu; moja upatikanaji wa mvua ya uhakika ambayo imekuwa shida, tunataka Serikali na Wizara ituambie tunafanya nini kuhakikisha kwamba maji tunayapoteza ukiwa unaenda Dar es Salaam wakati wa masika haipitiki barabara yetu kwa sababu ya mvua na maji mengi, Serikali ingefanya mchakato wa kukusanya yale maji ili kujenga bonde hilo ikawa ni zone

ya umwagiliaji na tukawa na kilimo chenye tija kwa ajili ya maslahi ya Watanzania kuliko kupoteza haya maji bure mengi ambayo kwa kweli wakati mwingine yanatuletea maafa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine upatikanaji wa pembejeo kwenye nchi yetu imekuwa donda sugu. Naomba Serikali na hili katika hili Bunge tukubaliane tunataka Serikali wakati wa majumuisho mtuambie mnafanya nini kuhakikisha pembejeo za hakika zinapatikana kwa wakulima. Kila mwaka tunaletewa pembejeo *fake* lakini Serikali haiwachukulii hatua wale wanaotusababishia pembejeo hizo na Serikali imeondoaruzuku katika pembejeo tunapata wapi pembejeo ili wakulima walime kwa haki na kwa ustawi wa Taifa hili. Serikali haiwezi kulima lakini itutengenezee mazingira rafiki ili tuweze kulima kwa tija, wakulima hawajui wanapata wapi pembejeo, Serikali mnafahamu nini mikakati ya kwenu kuhakikisha kwamba pembejeo tunazipata kwa gharama zetu wenyewe wakulima siyo kwa gharama zenu, lakini hatuzipati. Kila mwaka mnasema mnawashughulikia waliotuletea *fake* halafu mwaka huo nani anatufidia sisi wakulima kwamba tumepata hasara na Serikali hiyo ambayo wako kule chini wanaosimamia hizo pembejeo kwanini hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho mimi naomba kwa niaba ya wafugaji wa nchi hii tumeona tozo nydingi mmefuta tunawapongeza sana, lakini tozo mlizofuta ni za wafanyabiashara wa viwandani, sisi wafugaji wa chini tunatozo mnayotutoza kila ng'ombe shilingi 30,000 tunavyopeleka ng'ombe Kenya au kutoa nje ya nchi na huku hakuna masoko, mtuhurumie katika eneo hilo tumehangai na Wizara sasa tumeleta kilimo chetu Mheshimiwa Waziri wa Fedha msipotusikiliza tutaenda kwa Rais na Rais atafuta hiyo tozo. Kwa nini m-*charge* mfugaji wa kawaida ng'ombe zake anaenda kuuza Kenya mnawambia kila ng'ombe aliye shilingi 30,000 huyo ng'ombe tumefuga pamoja? Huyo ng'ombe tumelisha pamoja? Hapana tunagawanaje faida shilingi 30,000 ni mgao gani nchi hii ambao mna-*charge* shilingi 30,000 ng'ombe peke yake 30,000 kichwa cha

ng'ombe mmoja kupeleka Kenya hii si sawa mtuondolee tozo hiyo tugawane nusu mchukue 15,000.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani shilingi 30,000 kila ng'ombe mmoja kupeleka Kenya unalipa shilingi 30,000 kwa nini? Mbona hamna utaratibu halafu huku kwenye Halmashauri unalipia shilingi 2,700, umelipia sijui shilingi 5,000 nyingi ya kutosha hii tozo naomba Serikali ipunguze bei. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Monduli. Mheshimiwa Sixtus Mapunda atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii. Nchi yetu bado ni Taifa changa linalo-*struggle* sana kwa wananchi wake kuwa na uhakika wa kupata chakula, kuwa na uhakika wa kupata sehemu ya kulala na vilevile wanahangaikia sehemu ya kujihifadhi katika maana ya nguo na mambo mengine elimu na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hali ya namna hiyo, ni ngumu sana mtu unapoyahitaji yote kwa wakati mmoja kwa aina ya uchumi wetu ukayapata yote kwa wakati mmoja na kutokana na hali hiyo hiyo mahitaji yote unayataka kwa wakati mmoja, vilevile ni ngumu kukiacha kimoja ndiyo maana naungana sana na Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa jitihada zake za kwenda na miradi mikubwa wakati huo huo ikirekebisha mambo madogo. Haya mambo yote ndani ya nchi yetu siyo mapya yana mifano, wote mtakumbuka tuliposema tuwe na shule za sekondari kwa kila kata na wengine hapa mtakuwa mashahidi watu humu ndani waliwahi kusema ni vema tukaanza kutengeneza walimu, halafu baadaye tukajenga shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kutokana na hali jinsi ilivyo hatuwezi tukasubiri watu kuzaliana watoto wakakua wasubiri kwanza mwalimu atakayepatikana kwa muda wa miaka saba, badala ya kujenga boma moja utakalolimaliza baada

ya miezi mitatu. *The same here*, leo tunaongelea kuhusu viwanda mwingine anasema hapana tusijenge kiwanda twende kwanza tuka-produce, tukishazalisha kivilango cha hali ya juu sasa twende kwenye viwanda hili linakuwa ni kosa la pili linafanana vilevile leo unataka kujenga shule kipindi huna mwalimu, ukizalisha sana kabla hujaenda kwenye viwanda *crisis* yake itakuwa ni kubwa zaidi ni vema ukaanza kiwanda ukakikuza kiwanda kulingana na mahitaji yake kuliko ukaenda kwenye kuzalisha sana bila kiwanda yale malighafi utapeleka wapi? Ndiyo kwa maana nikasema nchi yetu ni nchi changa, inahitaji yote kwa wakati mmoja na yote lazima yaende hatuna njia ya mkato, kila utakalolichagua halitakuwa sahihi zaidi kuliko lingine. Ukitsema leo uwekeze kwenye kilimo huwezi ukaacha afya, ukisema leo uwekeze kwenye afya hutaacha elimu. Kwa nchi yetu jinsi ilivyo hakuna namna, kweli kupanga ni kuchagua *we don't have choice, we must choose all of them.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba niseme kidogo kwa mambo ambayo yameongelewa kwa muda wa miaka hii mitatu/minne kwa mfululizo miradi mikubwa sana mradi wa reli ya Mtwara, Liganga na Mchuchuma katika upande wa chuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapoenda kwenye maendeleo makubwa ya viwanda na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nitakuomba sana ultizame hili kama nilivyosema awali kupanga ni kuchagua mjadala wa Liganga na Mchuchuma umekuwa mrefu mno, tunaanza sasa hivi reli ya kati ya kisasa Liganga na Mchuchuma imejadiliwa miaka na miaka kwa nini tusimalize hilo? Lakini jambo la pili, siyo kila kitu lazima tukifanye wenyewe. Reli ya Mtwara itakwenda kuunganisha Liganga na Mchuchuma, itapita mpaka kwangu pale Mbanga, itakwenda mpaka Mbamba bay kwa nini tusianze kwa *PPP* kwa *theory* ile ile bila kuogopa miradi mikubwa kwenda nayo pamoja, kupanga ni kuchagua lakini hatuna *choice* lazima tuyachague yote kwa wakati mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hili naomba niliseme kwa utulivu kidogo; Mungu alipotuumba wanadamu, kwanza

zile siku zake tano za mwanzo akasema na liwe juu na uwe mwanga, ardhi na mimea vyote vikawepo. Ilipofika siku ya sita akasema na tufanye mtu kwa sura na mfano wetu. Baada tu ya kumuumba na kumwambia zaeni mkaongezeke akamwambia ukavitawale viumbe vyote vya ardhini na ndege wote wa angani; maana yake nini kila kitu kilicho juu ya sura ya ardhi ya Tanzania lazima kitawaliwe bila masharti yoyote kwa sababu tu kinatija kwa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, leo hii mnaongelea mambo ya umeme, reli ya kati mnasema mto Rufiji, *Stiegler's Gorge*, nakupa hoja nyngi za kubeza mimi niseme kitu kimoja, moja ya biblia imesema tutawale, tuweke umeme kwa njia zozote zile lakini kwa hoja ya pili ni hoja ya kisayansi watu wamesema sijui maji, yataisha, sijui nini kitatokea, kuna kitu kimoja kwenye sayansi na wanasayansi wa *anatomywatanisaidia*. Ukitosha *Introduction to anatomy inakuambia sensitivity, irritability na adaptation*; kila kiumbe duniani ameumbwa kwa ajili ya kukabiliana na mazingira. Ukiiona jambo linakusaidia leo kwa ajili ya kupiga hatua moja hata kama ina *negative effect* akili yako mwanadamu umeumbwa kukabiliana na mapungufu yanayotokana na maamuzi yako.

Mheshimiwa Spika, tukienda leo pale kuweka ule mradi kuna watu wanasema kuna baadhi sijui ya swala hawanywi maji wanakula ule mvuke unaotokana na maporomoko tutapoteza utalii, si kweli; kama binadamu anayekuwa kwenye baridi akitoka kule Mbeya anakuwa na vinyoleo akifika Dar es Salaam miezi miwili vinyoleo vinapuputika kwa ajili ya joto. Huyu swala atashindwa ku-*adapt nature?*

Jamani tusiogope kutoa maamuzi kwa ajili ya *nature*, Mwenyezi Mungu katuumba na hizi rasilimali tuzitumie, tukiziacha zitakuja kuwa laana kwetu, hatuwezi leo kwenda kulipa gharama kubwa sana ya umeme kwenye majenereta miaka nenda miaka rudi umeme wa maji uko pale hata kama utakuja kuchukua kinu cha kwanza kitaoa umeme mwaka 2029 *is betterku-make decision* leo. Ukiacha kutoa maamuzi leo, kesho aje atoe nani? Waliotengeneza reli ya kati

walikuwa wanajua tutahitaji namna hii wali-*make decision*, we must make decision hata kama hata maamuzi yanatumiza sana lazima tuyafanye. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini moja la mwisho niseme kuhusu Watanzania. Watanzania inabidi si neno zuri sana kulisema lakini inabidi niliseme inabidi kidogo tuangalie akili zetu zikoje, kuna muda hatujui tunachokotaka, ukiambiwa reli isipokuwepo matatizo, ikiwepo mbona miradi yote mikubwa inaenda kwa wakati mmoja. Ndege isipokuwepo matatizo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, ukilleta...

SPIKA: Mheshimiwa Sixtus malizia.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa maneno mawili ya mwisho; Watanzania tujifunze kujua tunachokotaka lakini la pili ni afadhali tuwe na uwezo na udhubutu wa kutoa maamuzi yenye tija hata kama yatakuwa na hitilafu gari lilloanza safari ni rahisi kulirekebisha kuliko ambalo halijaanza kufanya safari. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mapunda, nilikwisha mtaja Mheshimiwa Ahmed Shabiby atafuatiwa na Mheshiimiwa Japhary Michael.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji. Kwanza niunge hoja mkono na niishukuru Wizara hii na niwashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wote wanaohusika kwenye Wizara hii. Labda na mimi sana sana ni kutoa ushauri na ushauri wangu utajikita

katika sehemu za biashara hasa katika wafanyabiashara wa kati na wa chini na hii katika ushauri tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nitaanza na mashine za *EFD* kwa sababu tupo kwenye Wizara hii ya Bajeti na Fedha. Hizi mashine za *EFD* lazima zitafutiwe mikakati katika hawa wafanyabiashara wadogo na hata wale wakubwa ambao wanatumia mashine za *EFD*. Mashine za *EFD* sasa zimekuwa kero sasa sijafahamu ni makampuni yaliyopewa hii *tenderza ku-supply* kwa sababu utakuta mtu ana duka dogo lakini ile mashine kila siku ni mbovu na sasa imekuwa ni mataji kwa wale watu wenye mashine, utakuta sasa unatakiwa ubadilishe mashine leta hela nyingine, uiboreshe lete pesa nyingine. Sasa hii imekuwa tatizo kwa wafanyabiashara kwa hiyo zingaliwe upya. Hawa-*supply* au *model* ya hizi mashine zinazotumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kwenye biashara ya *transportation* na hasa malori, mimi sina malori. Lakini nafikiri uchunguzi haujafanyika kwa kina kwamba sasa hivi tunazidi kupoteza Watanzania wote ambao wanafanyabishara ya *transportation* ya malori. Mheshimiwa Rais pamoja na sisi Wabunge tulijitahidi sana wakati ule wa *VAT* na ile *single customer* ili bandari yetu ifanye kazi, lakini sasa hivi bandari yetu inafanya vizuri sana, *custom*pale wanafanya vizuri sana, lakini *transportation* yote wanafaidika watu wa nje Burundi, Zambia na Rwanda.

Mheshimiwa Spika, watu hawalifahamu lakini sasa hivi magari yote ya Watanzania yanasa jiliwa Zambia, Rwanda Burundi na Uganda. Ukitaka kufanya uchunguzi huo kaa barabarani zikipita gari za *transit* nne; tatu au mbili zina namba ya Rwanda, Burundi au Uganda au Zambia na kwa ushahidi zipo gari zinakuja mpya gari 100/gari 50 zinaenda Zambia zinasajiliwa lakini za Watanzania zinakuwa namba ya kule, kwa hiyo, kodi yote inalipiwa nchi za nje. Na ukitaka kujua kwa akili nyepesi ukiangalia gari za Rwanda, Rwanda wanatumia *left hand drive* utaona gari ina *right hand drive* unajua hii gari ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo gari zote za *transit* sasa hivi zinahamia nchi jirani, tatizo ni nini? Lazima hapa tujiulize hapa kuna shida gani. Nilikuwa naomba watu wa *TRA* hasa ndugu yangu aliyepewaa ukamishna sasa hivi kwa sababu najua ni msikivu, ajaribu kukaa na hawa wafanyabiashara angalie kuna shida gani hadi watu sasa wanahama kupeleka kodi kwenye nchi zingine na nilikuwa nashauri sehemu kama hii ni lazima waweke *limit* kwa mfano kama *income tax*, najua ukiweka kwenye mambo ya *transportation* iwe mabasi iwe malori kwamba kodi yetu tukipiga mahesabu kwa jumla ya *transportation* zote zilizopo Tanzania idadi ya magari labda tunapata kiasi fulani, lakini tuwekea *limit* kila gari iwe inalipa kiasi hiki najua kabisa mtapata zaidi ya mara kumi ya kodi ya sasa hivi. Kwa sababu wafanyabiashara watanzania ukitaka wafanye hesabu saa nyingine hata tunalaumu *TRA*, lakini wafanya mahesabu wenyewe wa Tanzania nao ni *fake*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukawa mfanyabiashara unafanyiwa mahesabu unampekea *consultant* wa mahesabu anakufanya mahesabu anaonesha unadaiwa wewe sasa *TRA* atafanya nini? Wakati huo unayemuamini kwenye mahesabu yeye ndio aliyekufanya mahesabu anaonesha unadaiwa wewe sasa *TRA* atakwambia hudaiwi? Kwa hiyo, lazima tuangalie hizi biashara watu wanazozifanya wengi ni watu wa kawaida na watu wa kat. Kwa hiyo, lazima tuangalie namna gani yakuwasaidia na namna gani Serikali itakusanya kodi yake bila kupunguza kodi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitakuja kwenye *EFD* za kwenye mafuta, hizi ni wizi mtupu kwenye *petrol station* na wewe nafikiri ni sahidi kwa sababu unafanya hii biashara, hizi ni za wizi na ninajua kabisa Dkt. Mpango, Ndugu Kichere...

MHE. RICHARD M. NDASSA: Kichere hayupo.

MHE. AHMED M. SHABIBY: ... Ndugu Kidata na wote walikuja hawakushiriki katika mchakato wa kuleta hizi *EFD* walikuta ule mchakato upo, hatuwezi kuwalauku hao watu.

Mheshimiwa Spika, lakini unanunua lile dubwasha kwa dola 3,000 mpaka 5,000; unalifunga kwenye *petrol station* kwa mwaka unalipa shilingi 1,200,000 kwa ajili ya yule fundi. Halafu mkoaa mzima kuna fundi mmoja, halafu ikiharibika unatoa ripoti *TRA* kwamba mashine imeharibika, unaendelea kuuza, ile mashine haifanyi kazi, kesho na kesho kutwa anakuja fundi anakwambia kadi imekufa, anachukua shilingi 300,000 kwenye kila *pump*, yale makaratasi yanayotumika pale ni ya mamilioni kila siku halafu haina faida yoyote kwa sababu *EWURA* wanatoa bei, tuna chombo cha Serikali kinaitwa *EWURA* kinajua kabisa mfanyabiashara wa rejareja kwenye kila lita anapata kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mtu anaendesha Kituo cha Engen au Total au Oryx au Gapco au nani anajulikana kabisa kwa lita anapata shilingi 72. Huyo mwendeshaji wa kituo na mafuta yote yanatoka *depot*. Kwa nini msichukue huko mkate kwenye ile *profit* ya huyo muuzaji kwa nini msikate pesa yenu huko? Mkatie huko Dar es Salaam kama hii ni shilingi 72 tunachukua tunakata shilingi 15 kwa lita, kusanyeni huko. Kwa sababu mnapotaka kukusanya mafuta yakuja kwa muuzaji wa *retail*, sasa hivi Wilaya zote kuna boda boda na kuna nini na kuna watu wanauzu kwenye mapipa na wanashindwa kudhibitiwa, mtu wanamshushia kutoka kwenye tenki la gari, ana mapipa yake 20 chumba cha 4,500 yanaenda moja kwa moja kwenye mapipa.

Mheshimiwa Spika, mtu ana malori yake, anashusha gereji, haipitii kwenye *petrol station*, sasa hiyo *EFD* inafanya nini? Kwa sababu mtu anaamua kuiba anavyotaka yeye, sasa hiyo *EFD* inafanya nini? Leo mimi nina mabasi, naamua kushusha gereji kwangu na *EFD* gereji? Kwa hiyo nimechukua mafuta lakini hayakupita kwenye *EFD* nataka kumuuzia mtu anaenda kuuza kwenye mapipa natoa kwenye gari *direct* moja kwa moja mpaka kwenye mapipa, kuna *EFD*?Napeleka shambani kuna *EFD*?Kwa hiyo kateni huko angalieni kwamba katika vituo vyote tunapata milioni ngapi na tukikata hapa huku basi hatupotezi wala hatupunguzi yale mapato tunayopata.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukilichukua hilo utapata hela nyingi sana, hizi *EFD machine* yaani ni kupoteza muda tu kabisa kabisa. Endelea Mheshimiwa Shabiby. (*Makofi*)

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ndio cha msingi.

SPIKA: Kata kule kule Dar es Salaam upate hela yako.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, juzi nimekwenda Kiteto unakuta fundi anaambiwa amemuita fundi ana wiki tatu hajafika kutengeneza mashine za *EFD* wakati kuna njia rahisi kabisa za kukusanya mapato. Halafu sisi tunawashauri na tunasikia kwa wafanyabiashara wenzetu ili Serikali ipate fedha, basi tunaomba muwe wasikivu hata kwenye haya magari wangeamua tunasema labda kila gani fulani linakwenda *transit* tunachukua kodi yetu milioni mbili au tatu kwa mwaka wewe shauri yako.

Mheshimiwa Spika, sasa utakuta mtu akiwa ana gari nne hafanyi hesabu, analipa labda milioni moja, mwenye gari tano kwenda mbele anafanya hesabu analipa milioni tatu. Mtu akifikia uwezo wa kununua gari huyo ana uwezo wa kulipa kodi. Kuna haja gani ya kumwambia asifanye hesabu au kama mtu anafanya hesabu afanye lakini pawe na bei inayoleweka kwamba gari hii mtaondoa hata vyanzo vingine sababu ya kutoa rushwa si kukamata. Hata uweke wakamataji wawe wa wangapi utakamata wote? Sababu ya utoa rushwa ni kutoa vyanzo nya rushwa, kwamba nini kinasababisha hapa ndio unatoa rushwa. Kwamba hiki kinasabaisha rushwa tukiweke mazingira kitakuwa hakina rushwa, hiki kina sababisha kero hii tukiondoa kitakuwa hakina kero, lakini tusitegemee TAKUKURU, TAKUKURU atakamata watu wangapi? Hii kitu haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya kuna ile watu hapa mwaka jana ilifutwa ilikuwa milioni tatu sijawahi kufanya hiyo. Wala kwa mimi siipendi kuweka jina langu kwenye gari, lakini kuna watu wanapenda kuweka majina kwenye magari, unakuta

mtu anaandika *King Musukuma*, nitolee mfano Musukuma gari yake imeandikwa *King Musukuma* alikuwa nalipa shilingi milioni tatu lakini wakaja wakapandisha, sasa mwingine haweki lile jina la kwenye *plate* namba kwa sababu labda ni starehe. Mwingine ana kama akina dada hapa Wabunge na wadada wengine walioko mtaani gari zao wanazitumia vizuri ana TZB hataki hiyo gari ionekane ni TZB anaamua kuandika jina lake pale ili afute ile namba gari isijulikane kama ni gari zamani au gari mpya. Kwa sababu gari yake bado ni nzuri. Wewe unaenda unaweka kodi kubwa, sasa hata nikiangalia sasa hivi kama mapato yapo pale pale lakini waliosajili ni wachache, eeh, tuweke bei ndogo watu wawe wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna yale bango yalikuwa kwenye malori hatuna sisi viwanda, lakini mabango ya kwenye viwanda hata sasa hivi ukiangalia unasema malori ya bakiresa yako wapi mbona hayapo, malori ya fulani yapo wapi mbona hayapo, sio kwamba hayapo yale mabango yalikuwekewa sijui milioni nne kwa mwaka ukiandika kwenye lori tu kwamba hii bidhaa fulani inauzwa unalipia milioni nne/ milioni ngapi sasa mwishowe watu wameamua kufuta tu wamebakiza magori mawili/matatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, weka pesa kidogo upate mapato mengi. Kuna hii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Nimekuongeze dakika kidogo endelea Mheshimiwa Shabiby. (*Makofi*)

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa hiyo, utakuta tunachotakiwa sisi kufanya tusizungumze sawa tunasema kwamba kuna biashara zimefungwa labda 1,000 zimefunguliwa biashara 14,000. Lakini biashara zilizofunguliwa 14,000 na zilizofungwa zipo sawa? Inawezekana biashara wamefungua 14,000, 12,000 lakini

biashara za *briefcase*, mtu akenda *BRELA* kasajili, kaenda *TRA* kachukua *clearance*, kaenda Halmashauri kachukua leseni, kafungua biashara, lakini hata duka lenyewe hana. Ukiangalia biashara zinazofungwa na zinazofunguliwa na kero nyingine hajatajwa kwenye bajeti hii watu tumeng'ang'ania kero za *TRA*, lakini kuna watu wengine wana kero kuliko hiyo *TRA*.

TAARIFA

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante naomba nimpe taarifa mzungumzaji Mbunge Mheshimiwa Shabiby kwamba anasema kwamba biashara za kuandika bango na hii imepoteza hela nyingi sana katika nchi yetu kwa mfano mtu ana *salon* yake akiandika bango ama hoteli wanam-*charge* hela nyingi, matokeo yake watu wanafuta. Kwa hiyo biashara nyingi hata sasa hata hoteli, maduka, *salon* wote wameondoa mabango kwa hiyo *TRA* wanapoteza hela nyingi sana. Bora wapunguze bei ili hawa watu waendelee kuweka bango katika biashara zao. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Shabiby ilikuwa ni taarifa kwako tu.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu ni taarifa ya kujenga na tupo pamoja. (*Makofi*)

Kwa hiyo sisi tunaishauri *TRA* na nina uhakika kabisa hata watu wanapoizungumzia habari ya *TRA* lazima tuseme ukweli. Ukiangalia huko juu kwa Makamishna huko hakuna matatizo kabisa, huku chini na ndio maana Rais alisema. Hapa Dodoma mlikuwa mnashuhudia wenyewe mtu anakwenda anafunga duka anasema hapa kazi tu. Kumbe ana roho mbaya, huyo anakuwa ana roho mbaya na Rais Magufuli tu wala hana kitu kingine, hapa kazi tu tumetumwa, wanasesma.

Mheshimiwa Spika, Iakini sasa hivi bahati nzuri tunashukuru kuna Meneja wa *TRA* amekuja mpya hapa Dodoma ameondoa hilo tatizo, kwa hiyo, mimi ushauri wangu ni huo. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Tunakushuru sana sana, Mheshimiwa Shabiby anatoa usoefu ndani ya biashara *practical*, sio ile ya kwenda *library* halafu unapitia pitia unatuletea *theoryza* chuo hapa. Ahsante sana, Mheshimiwa Japhary Michael nilishakutaja tafadhalii. (*Kicheko*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2019/2020. Mchango wangu kwa Serikali ni kwamba tuna kipindi cha miaka minne tangu tumepewa dhamana kwa upande wa Chama cha Mapinduzi kuongoza nchi hii, nilitaka kupata tafakari ya Serikali kwamba je, kwa miaka minne hiki walicho-*achieve* ndiyo walikuwa matarajio ya Watanzania? Na ninajaribu kutafakarisha Serikali kwa sababu naamini mwaka 2015 wakati wa kampeni za kuogombea kila upande ulikuwa na *movement zake for change*. CHADEMA walikuwa na *movement for change* na upande wa CCM walikuwa na *Magufuli for change*. Maana yake nikwamba wananchi walikuwa na matumaini makubwa sana ya mabadiliko makubwa ya maisha yao katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa nilifikiri kwamba labda Serikali itafakari baada ya miaka minne yale matatizo ya wananchi yametatuliwa na yametatuliwa kwa kiwango gani? Nadhani tungetafakari hili kwa undani tungejipima vizuri zaidi. Hapa tunabishana kati ya maendeleo ya watu na maendeleo ya vitu ambayo kwa ujumla yote ni muhimu katika nchi yetu. Lakini wananchi walipokuwa wanakimbizana na sisi barabara zilikuwa hazijengwi? Wananchi walipokuwa wanakimbizana na sisi reli zilikuwa hazijengwi? Ndege zilikuwa hazipo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa haya maswali tukitafakari tutajua hitaji kubwa la wananchi katika nchi hii ilikuwa kuondokana na umaskini walionao. Je, katika miaka yetu minne tumeweza kuondoa umaskini Watanzania walio nao? Hayo ndio nafikiri maswali ya msingi ya kuuliza. Hivi sisi tunataka tushukudie nini?

Mheshimiwa Spika, nadhani sisi Watanzania hasa Chama cha Mapinduzi tunakuwa wagumu kuamini kuliko hata tomaso alivyokuwa ameaminu ufufuko wa Yesu. Kwa nini kwa sababu Watanzania wote tulipo hapa tunafahamu kabisa ndugu zetu ni maskini, wana maisha ya dhiki, wana matatizo, wote Wabunge hapa tulipo hapa ndani tunajua kwamba tuna matatizo makubwa ya *dependence* ya watu wetu, kwa sababu hawana uwezo na tuna uhakika kwamba *dependence* imeongezeka halafu tunaambia uchumi unakuwa kwa 7% kwa hiyo *articulate* hali yetu ya maisha ya Watanzania na tunapongezana kabisa yaani mnapongezana *as if your doing so well*, hamtaki kukubali kwamba Taifa limerudi nyuma mno maisha ya watanzania yamezidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, lazima tujipime kwamba hivi mwaka 2015 maisha ya Watanzania yalivyokuwa ya huko kijiji na miaka minne sasa maisha yalivyo. Hivi mazuri yakikuwa wakati gani yalikuwa mazuri kipindi hicho au kipindi hiki? Ndicho kipimo cha maendeleo ya wananchi. Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidia ni mtu mwenye weledi mkubwa sana na ni mbobezi wa masuala ya uchumi anisaidie na Naibu wake Waziri nawaamini kabisa kwa uwezo wao, sina mashaka nao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, labda waniambie ni kwa nini wamechagua mtazamo wa uchumi uliofungika kwa maana ya *contractionary economic policy and in ward looking policy* kuliko kuangalia *expansionary policy* uchumi unaoangalia nje zaidi. Tafakuri yangu inaniambia tunapotazama uchumi wa ndani tukaangalia kodi zetu za ndani na mapato mengine yasiyo ya kodi ya ndani kama chanzo cha ku-*finance* miradi ya maendeleo tunazidi

kuumiza watu wetu. Tunaweza tukawa na mawazo bora sana ya kusaidia miradi mikubwa ya nchi hii, ya kusaidia maendeleo ya nchi hii lakini tukaosa *approach* bora ya kui-finance miradi hiyo hayo ndio mawazo nafikiri hayo ndio mawazo ya Kambi ya Upinzani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani hajjawahi kufikiri kwamba kuna ubaya wa kujenga reli, Kambi ya Upinzani hajjawahi kufikiri kama kuna ubaya wa kuwekeza kwenye ndege, Kambi ya Upinzani hajjawahi kufikiri kwamba kuna ubaya wa kuwekeza kwenye miundombinu yoyote ile. Lakini tunadhani tunachofautiana Mheshimiwa Waziri katika *approach* ni namna gani tu-finance hii mipango ili wananchi wetu wa chini wasiteseke. Sasa *problem* tuliyonayo ni kwamba tunabishana hapa tu kwamba labda kuna watu wanaopinga haya mambo, *which is not true*. Wote tunakubali kwamba lazima wananchi waendeleee, lakini *approach* zetu zikoje katika suala la mtazamo ya kiuchumi, sasa nyie ni wabobezi wakubwa mliopewa dhamana hii kubwa, ni vizuri Mheshimiwa Waziri na mimi ungeniambia ni kwa nini *ume-opt* kwenye mawazo ya uchumi uliofungika ya kubana uchumi zaidi kuliko kufungua uchumi, nadhani *unge-opt* kwenye *approach* ya kufungua uchumi leo hotuba yako Mheshimiwa Waziri ingekuwa inaonesha namna gani uta-attract FDI - *Foreign Direct Investment* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ingeonyesha hivi kama solution, labda hotuba leo ingeonesha namna gani uta-incorporate PPP - *Public Private Partnership* ambayo ingeweza kusaidia, lakini kwenye mpango wenu mnaonekana sana kwamba mna-discourage PPP, mna-discourage uwekezaji kutoka nje. Mnaamini kwamba through hizi Kodi ambazo mnaumiza wafanyabiashara, mnaumiza wafanyakazi zinaweza zikawasaidia kwenda mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi naamini kwa Kambi ya Upinzani hatuamini kwamba mko kwenye mtazamo sahihi, ndio ninachofikiri hicho na kimsingi hapa ndipo tunapopata tatizo hapa, kigugumizi kwa sababu watu hasa tunabishana, hivi wananchi wanapata maendeleo ama ni wanataka vitu?

Wananchi wanataka vitu maendeleo ya vitu, lakini wanachotaka maendeleo yao pia. Hawataki vitu tu, wanataka wapate uhakika wa huduma za afya, wanataka wapate uhakika wa huduma za maji, wanataka uhakika wa kipato cha kulisha familia zao, wanataka wapate uhakika kucomesha watoto wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hamuwezi kusema mme-*achieve economically while people are suffering*, na mnakusanya Kodi mnazitumia kwa *expense* ya maisha ya Watanzania kwa *sacrifice* ya maisha ya Watanzania, haiwezekani, kwa hiyo ni lazima Mheshimiwa Waziri kwa uwezo wako na kwa ubobezi wenu mtazame hili kwa upana wake, na hili nafikiri siyo jambo la kubishana sana ni jambo la kutazama namna gani tunahakikisha miradi ya maendeleo inafanyika lakini namna gani tunahakikisha kwamba watu wetu wanapata huduma wanazostahilli na vipato vyao vinakuwa, ili na wananchi nao wa-*feel*/huu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unapowekeza kwenye *standard gauge* unafanya jambo jema, lakini mradi utakapo toa matokea baadaye sana je kwa sasa hivi Mwananchi huyu wa Tanzania aendelee, amefunga mikanda *for fifty years*, hajapata mabadiliko, amepata matumaini kwamba baada ya kuingia Serikali hii atapata mabadiliko, ataongeza kipato chake, *as we are talking* leo mfanyakazi hajaongezewa mshahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia leo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, watu wanapunguzwa kazi, tunapozungumzia leo biashara zinafungwa, ninapozungumzia leo matatizo ni mengi makubwa katika nchi hii, lakini sisi tukikaa hapa kwenye Bunge hili tunapongezana kwamba tunafanya vizuri katika

uchumi huu, tunahitaji *philosophy* za kitaalam sana tuchanganyane huku ndani, lakini wananchi... (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, *philosophy*, kwa hiyo ninadhani ni wakati wa kutafakari...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Eti! Ni ya pili tayari.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, ya kwanza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: No, alianza na dakika 35.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, ya kwanza.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Tayari ni dakika kumi. (*Makofi*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, Ya kwanza.

SPIKA: Wala hujaonewa kabisa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, nimeonewa kwa kweli.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Tayari, tayari dakika kumi.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Serukamba. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Bajeti ya Serikali, kwanza naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Waziri wa Fedha kwa *speech* nzuri sana, lakini pia nimpongeze kwa kusikia kilio cha Wabunge toka tumeanza kuondoa tozo zote, tozo 54. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Waziri wa Fedha kwa mara ya kwanza tumekuja tunafanya bajeti, siyo bajeti ya pombe, siyo bajeti ya sigara, hongera sana ndugu yangu, lakini la pili niipongeze Serikali kwa barabara ya Kigoma - Nyakanazi; naishukuru sana Serikali kwa kutukumbuka watu wa Kigoma, nadhani umefika wakati sasa tuhangaike na barabara ya Mwandiga, Chankere, kwenda Kagunga kwa sababu tutapitia pale gombe ambayo itasaidia sana kwa maana ya utalii nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nimesoma vitabu vyote hivi vya bajeti, nimesoma Mpango wa Taifa kuna maeneo mimi nadhani ningeomba Serikali tuyawekee mkazo unaostahili, tukiyawekea mkazo unaostahili tutapata fedha nyingi sana na mimi leo nataka nijikite kwenye *growth* na *production*. Nadhani umefika wakati Serikali tuhangaike na *growth* na *production* kwenye kilimo nimeingia Bungeni hapa huu

mwaka Mungu akinijaalia mwaka kesho utakuwa mwaka wa kumi na tano, haiwezekani kila mwaka nimechukua mazao machache, kila mwaka uzalishaji wa kahawa, hauzidi tani 50,000; uzalishaji wa chai, tani 19,000; pamba haizidi tani 300,000; mkonge haizidi tani 36,000 na korosho haizidi tani 210,000. Nimeamua kuchukua haya machache. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani Waziri wa Fedha umefika wakati ukae na Waziri wa Kilimo tupeane utaratibu kwamba ili tumpime Waziri wa Kilimo mwaka kesho tunataka aongeze tani za kilimo akishindwa then tujue wewe hutufanyii kazi yetu, sasa yeye ndiyo aseme hili niweze kuzalisha tani hizo nyingi ninahitaji uwekezaji huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naona suala la *growth* hatuhangaiki nalo, siyo sawa, maana hata hii kodi tunayotafuta kama hakuna *growth*, hakuna *production* ni kwamba tutaendelea kushikana mashati tu, wenzetu wanafaidi kwa sababu ya *economies of scale* kwamba hata bei ya dunia ikianguka kwa sababu umezalisha sana bado hutopata taabu.

Suala la pili ni suala la samaki, ukisikiliza hapa ni suala la Waziri wa Uvuvi anahangaika na wavuvi kuchoma nyavu, kukimbizana nao, toka tunaingia ndio kazi tunafanya, lakini leo wenzetu Kenya na Uganda wameanza namna mpya ya kufanya uvuvi, wanafanya vizimba. Maana yake ni nini kwa kufanya vizimba Uganda wamekwenda wamechukua wataalamu Kenya wamewapeleka Uganda kufundisha namna ya kutengeneza vifaranga na kuvigawa bure kama Serikali Kinachotokea leo Uganda na Kenya wataanza *export* samaki kuliko sisi hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sisi tuna Tanganyika, tuna *Lake Victoria*, tuna Nyasa kwa kweli kutohangai na hili hatuhangaiki kuondoa umaskini wa watu, tukihangaika na suala la vizimba (*cage*) wanasesma *fishing caging fishing* ninayo hakika kama Tanzania tutaongeza fedha nyingi za kigeni kwa *ku-export* samaki, lakini angalia nguvu zetu zinaenda wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwenye kuchoma nyavu, kwenye kukamata watu na vipuri vyao, kukamata watu na mashine zao, huko ndiyo nguvu tumepeleka, huko ambako tungepeleka tupate pesa wala hatuendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanya vizimba niwaambie kitakachotokea uvuvi ndani ya maziwa yetu kwa maana ya samaki wataendelea kuwapo kwa sababu ukishakuwa na *cage* unalisha pale moja kwa moja vinaanguka chini na samaki wengine kule chini wanakua, haya hatufanyi. Kupata kibali cha kuanzisha caging ni shughuli kubwa sana sasa mimi sielewi tunafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la utalii, hivi leo tuulizane Waheshimiwa Wabunge na hii naisema kwa nia njema kabisa, ukiindoa Zanzibar fikiria tungekuwa hatuna Muungano huu, maana yake tungekuwa hatuna utalli wa bahari, *beaches* Tanzania hazipo, lakini *we have the longest beach* kuanzia Tanga mpaka Mtwara tunafanya nini? *Beach zipo* Mungu ametuumba nazo lakini *we do nothing*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, so nadhani umefika wakati watu wa Wizara hii waje na mkakati wa kufanya tuwe na *beach hotels*, tuwe na *beach tourism* Mungu ametupa, hajatupa kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Spika, kutotumia ni dhambi na mimi nataka leo ni-suggest Serikali tuna mbuga nyangi sana Spika wewe hili unalijua sana, mimi nataka niishauri Serikali tuamue kwamba Ngorongoro na Serengeti ukitaka kwenda kule tuweke kwa watu wenye fedha, tuseme ukiingia kule ni dola 1,000, dola 2,000; tutapata pesa tutashangaana hapa, wale ambaeo hawana uwezo, hawana fedha iko Mikumi, Selous, Tarangire, iko wapi waende huko, kwa sababu wanyama watawaona, iko Katavi, Ruaha waende huko, lakini ukitaka kwenda Serengeti, Ngorongoro tuseme ni *for high and kitakachotokea* na mimi nasema hii imetokea Rwanda. Rwanda hawana vitu vyaa maana, wana nini, wana *chimpanzee* peke yake, walianzisha dola 750 kwa ajili ya kwenda kuona, ikawa *over subscribe*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kagame amekwenda Marekani kakutana na watu pale *seekerville* wakamwambia unaweza hela ndogo ndiyo maana wengine hatuji, wameweka dola 1,500 bado kunajaa, maana yake nini, matajiri hawapendi kubanwa, matajiri hawapendi kuzungukwa na watu wengi. Kwa hiyo bado unaweza ukasema kwa mbuga zetu hizi mbili nitaweka tu hawa na nina hakika watajaa na tutapata pesa ny ingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la biashara, nimemsikia rafiki yangu hapa amesema vizuri sana Mbunge wa Gairo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Shabiby.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: ...Mheshimiwa Shabiby na mimi nataka niende kwenye *angle* moja, juzi Mheshimiwa Rais alifanya jambo kubwa la kihistoria allikutana na wafanyabiashara, moja ya mambo muhimu sana Rais amesema sijui kama naona hamna anaye-*pick up*, Rais amesema anatamani akimaliza muda wake atengeneze mabilionea 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais anatamani Watanzania waende kuwekeza Kenya, waende kuwekeza kwenye *SADC*, waende kuwekeza kote Afrika, sasa ukitaka kwenda kuwekeza leo nje ya Tanzania, kupata vibali pale *BOT* ni shughuli kubwa mno, leo una fedha zako kwenye *bank account, there is a business* unataka kwenda kuwekeza Burundi, brother kupata vibali *BOT* ni shughuli kubwa mno, kuna *over regulation*, ukiweka *over regulation* huwezi kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hizi nchi ambazo bado tunakua lazima kuwe na *flexibility*, leo hapa amesema habari ya magari yote yanakwenda yanaji-*register* Rwanda na Zambia, nikwambie ukiwa na magari ya *transport* Rwanda unalipa kodi hii, moja tu shilingi milioni moja basi, hakuna *Corporate Tax*, hakuna nini, ni shilingi milioni hii mmemalizana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ukiwa na magari 100 wana milioni yao mia moja unaenda unalipa shughuli imeisha, wewe ungekuwa mfanyakibashara utaacha kwenda huko, njoo hapa kwetu, kuna *Corporate Tax*, kuna OSHA, kuna nani, kuna *service levy* yote haya ni huyo mwenye magari. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa maana ya mfanyakibasha yejete atakwenda huko, nataka kusema kama tunataka kwenda huko lazima tufanye kama wenzetu, lakini nataka nipendekeze na amesema hapa Mheshimiwa Shabiby suala la *VAT* kwenye *petrol stations* mimi niwaombe Serikali na Waziri naomba hili ultafakari sana, hakuna mwenye *petrol station* ambaye anajuzia mafuta? Wote mafuta wanachukua kwenye *depot*, kama wewe ni mtu wa *PUMA* unachukua *PUMA*, kama ni *TOTAL* unachukua *TOTAL*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo leo Serikali ukienda pale *PUMA* ukamuuliza swali moja tu una *petrol stations* ngapi atakwambia 50, nipe *sales* zao au walivyoagiza mafuta kwa mwaka anakupa *list* yako, akishakupa anakupa na *cost* unajua kwa sababu una *EWURA*, maana yake ni nini, unajua kwa kituo hiki kwa mafuta aliyouza labda lita milioni moja kwa mwaka alipata faida kiasi hiki, atakuonesha *cost* zake analipa kodi, rahisi tu, rahisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini hii tunaweka, haya amesema naweza mafuta yasifike kwenye *petrol station* na bado hiyo *EFD* mashine wala isifanye kazi, so mimi ninachosema tutafakari umefika wakati tupunguze gharama za kukusanya kodi, kwa sababu gharama za kukusanya kodi nazo kubwa sana, kwa hiyo niombe hilo watu wa Wizara ya Fedha mtusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, namshukuru Rais na amesema vizuri sana, tunahitaji tuwe na marafiki na wafanyakibashara, naombeni sana unajua kwa miaka minne hii, nimekuwa namsikiliza sana Naibu Waziri wa Fedha akiwa anajibu hoja Bungeni hapa, siku zote suala la biashara kufungwa halijawahi kumshtua huyu mama hata siku moja, anasema biashara zitafungwa, tunafungua zingine. Ni sawa,

lakini jamani hivi kuna nyongeza mbaya? Kama biashara ipo halafu ukafungua zingine hivi ni dhambi? Kwa nini ujidai kwa kufunga? Kama unaona ni faraja nimefunga *why*? Lakini tunasahau biashara inayoanzishwa leo haileti kodi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunasahau, biashara ikianzishwa leo haileti kodi hiyo, biashara ikianzishwa leo hailipi kodi, lakini yule aliyekuwepo huyu tuna historia naye. Kwa hiyo mimi ningewaomba sana Waziri ndugu yangu tujitahidi tusifunge biashara na hii habari na mimi naomba sana, hii habari ya kuwa-*involve* TAKUKURU, watu wa vyombo nya ulinzi kwa ajili ya kodi siyo sawa. Kodi tuwaachie wafanyakazi wa kodi, kodi tuwaachie watu waliosoma kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana leo unasikia pale Wizara ya Fedha wamepangishwa foleni wafanyabiashara, kwani ungemuita Ofisi ya *TRA* akaenda akakutana na mtu wa *TRA* kuna dhambi gani, *why* uwatishe, saini hapa, tunakupa siku saba, uwe umelipa, hii siyo sawa, hii siyo sawa na naamini Mheshimiwa Rais hili halijui, kwa sababu Rais anataka *dialogue* kwamba wewe njoo ufanye biashara na mimi nifanye biashara na wewe. Naombeni watu wa kodi tubadilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba sana suala la Marekani kuna kitu wanaitwa *Small Business Act*, Waziri wa Fedha naomba utafakari kuleta *Small Business Act*, kwamba *Corporate Tax* ni *thirty percent*, inawezekanaje ACACIA aliye *thirty percent* na *Serukamba Company* aliye *thirty percent* ni watu wawili tofauti hawa, tutengeneze utaratibu kulingana na mitaji ya watu. Tunasema kuanzia mtaji wa milioni mpaka milioni 20 *blacket yake* iwe hii, kutoka milioni 20 mpaka milioni 100 iwe hii, kutoka milioni 100 mpaka bilioni moja iwe hii, bilioni moja *and above* iwe hii, maana yake ni nini, watu wana-*graduate* akifanya vizuri zaidi anapanda kule, *on doing this* tutawa-*incoporate* watu wote wataingia kwenye wigo wa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema na mimi hii nairudia tena, Watanzania wengi wote, Watanzania wote wanalipa kodi, tofauti yetu kuna anayelipa *direct tax* kuna anayelipa *indirect tax*. Mtu ye yote anayenunua sukari analipa kodi, ukinunua soda unalipa kodi, ukinunua mkate unalipa kodi, wote na ndiyo maana nchi zilizoendelea kama kuna eneo wanahangaika nalo ni suala la *employment*. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, ukihakikisha watu wako wana kazi, maana yake wana *purchasing power*, wakishakuwa na *purchasing power* watatumia, wakitumia watalipa kodi. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi namshukuru sana Waziri wa Fedha, nampongeza sana yeye na watu wake Wizarani kwa kazi kubwa wanayofanya, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge na jioni tutaendelea na mjadala wetu, kama nilivyosema kila ambaye jina lake limekuja hapa atapata nafasi ya kuzungumza, kwa hiyo msiwe na wasiwasi kabisa, tutaanza na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Augustine Vuma, Mheshimiwa Saed Kubenea na kadhalika, wote mtapata nafasi ya kuzungumza.

Tulipata wageni wengine, tuna wageni wengi sana jambo ambalo nawapongezeni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kweli Bunge letu limekuwa ni moja ya kivutio kikubwa sana cha utalii kwa Dodoma kabisa, kabisa na hasa kwa watoto wetu wa mashule mbalimbali wamekuwa

wakisafiri toka kona zote za nchi yetu kuja hapa na kujifunza kuhusu Bunge lakini pia tunapata wageni wa aina mbalimbali, jambo ambalo linatia moyo kabisa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuna wageni wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni wapiga kura wake toka Mbulu Vijijini ambaao ni Ndugu Neema Damiano na Ndugu Daniel Safari popote pale mlipo karibuni sana. (*Makofi*)

Lakini, pia tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambaao ni rafiki zake kutoka Mikoa ya Kagera na Mwanza wakiongozwa na Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Kagera CCM, Ndugu Christopher Kilaja karibuni, yule kule. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni kutoka *Tanzania Parliamentarian Against Malaria* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Joyce Kafanabo, karibu sana Joyce na wengine, wengine wanaweza wakawa wako kantini kule. (*Makofi*)

Wageni 119 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari Nyanza Adventist ya Jijini Mwanza wakiongozwa na Mwalimu Charity Echenga, ooh karibuni sana, sana, sana, sana, karibuni watoto wetu mnapendeza kweli kweli kutoka Shule ya Sekondari ya Nyanza Adventist hao. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Raphael Michael ambaao ni Waandishi wa Habari kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Paul William Mruma karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni kumi na tatu wa Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba na Mheshimiwa Abdallah Chikota ambaao ni wahitimu wa Chuo cha Ualimu Marangu, Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Ndugu Jumanne Hussein, wa Marangu wale, karibu sana, ahhha, wale kule, karibuni sana jamani, Chuo kizuri sana kile. (*Makofi*)

Wageni thelathini wa Mheshimiwa Shaaban Shekilindi ambaao ni wanafunzi kutoka *Youth Peace Makers* ya Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Ndugu Peter Jali karibuni sana *Youth Peace Makers*, karibu sana Dodoma. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambaao ni jamaa zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Leo Wang na Ndugu Daniel Just, karibuni sana, wale pale. (*Makofii*)

Wageni sana wa Mheshimiwa Abdallah Ulega ambaao ni wakulima kutoka Jimboni Mkuranga, Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Abdul Zombe, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa John Pallangyo wakiongozwa na Mwallimu James Mcchembe *DASwa Wilaya* ya Arumeru karibuni sana popote mtakapokuwa, wale kule, lakini kwa ajili ya mafunzo walimu na wanafunzi ishirini na nane kutoka Shule ya Sekondari ya Mtitaa iliyoko Dodoma, wale wa Mtitaa, oohh karibuni sana, karibuni watoto wa kutoka Mtitaa ahsanteni sana, hicho ni kijiji kimojawapo cha wakulima wakubwa wa zabibu. (*Makofii*)

Kama nilivyosema mwanzoni wale wote ambaao mnakwenda Misri maelezo mtayapata kwa Mheshimiwa Ngeleja na timu yake ile ambayo tumeshaitaja mwanzoni kama mnahitaji maelezo yoyote yale ziada kitu muhimu ni kwamba safari ni kesho usiku, mtapata taarifa zote huko.

Kamati ya Uongozi tukumbuke kukutana *immediately* baada ya hapa kwenye Ukumbi wa Spika hapa nyuma yangu.

Basi baada ya matangazo hayo naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ya leo.

(Saa 07:00 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11:00 Jioni)

(Saa 11:00 Jioni Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae!

Katibu!

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Augustine Vuma, Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Hasna Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Christopher Chiza ajiandae.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Kwanza nianze kwa kumpongeza kaka yangu Dkt. Mpango pamoja na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti naona ni namna gani taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri ilivyozingatia maoni mbalimbali ya wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Mheshimiwa Waziri hongera sana. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie hali halisi ya reli ya katii; sote tunafahamu kwamba reli ya katii ni reli ambayo inasaidia sana wafayabiashara wanaopeleka mizigo Congo, Burundi na Zambia. Lakini leo hii kuna tatizo kubwa la upungufu wa mabehewa kwenye Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano na Mpango wa Mwaka Mmoja wameonesha kwamba wanajipanga kununua mabehewa mapya na wanajipanga kununua vichwa vyta treni.

Mimi naomba tu niiishauri Serikali hebu tuharakishe haraka kununua mabehewa, kwa nini nasema hivi; juzi tu hapa mimi ni mdau katika kufanya biashara kidogo tumelipa shilingi 54,195,000 kwa ajili ya mabehewa 13 kusafirisha tani 520 kwenda Kalemi. Kwa bahati mbaya tunaambiwa kwamba mmelipa hizi pesa, lakini mabehewa mtayapata baada ya miezi mitatu au miezi sita. Sasa wafanyabiashara wanashindwa kuendelea kufanya biashara na Wakongo kwa sababu unachukua *tender* kwa Wakongo, unawaahidi kwamba ndani ya wiki tatu au mwezi utakuwa umewafikishia mizigo yao Kigoma ili waweze kupakia kwenye meli kupeleka Kalemi au kupeleka Burundi matokeo yake wenzetu wa *TRL* hawana mabehewa ya kutosha kwa ajili ya kubeba mizigo.

Kwa hiyo, mimi niliomba nijikite kwenye hili ili Mheshimiwa Waziri kwa sababu mmeonesha kwenye bajeti ya Wizara ya Mlundombinu kwamba wana bajeti yao ya kununua mabehewa mapya na vichwa mimi naomba pesa ile ipelekwe ili waweze kununua mabehewa mapya, wafanyabiashara waweze kubeba mizigo kupeleka Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili reli inakwenda na bandari. Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba Bandari ya Kigoma mnaendelea kidogo kidogo kuiboresha. Tunaomba kasi ile ya kuboresha iongezeke zaidi, lakini huku tukiboresha bandari nimeona katika mpango na katika bajeti ya mwaka 2019/2020 mmeonesha kwamba kuna ununuzi wa meli mpya kwa ajili ya mizigo kwenye Ziwa Tanganyika, lakini kuna ununuzi wa meli mpya kwa ajili ya abiria. Mimi niombe Mheshimiwa Waziri utusaidie meli hiyo iweze kununuliwa kwenye mwaka wa fedha ujao kama ambavyo mlivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie *SGR*; nimeona kwenye Kamati ya Bajeti hapa ule mtandao wa ujenzi wa *SGR* kwa maana ya kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka; Isaka - Mwanza halifu ndio iende Tabora - Kigoma; Kigoma - Kalema, na hatimaye Uvinza huko Songati mpaka Kigali. Mimi niombe Serikali natambua kwa sasa hivi tumejipanga ku-

concentrate na huu mtandao wa kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka; Isaka - Mwanza lakini wakati tunakwenda Mwanza tuangalie nah ii *route* ya kwenda Tabora; Tabora - Kigoma tukifanya hivyo tutawezesha sasa kupokea mizigo inayokwenda Kongo lakini pia mizigo inayotoka Kongo inayoingia Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa nilizonazo Rais Mstaafu Kabila wa *DRC* ameshasimamia kule Kalemi bandari imekamilika, wamekamilisha na meli kubwa ya kubeba mizigo na *target* yao ni nini? *Target* yao ni kuchukua yale madini ya kolta kuyatoa Kalemi na kuyaleta Dar es Salaam na tayari wameona kwamba Mheshimiwa Rais wetu ameanzisha masoko ya madini kitu ambacho Wakongomani kimewafurahisha sana. Sasa wanajipanga kuwa wanatoa dhahabu, wanatoa yale madini ya kolta kutoka kule kuyaleta Dar es Salaam. Sasa tukuombe Mheshimiwa Waziri hivi katika huu mtandao wa *SGR*tuweke mkazo na kutoka Isaka - Tabora - Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili nizungumzie kiwanja cha ndege cha Kigoma. Hivi karibuni tulimpokea Spika wa Bunge la Burundi pamoja na Wabunge walisafiri kutoka Burundi kwa magari mpaka Kigoma, wakapanda ndege pale mpaka Dar es Salaam, Dar es Salaam ndio wakapanda tena ndege kuja Dodoma, lakini wanachosikitika wao ni kwamba hakuna yaani ile *airport* pale ikiboreshwaa wao wanaweza wakawa wanasafiri kwenda nje ya nchi kwa kutumia kiwanja kile kile ili mradi tu *connection* ziweze kuimarishe vizuri. Sasa kile kiwanja cha Kigoma tulishawalipa fidia wananchi, wananchi hawadai tena fidia.

Sasa najiuliza swalii kigugumizi ni nini katika kuendeleza kile kiwanja cha Kigoma? Tukiendeleze kiwanja cha Kigoma ili tuwe na *route* ya kwenda Kalemi tuwe sasa hivi tuna *route* ya kwenda Bujumbura tunataka sasa tuwe na *route* ya kwenda Kalemi, tuwe na *route* ya kwenda Lubumbashi, tufungue mipaka zaidi ya kibashara, wafanyabiashara kutoka nchi hizi jirani waweze kuingia Kigoma wafanye biashara zao na hatimaye warudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo sasa nizungumzie masuala ya jimboni kwangu. Tunafahamu kwamba vyanzo vingi vya Halmashauri vimechukuliwa na Serikali kuu na sasa hivi hali ya Halmashauri zetu Wakurugenzi wanashindwa kuwalipa Waheshimiwa Madiwani hata posho za vikao. Sasa nilifikiri katika hii *Finance Bill* labda vile vyanzo tulivyovichukua vya Halmashauri ilikuwa sasa ni wakati muafaka kuvirejesha kwenye Halmashauri zetu. Kwa nini nasema hivyo; tuone kwenye makusanyo ya majengo, kodi ya majengo tulimuuliza *DG* wa *TRA* kwamba ninyi *target* yenu mlikuwa ni kukusanya kiasi gani wanasema ilikuwa ni kukusanya Halmashauri zote 180; lakini mmekusanya kiasi gani? Tumekusanya kwenye Halmashauri 30 tu.

Sasa unajiliza tuna Halmashauri 180 *TRA* wameweza kukusanya Halmashauri 30 peke yake; kwa nini hivi vyanzo sasa kama vimeshindikana Serikali Kuu tusivirudishe kule halmashauri ili Wakurugenzi waendelee kusimamia. Nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu hali za Halmashauri zetu ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie miradi ya maendeleo. Tunayo miradi ya maji, imekuwa ni hadithi. Tuna miraji ya maji ambayo inashindwa kukamilika zaidi ya miaka 15 tangu awamu ya Mheshimiwa Mkapa, awamu ya Mheshimiwa Jakaya na sasa tuko awamu ya Mheshimiwa Magufuli tunayo miradi ya maji ambayo haikamiliki. Mfano peke yake mimi jimboni kwangu nina mradi mkubwa kule Rukoma na mradi mkubwa pale Kandaga...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasna sekunde 30 malizia sentensi muda wako umeisha

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru niombe tu Serikali labda tufunge macho, tujaribu kumaliza miradi yote ile ya maji iliyokuwa huko nyuma halafu ndio tuendelee na miradi mipya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba kuunga mkono na nampongeza sana kaka yangu Mpango. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye bajeti yetu ambayo imewasilishwa kwa umakini mkubwa sana na Waziri wetu wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango na kwa kuanza tu niwatoe mashaka juu ya utendaji wenu wa kazi Dkt. Mpango na Naibu Waziri na mimi nataka niwape moyo kwamba ukiona watu wa upande wa pili wanawashambulia basi mjue mnafanya kazi nzuri, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imejaa hali ya matarajio makubwa sana kwa Watanzania na sisi wote tunaunga mkono juhudhi ambazo Serikali inazifanya chini ya uongozi wa Rais wetu Jemedari Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kwa hakika wananchi wengi wamekuwa na imani kubwa na bajeti ya mwaka huu hasa pale ambapo mlilikita sana katika kuhakikisha kwamba mnapunguza kodi mbalimbali, lakini kuweka utaratibu mzuri wa wafanyabiashara kutozwa pale *TRA*, kwa hiyo, mwaka huu mmeweuka maelekezo mazuri ambayo wafanyabiashara wengi wameunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nijikite kwenye Serikali kwanza Serikali za Mitaa. Uongozi wa Serikali unaanzia kwenye kijiji na pia kwenye mtaa. Mimi niiombe Serikali, Wabunge wengi wamekuwa wakilalamikia juu ya kutoona umuhimu kwa sasa wa kuwalipa walau kifuta machozi Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa. (*Makofii*)

Mimi nataka niseme *ni-declare interest* kwamba ni nafasi ambayo niliitumikia niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa pale Dar es Salaam, nimekuwa Diwani,

nimekuwa Meya, hadi sasa nimekuwa Mbunge, hakuna nafasi ngumu kuiongoza kama ya kuwa Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Mtaa. Kwa hiyo kwa kweli ningeomba sana kama haiwezekani kuwapa hizo posho kila mwezi basi tunapofika mwisho wa kipindi cha miaka mitano nafasi hii ifikiriwe kama wanavyofikiriwa Madiwani na wanavyofikiriwa Wabunge walau wanapata chochote kutokana na kazi waliyofanya katika miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije pia katika suala zima la umuhimu wa afya ya Watanzania; kwanza nipongeze Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi ambavyo imesaidia sana kwenye sekta ya afya. Tumejenga vituo vya afya zaidi ya 350, tumejenga hospitali zaidi ya 67 sasa hivi na bado mahitaji yapo ni makubwa. Mimi niombe tu Serikali sasa pia ielekeze katika maeneo mahususi ambayo huduma hii ya afya inahitajika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenda jimbo langu pale Jimbo la Lulindi Wilaya ya Masasi kuna maeneo mawili ambayo yanahitaji kwa kiasi kikubwa sana Serikali itazame macho kuwapelekea kituo cha afya na maeneo hayo ni Mnavira pamoja na Kata ya Lipumburu. Kata ya Mnavira iko mpakani mwa Tanzania na Msumbiji, eneo hili limekuwa likikubwa na matukio mbalimbali ya wananchi kupoteza maisha, lakini kupoteza viungo kutokana na wimbi kubwa la mamba ambao mara nyingi nimekuwa nikilisema ndani ya Bunge. Hivyo wakipata majeraha wengi wanapoteza maisha kwa sababu kutoka Mnavira hadi kufika kwenye Hospitali ya Wilaya ni kiometa 50 kufika Masasi Mjini, kwa hiyo, pale panahitajika na bahati nzuri wananchi wa pale pamoja na Halmashauri imejitolea kujenga Jengo la *OPD*. Kwa hiyo, majengo mengine tu yaliyobaki ili pale pawe na kituo cha afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kwenye ile Kata ya Lipumburu ambayo pia ndio kata ambayo Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin Mkapa anatoka kwa kweli lile eneo linahitaji kuwa na kituo cha afya ambacho

kitahudumia kata ile ya Lupaso pia na Kata ya Lipumburu.
(Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la ukusanyaji wa mapato ya *property tax*. Bahati nzuri mimi nilishuhudia wakati nilipokuwa kwenye ngazi hizi zingine za Serikali za Mitaa jinsi ambavyo Halmashauri tulikuwa tunafanya vizuri katika ukusanyaji wa *property tax*. Lakini baada ya kuchukua *TRA* naona kama kuna hali ya kushuka kwa kiwango cha ukusanyaji wa kodi hii. Mimi niseme tu wananchi wapo tayari kabisa kulipa lakini mamlaka zinazopewa kazi hii ya ukusanyaji haziko makini katika kuhakikisha zinafuatilia suala hili la kodi ya majengo, nisehemu ambayo likizingatiwa tutapata kipato kikubwa na kuisaidia Serikali kutimiza wajibu wake katika maeneo mbalimbali.
(Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilitaka niliseme ni juu ya suala zima la umuhimu wa mitandao na ujenzi wa minara katika maeneo yetu. Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikisema kwamba kama kuna maeneo muhimu ya kuhakikisha minara inajengwa ni mipakani yaani kati ya nchi na nchi na mimi jimbo langu linapakana na Msumbiji. Lakini hadi sasa hivi ninavyosema wananchi wa maeneo yangu ya Nanyemyo, Mnavira, Chipolopola, Sindano wanatumia mitandao kutoka Msumbiji. Kwa hiyo, mimi ningeomba sana Serikali kwamba badala ya wananchi kwenda kununua vocha za mitandao ya Msumbiji basi fedha zile zingetumika kununua mitandao ya hapa nchini na kuiingizia mapato Serikali yetu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ihakikishe kwamba maeneo haya ya mipakani ambayo Serikali ilishaeleza umuhimu wa kujenga minara hiyo iweze kujengwa. *(Makofii)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningeomba sana ni kwamba bahati nzuri tuna Daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, lakini eneo kubwa la kiuchumi ambalo linafanya biashara kati ya Msumbiji na Tanzania halipo kwenye eneo lile ambalo daraja limejengwa. Ningeomba sana Serikali tunapoteza mapato mengi sana kutokana na

jinsi ambavyo hatuzingatii suala la ukusanyaji mapato katika nchi ya Tanzania na Msumbiji. Vifaa vingi vinatoka Msumbiji kuingia hapa lakini hakuna ushuru wowote uliotolewa. Pia Serikali iangalie kwamba uwepo uwezekano wa kujenga daraja lingine pale Mtwara maeneo ya pale Chilambo ambapo tukijenga daraja lile pale tutaweza kudhibiti kwa kiasi kikubwa sana mapato kati ya Tanzania na Msumbiji. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hili jambo ningeomba sana sana Serikali ilitazame kwa macho mawili kuhakikisha kwamba tunapata mapato kutoka Msumbiji kama tulivyopata mapato kutoka nchi zingine zinazopakana na Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na mchango huo na najua muda ni mfupi kwa hiyo naunga mkono bajeti hili kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Christopher Chiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea, Mheshimiwa Alex Gashaza ajiandae.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru na nafasi hii naomba kwanza na mimi niwapongeze mawaziri hawa mahiri kabisa ndugu yangu Mpango na dada yangu Kijaji, kwa kweli ninyi ni mahiri kwa sababu hata mnavyojenga hoja zenu na mnavyojibu maswali yetu hapa inaonesha kabisa kwamba ninyi ni mahiri na kwa maana hiyo ndio maana mmetuletea bajeti *proposal* ambayo pia ni mahiri inatekelezaka, kwa kweli nawapongeza sana. (*Makofi*)

Pia naomba kabla sijaingia kuchangia niwashukuru kwa sababu Serikali inapotenga bajeti hata kama mambo mengine yanajitokeza hata kama hatuwezi tukatekeleza bajeti yote kila mwaka, kwa kweli sidhani kama kuna bajeti ambayo inatekelezwa 100% lakini ukiweza kuitekeleza kiwango *percentage* fulani hilo ndilo tunalolitaka. Kwa maana hiyo nataka niwashukuru leo hii nikiwa hapa hapa nataka niwashukuru Serikali yangu sikivu dada yangu

Ndalichako amepeleka fedha shilingi milioni 66 kule Kigoma kwenye shule ambayo aliahidi alipotembelea kule shilingi milioni 66; nakushukuru sana Mheshimiwa Ndalichako nashukuru sana Serikali kwa sababu ndio maana ya kutenga bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikiwa hapa hapa nimepata taarifa kwamba Profesa Mbarawa ametuma *man engineer* kule kwangu baada ya kukagua miradi ya maji ambayo imejengwa wakati ule wa vijiji kumi tukapoteza shilingi bilioni 1.8, miradi haikujengwa vizuri lakini akaja akaahidi kwamba sasa nitatuma wataalam na wataikarabati ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa na hapa nikiwa hapa hapa nimepata taarifa kwamba ametuma kwa kweli nakushukuru sana, naishukuru Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na mwenzake na Wizara nzima kwa kuleta pendekezo la kuondoa tozo hizi mbalimbali 54 na nitajikita kwa chache kama muda utatosha nitakwenda kwa mambo mengine. Naomba nizungumzie pendekezo la marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nadhani iko kwenye ukurasa wa 57. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi nadhani alikuwa Mheshimiwa Shabiby alizungumzia masuala ya mashine za *EFD*, na hapa nimeona Serikali inapendekeza kuondoa ushuru au kupunguza ushuru wa mashine za *EFD* kutoka 10% mpaka 0%. Kwa kweli ni jambo jema kwa sababu mashine hizi zinatusaidia kukusanya mapato. Nataka nikwambie Mheshimiwa Waziri, mimi niliwahi kuhudhuria mkutano wa *TCCIA* na alikuja mtu wa *TRA* akatufundisha jinsi mashine zile zinavyoagizwa. Akatuonesha pia kwamba mashine zile kama zilivyo *gadgets* nydingine hizi za simu, hata zile nazo watu wanaweza ku-*tempernazo* na kwa maana hiyo mashine zile wakati mwengine zinaweza zikawa hazitoi taarifa sahihi, zikawa ama zinaiumiza Serikali au zinamuumiza mlaji.

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu hapa ni kwamba mashine hizi zikaguliwe mara kwa mara, kwa sababu mtu huyu aliyetuambia alikuwa mtu wa *TRA* mwenyewe. Naamini watu wa *TRA* ndiyo wanaozisimamia mashine hizi, bila shaka alikuwa anasema kitu anachokijua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la pili kwa Mheshimiwa Waziri, kwa mfanyakishara anayetaka kutunza taarifa zake ili baadaye aweze kujikagua au akaguliwe anahitaji kutunza kumbukumbu. Mashine nyingi za *EFD* hasa hizi za kwenye mashine za *petrol* ukiweka nyumbani baada ya miezi mitatu, minne haisomeki tena yamefutika yote, kama hujaweza kuzipiga *photocopy* basi hizi taarifa na kumbukumbu utakuwa hunazo tena.

Kwa hiyo, naomba kwa kweli hizi ziangaliwe upya, kama ikiwezekana zikaguliwe, kama ni mashine ziwe *improved* kwa sababu tunapopata zile risiti tunazihitaji kuzitunza ili mwisho wa mwaka tuweze kufanya tathmini kwamba na sisi katika biashara zetu tumefanya nini, lakini unapokwenda kukagua tena risiti zako unakuta haisomeki huna tena mahali pa kufanya *reference*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kidogo sasa nizungumzie habari ya sukari; umependekeza kupunguza ushuru wa sukari hasa ile ya matumizi ya kawaida (*brown sugar*) kutoka asilimia 100 kwenda asilimia 35. Hili ni Jambo ambalo nadhani mara nyingi karibu kila mwaka tunapopata upungufu wa sukari linajitokeza na kwa kushirikiana na wenzetu Afrika Mashariki linatekelezwa. Jambo ambalo sikuona Mheshimiwa Waziri labda sikusoma vizuri, lakini sikuona ukizungumzia habari ya sukari ya viwandani (*industrial sugar*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaja hapa nimeongea na Bodi ya Sukari, wakaniambia mahitaji ya sukari yote yaani ile ya mezani na ya viwandani tani 670,000. Mahitaji ya viwandani kwa maana ya sukari ile ya kutengeneza bia, pipi, *biscuit* na vitu vingine peremende ambavyo ni viwanda hivyo ni tani 155,000. Sukari yote hii tani

155,000 hakuna inayozalishwa ndani, hakuna labda kama wameanza sasa, lakini mimi ninavyojuwa viwanda vyetu vyote *TPC*, Kagera, Mtibwa, Kilombero sidhani kama kuna kiwanda kinachozalisha *industrial sugar*, yote hii inatoka nje. Kama inatoka nje kwa uzoefu najua na yenyewe huwa inasamehewa kodi na ikisamehewa kodi sukari hii ikiingia basi inabidi kwa kweli iangaliwe vizuri maana uzoefu umetuonesha wakati ule wa sakata la sukari kwamba sukari hii hii ambayo inaingizwa ikiwa imesamehewa ushuru mara nyingine tena unaikuta kwenye *supermarkets* ikitumika kama sukari ya kawaida. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili siyo jambo zuri, kwa kweli hata kwa wafanyabiashara siyo jambo zuri lakini hata kwa walaji maana yake ile sukari sidhani kama inatakiwa itumike kwa ajili ya chai au kwa ajili ya uji. Ile ni *purely* kwa ajili ya viwandani, *I stand to be corrected*, lakini mimi ndivyo ninavyoelewa, sasa sikuiona ikizungumziwa katika hotuba yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida ni tani 515,000 na uzalishaji wa ndani mwaka huu kwa *brown sugar* nimeambiwa ni tani 359,219 angalau kwa mwaka huu. Ukitazama hesabu zote hizi ukijumlisha ile sukari ya viwandani na sukari ya mezani ambayo ni upungufu wa tani 155,781 unakuta bado tuna upungufu wa zaidi ya tani laki tatu na kitu. Maana yake ni kwamba lazima tutaendelea kuagiza sukari na hii ya *industrial sugar* hii ndiyo hasa nataka niizungumzie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, mimi ushauri wangu ni kwamba tuongeze uwekezaji katika mashamba ya miwa, lakini mashamba ya miwa hayawezi kuendelezwa bila umwagiliaji. Mashamba ya miwa lazima yaende sambamba na umwagiliaji, yako mazao karibu matatu ambayo sasa kitaalamu huwezi uka-break even bila kumwagilia. Moja ni miwa, lingine ni mpunga na lingine ni mazao ya bustani (*hot cultural crops*). Mazao haya sitaingia kwa undani kwa nini, lakini huwezi uka-break even bila kumwagilia, mengine utakuta kwamba hata *circle*

yake uzalishaji yanakwenda zaidi ya miezi sita hakuna mvua inayokwenda zaidi ya miezi sita katika nchi hii lazima ufanye supplementary irrigation.

Kwa hiyo, katika kuwekeza katika uzalishaji wa miwa ni lazima tuongeze uzalishaji, tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji vinginevyo hatutaweza ku-*break even*. Kwa maana hiyo ni kwamba wale wanaolima miwa wakiwa ni wazalishaji wakubwa wao wanaweza kuweka miundombinu yao, lakini wale wana-nuclears farms, outgrowers lazima wasaidiwe. Ukienda Kilombero kuna outgrowers, wale hawawezi kujiwekea miundombinu wenyewe ya umwagiliaji ili wazalishe miwa mingi ya kukiuzia kiwanda kwa hiyo hapa ni lazima Serikali itusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu namba mbili, naomba sasa kwa kuwa viwanda vyetu vya ndani havizalishi sukari ya viwandani na ninajua sababu kubwa, sababu kubwa ni kwamba wanaogopa kuweka mitambo ile ya kusafisha sukari maana ile *industrial sugar* ile siyo sukari nydingine ni kwamba ni hiyo hiyo inakuwa *refined* vizuri, sasa hawaiweki hii mitambo hii. Kwa hiyo, ninaomba wakati tunawahamasisha wawekezaji hawa tuwawekee na component hii kwamba jamani eeh mnapotuzalishia sukari m jitahidi kuweka na mitambo ya kusafisha sukari hii tuzalishie sukari ya viwandani. Maana sukari ya viwandani hii ni malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu, viwanda hivi vya pipi vinginevyo viwanda hivi tutaendelea kuagiza malighafi kutoka nje kwa ajili ya kulisha viwanda hivi. Ushauri wangu namba tatu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba nimeshausema lakini nataka nirudie, *industrial sugar* isiuze kama sukari ya kula mezani, isikutwe katika supermarkets. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nirudi tena kwenye kilimo, wengi wamezungumzia kilimo, wamezungumzia umwagiliaji na kwamba ili tutoke kwenye agrarian reforms sasa tuingie kwenye mambo ya viwanda, kilimo bado ndicho kitaendelea kuwa mhimili wa kutoa malighafi. Ninachotaka kuzungumza.... (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Saed Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza, Mhehimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha ya Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali. Kwanza niseme masikitiko yangu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anawasilisha hotuba yake hapa Bungeni, aliacha jukumu lake la msingi la kusimamia sera za Serikali juu ya bajeti akajikita kwenye ushabiki wa kushabikia Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu ni Taifa changa sana na sisi wengine hatuna mahali popote pa kwenda, tumezaliwa hapa, tumekulia hapa, tumeishi hapa. Hatujawahi kwenda hata nchi za watu kuishi miaka mitano, miaka kumi, kwa hiyo hatuna mahali pa kwenda, bila kuheshimu utulivu wetu, amani yetu na busara zetu hakika Taifa hili tunaweza tukalipeleka mahali pabaya sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Mpango jukumu lako kubwa ni kuisimamia Serikali juu ya mapato na kututoa hapa tulipo na kuachana kabisa na huu ushabiki wa kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye ukurasa wa 87 na 88 anasema; fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya maendeleo ni shilingi triliioni 12.25 ambayo ni sawa karibu na asilimia 37 ya bajeti. Ukiangalia kwenye hiki kitabu fedha karibu zote zimekwenda kwenye miradi isiyozidi minne,

wametaja hapa reli ya katи (*standard gauge*), umeme wa Mto Rufiji, *REA* na maji. Ili uchumi wetu uweze kukua tungewekeza katika kilimo, tungewekeza katika viwanda, tungewekeza katika umwagiliaji, lakini bajeti za Wizara hizo zote ziko chini ya asilimia tano ya bajeti yote. Sasa unajiuliza tunapojenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma, tumewezaje kuunganisha uchumi wa nchi na kule Congo - Lubumbashi ambapo Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma wanapigania kwamba reli yetu iende? Unajiuliza hiyo mizigo tunaibebaje ikifika Dodoma tunaunganishaji uchumi wetu na nchi za nje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa sana, nashangaa kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Mpango kabla hajawa Waziri wa fedha alikuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango na huu mpango wa miaka ishirini pengine umeandaliwa akiwa ofisini au alishiriki kuuandaa, miaka 25. Sasa leo anakuja na mpango mwingine kabisa wa umeme, na mimi najua kwamba nchi hii kipaumbele chake kikubwa ulikuwa umeme wa makaa ya mawe wa Linganga na chuma cha Mchuchuma, lakini kwenye bajeti nzima Serikali haizungumzi lolote juu ya Mchuchuma, haizungumzi lolote juu ya Liganga, haizungumzi lolote juu ya umeme wa gesi ya Mtware haina kitu kabisa. Wanakuja na miradi mipya kila siku kitu kipyä, kila siku kitu kipyä, tunakwenda wapi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri ni vizuri sana Serikali ikaangalia kwamba miradi ambayo tumeanza nayo mwanzo kama kipaumbele ifanyiwe kazi vizuri ili tusije tukawa tunakwenda kila mtu anakuja na kitu chake. Mheshimiwa Kikwete alikuja na umeme wa gesi hatujamaliza, hata gesi yenye hatujazalisha, hata deni hatujalipa leo tumeachana kabisa na gesi tunakuja na umeme wa maji. Huu umeme wa maji tuliuacha kwa sababu tulipata matatizo makubwa kwenye Kihansi, kwenye Nyumba ya Mungu, kwenye Mtera na Hale. Mabwawa yalikauka na Serikali ikalazimika kuingia kwenye mikataba na makampuni ya kufua umeme wa dharura, nchi ikaingia kwenye matatizo makubwa. Huu umeme wa Rufiji tunaofua hatuna uhakika kama mabadiliko ya tabia nchi hayataweza kutuathiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri Serikali badala ya kuangalia miradi kwa pupa pupa, ifanye uchambuzi yakinifu kwa kila mradi ili tunapoenda kwenye mradi, tunapoingiza fedha za walipa kodi wa nchi hii kwenye miradi mikubwa lazima tuitekeleze. Hii bajeti ukiisoma yote, fedha za maendeleo zinategemea fedha nydingi kutoka nje na fedha za nje hazina uhakika wa kuzipata. Tayari wafadhili kwa mujibu wa Kamati ya Bajeti imesema haiweze tena kuchangia bajeti ya Serikali, inakwenda kujenga miradi moja kwa moja, ni kwa sababu hatuaminiki tena. Usimamizi wetu siyo mzuri wa miradi ya watu na tunakuja hapa baada ya kuwashukuru hawa wanaotupa fedha, tunawakebehi na kuwaita mabeberu, siyo jambo jema hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti inazungumzia uchaguzi mkuu ujao, bajeti inazungumzia uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hapa ni mahali pazuri kabisa muhimu pa kurejesha heshima ya nchi yetu na utulivu wa nchi yetu. Nchi yetu hii imewahi kuingia kwenye matatizo makubwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000; mamia ya wananchi wa Zanzibar, wa Pemba walilazimika kuwa wakimbizi katika nchi yao. Nchi hii ambayo ilikuwa kimbilio la wakimbizi ikaacha ikazalisha wakimbizi kutokana na misingi mibaya ya kusimamia chaguzi zetu. Hata leo ukisoma matokeo ya uchaguzi yaliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi mwaka 2015 ukachukua kura zote zilizotangazwa kwamba zimepigwa, ukachukua kura halali, ukachukua na kura ambazo siyo halali ukijumlisha kwa pamoja hazifungamani kabisa, ni mbingu na ardhi, na hata idadi ya ilioandikishwa katika uchaguzi wa mwaka 2010 na waliopiga kura ni tofauti kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Serikali ikaiboresha Tume ya Taifa ya Uchaguzi na ikaachana na hii biashara ya kukata rufaa kwa ajili ya Wakurugenzi wa Halmashauri walioondolewa na mahakama kusimamia uchaguzi. Kitendo cha kukata rufaa peke yake kimeonesha hila, kinaonesha nia mbaya iliyopo, kwa hiyo, ili tuondoke huko watu waweze kuaminiana, yaliyotokea Zanzibar katika uchaguzi wa mwaka 2015 yasijirudie tena katika uchaguzi ujao wa 2020. Tuipe uwezo Tume ya Uchaguzi ya kusimamia

uchaguzi ulio huru na haki ili anayeshindwa huo uchaguzi aseme ahsante sana. Watu wapeane mikono, waache uhasama wa kisiasa, lakini kwa hii tabia ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango ameionesa humu Bungeni nachelea kusema nina hofu na uchaguzi ujao kwamba unaweza ukawa huru na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu hili limejengwa na wazazi wetu kwa misingi imara kabisa ya demokrasia ya hali ya juu sana, na hili Bunge ndiyo chombo kikubwa kabisa katika Jamhuri ya Muungano cha kuonesha umahiri wetu katika demokrasia. Tusiposimama hapa tukataka Tume yetu ya Uchaguzi ikaendesha chaguzi yetu vizuri na haki, yaliyotokea kwenye nchi za wenzetu yalitokana na mambo haya haya ya kufanya uchaguzi kuwa usanii fulani na wananchi baadae wakakataa uchaguzi huo, tusifike huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya nchi za wenzetu za Afrika ziliingia kwenye matatizo makubwa baada ya Tume zao za Uchaguzi kufanya kazi za kisanii, leo Tume yetu ya Uchaguzi haiaminiki katika macho ya dunia. Wanatokea wenzetu wanatuambia boresheni haki za binadamu, boresheni demokrasia, utawala bora, tunawabazaza. Wakati hao wanaantuambia baadhi yetu tumeishi kwenye nchi zao miaka kumi, tunesoma huko, tumeishi huko, wametupa *scholarship* za kusoma kwao na kuishi kwao tunakuja tunawatukana, siyo haki hata kidogo. Uhusiano wetu na mataifa ya nje ungekuwa ndiyo huo unaombiwa hapa ndani ya Bunge hili hakika isingekuwepo miradi ya *SIDA*, isingekuwapo *JICA*, isingekuwa miradi ya Wajapani wala miradi ya Waingereza hapa nchi hii isingekuwepo, lakini imekuwepo kwa sababu tulisahau yaliyopita tukaganga yajayo na ndivyo nchi zote zinavyojengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *South Africa* leo, kama Afrika Kusini wangekubali kurudishwa nyumba kwenye ubaguzi wa rangi nchi yao isingeenda pale. Ukienda Rwanda, kama Wanyarwanda wangekuwa wanakubali mauaji ya halaiki ya mwaka 1994 yawe kumbukumbu kwenye kichwa

chao nchi yao isingefika hapo ilipoenda, lakini walisahau. Hata kama walitufanya watumwa, walitutawala, tuachene na hivyo vitu tusonge mbele kwa manufaa ya nchi yetu ili kile walichokichukua waweze kukirudisha hapa, kiweze kutusaidia kwenye maendeleo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo la mwisho kabisa ni juu ya kodi ya *pad* ya kina mama ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameiondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika,...

(*Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Kubenea, sekunde thelathini.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utafiti uliofanywa na Shirika la *UNICEF* kati ya wanafunzi 10 wanaosoma shulenii mmoja ameacha shule kwa sababu ya kukosa taulo ya kujihifadhi. Badala ya Serikali ku-*deal* na wafanyabiashara ambaao wananaufaika na huo msamaha, wanakuja kuondoa kodi kwa watu wote, hili jambo sio sahihi na ninalipinga kwa nguvu zote. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa Kubenea. Waheshimiwa Wabunge, anaafuatia Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba ajiandae.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia walau maneno machache kuhakikisha kwamba bajeti yetu inakuwa ni bajeti bora kama ambavyo tumeipokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kuwapongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa namna ambavyo wamekuwa wakitenda kazi na wajibu wao sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba moja kwa moja nijikite kwenye suala zima la hali halisi ya viwanda. Tunafahamu kwamba Serikali yetu inayo dhamira njema ya kuhakikisha viwanda vyote vilivyoko nchini vinapata nguvu, vinawezeshwa, lakini viwanda vyote ambavyo vinategemewa kujengwa hapa nchini vijengwe kwa misingi ya kuzalisha lakini kwa misingi ya kutoa ajira na kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya viwanda halisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanza tuna viwanda vyatya samaki karibia saba mpaka nane. Hivi tunavyozungumza leo ni viwanda takribani vitatu au vinne peke yake ndiyo vinafanya kazi na vyenyewe havifanyi kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Lipo tatizo moja kubwa, mwanzo baada ya operesheni tunafahamu kabisa Serikali ilikuja na bei elekezi ya samaki kuanzia karibia shilingi 5,500 mpaka shilingi 6,000. Leo kilo moja ya samaki inauzwa shilingi 3,800. Huyu mvuvi ili akavue wale samaki sawasawa na kuwaleta anagharamikia zaidi ya lita moja ya mafuta kama unavyofahamu kwa sasa ni shilingi 2,480 hadi 2,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kuwa Serikali imeachaniza hii sekta ya viwanda vyatya samaki, imewaacha wenyewe wafanyakazi na wenyewe viwanda wahangaike kutafuta masoko, wahangaike kutafuta bei ambazo zinaweza kuwasaidia kwenye mafuta, wahangaike wenyewe kuona namna ambavyo wanaweza kuendesha viwanda hivi. Kiwanda kimoja peke yake kilichokuwa na uwezo wa kuajiri wafanyakazi zaidi ya 700 leo kinaajiri wafanyakazi 50 mpaka 90 kwa *shift* moja, kilikuwa na uwezo wa kukata tani 70, leo kinakata tani 15 peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali haitawekeza jicho huku na nimuombe sana Mheshimiwa Waziri hasa Waziri wa Uvuvi warudi nyuma waangalie kushiriki na wavuvi hao

wote ili waweze kushughulikia suala hili la viwanda nya samaki, vinginevyo vitakufa, tutaendelea kupoteza ajira na wafanyabiashara ndogo sio kwamba wanapenda kuweo wengi, wanakuja kwa sababu hakuna kazi za kufanya ndiyo maana wanatafuta mitaji ya shilingi 200,000 waingie sokoni ili waweze walau kuuza bidhaa yoyote ile wajikimu na maisha yao.

Kwa hiyo, niombe sana bidhaa hii jhasa bei ya samaki lazima irudi kuwa elekezi ili wavuvi nao wanakovua kule waone umuhimu na faida ya kwenda kukesha kwenye maji na kurudi nchi kavu kufanya biashara na viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nilitaka kuzungumzia Wakala wa Barabara (*TARURA*). Nimekuwa nikisema siku zote kwamba mimi ni muumini mzuri wa *TARURA*, kwenye bajeti iliyopita tumeongeza fedha kwa ajili ya bajeti ya *TARURA*, inakadirika shilingi bilioni 30 baadae tena ikaongezwa karibia shilingi bilioni 60 hivi na mimi nataka kusema jambo moja; *TARURA* kama tutaijali, kama tutaichukulia kama chombo ambacho tumekitengeneza kwa ajili ya kuja kutoa suluhisho kinaweza kufanya kazi nzuri sana. Suluhisho tunalolizungumza hapa kwenye chombo hiki ni lazima fedha zote zilizotengwa na fedha zilizoongezwa kwenye bajeti zielekezwe *TARURA* ili waweze kutoa mgawanyo ambao ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukichukua kwa mfano Wilaya mbalimbali zilizoko kwenye Jiji la Dar es Salaam na Wilaya zilizoko kwenye Majiji mengine kama Mwanza, leo ukichukua Kinondoni na Nyamagana ni kama vile tunalingana lakini ukija kwenye mgao Nyamagana inapata kidogo, Kinondoni inapata zaidi na hii sio sawa kwa sababu hata miji yote iliyoko pembezoni inahitaji kufunguliwa mtandao wa barabara ili tuweze kwenda sawa na mazingira tunayoyapigania sasa. Vinginevyo tutabaki kupiga kelele humu, fedha ziongezwe halafu fedha zisipokwenda hata utekelezaji wa miradi yenyewe hautafanana na kile ambacho tunakipigania kelele na tunachokiombea kila siku hapa.

Kwa hiyo mimi niombe sana, narudia; *TARURA* ni chombo muhimu na *TARURA* wameanza kuonesha njia. Kama watapewa fedha kama ambavyo tumekubaliana kwenye Bunge hili wakati wa bajeti iliypita ya kisekta sina shaka *TARURA* wanaweza kufanya kazi yao vizuri na mgawanyo narudia tena, uwe sawa kulingana na mahitaji ya kwenye kila mji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili liende sambamba na ahadi zilizokuwa zimetolewa na Mheshimiwa Rais hasa kwenye maeneo haya am bayo sasa yamekabidhiwa *TARURA*, mimi nina barabara karibia tatu za ahadi ya Mheshimiwa Rais, niombe sana barabara ya kutoka *SAUT – Luchelele*; Igoma – Kishiri kutokea Buhongwa; hizi ni ahadi za Mheshimiwa Rais na barabara hizi zimerejeshwa *TARURA* ni lazima sasa *TARURA* waje na mpango wa kutuambia barabara hizi zinajengwaje na Serikali ipeleke fedha hizi ili barabara hizi zijengwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme; tunafahamu *REA* haitoi huduma wala ujenzi wa miradi ya umeme kwenye majiji kwa maana majiji haya yote yana mitaa na hayana vijiji, lakini mimi nimuombe sana Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Nishati wafikirie jambo hili, tunachukua umeme tunapeleka vijijini, hatukatai, ndiyo mfumo. Leo wamekuja na umeme wa mradi wa *peri-urban*, huu mradi wa *peri-urban* kama hautakuja kutekelezwa sawasawa, miji yetu itabaki kuwa na giza ilhali watu wamejitoa na wamejenga majumba kwa kiwango kikubwa sana. (*Makof!*)

Kwa hiyo mimi niombe mradi wa *peri-urban* utakapoanza uelekezwe kwenye maeneo ambayo ni very *strategic* na hii ni biashara, *TANESCO* wanafanya biashara hapa, wanaingiza fedha. Sioni sababu unapeleka transfoma mbali kwa miaka miwili wameunganisha watu wanne badala yake tunapoteza fedha. Walete hizi transfoma mjini watu wamejenga zaidi ya kaya $15,000/20,000$ kwenye kila kata ili tuweze kupata suluhisho la mambo haya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tumejikita kwenye miradi mikubwa sana na sasahivi Serikali inafikiria kwenda kujenga mradi mkubwa wa kuhifadhi mafuta kwa pamoja. Tunakwenda tunafikiria tutatumia zaidi ya dola bilioni 22 lakini sisi tuna wadau, tuna *PUMA* na *TIPER*, hawa sisi tuna hisa asilimia 50 kwa kila kampuni. Lakini kama ndiyo msimamo wa Serikali, hebu tusubiri kwanza tuimarishe hii miradi mikubwa tulinayo, hiyo dola milioni 22 ukiipeleka kwenye *Stiegler's Gorge*, ukiipeleka kwenye *standard gauge* tutakwenda mbali zaidi kuliko kufikiri kujenga matenki ya mafuta leo na huku ni *ku-frustrate* wadau tulionao.

Kwa nini tusikae na hawa wadau? Maana shida ya Tanzania sio kuwa na *reserve* ya mafuta, shida ya Tanzania tulikuwa na uhaba mafuta yanapotoka yanaletwa na nani. Sasa tumeshamaliza mfumo huo, mafuta yanaagizwa kwa pamoja, yanakuja kwa pamoja. Bado iko tatizo, hata leo ukienda bandarini pale tunajenga *flow meter* mpya. Hivi ile *flow meter* ya zamani kule Mji Mwema ina matatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechunguza matatizo yake? Tumebaini matatizo yake? Haitoshi, tunafanya ujenzi mpya, tume-*engage* mkandarasi mshauri, hatumtumii, tunamuacha kama alivyo, leo tunafikiria kuwekeza mradi mwingine tuwatengenezee watu kichaka kipyra na hii ndiyo maana tunaambiwa sisi tunaotunga sera na kuzisimamia tuanzidiwa sana maarifa na watu wanaofanya baishara hizi kule nje na hii sio sawa. Ni lazima maarifa ya watunga sera na wanaozisimamia sera yawe na weledi mkubwa kuliko hawa walioko nje ili tuweze kwenda sambamba na kazi ambayo tunaifikiria na kuifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema tunatamani sana miradi hii mikubwa ikamilike kwa wakati, *Stiegler's Gorge*, *standard gauge* ikifika Mwanza wananchi wa Mwanza watakuwa na ahueni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga hoja mkono asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Masoud Abdallah ajilanda.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako tukufu. Kwanza nianze kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote katika Wizara hii ya Fedha na Mipango kwa sababu kwa ukweli wanajitahidi. Wanajitahidi, hilo halina shaka kwa sababu makusanyo yameongezeka na miradi inatekelezwa. Niseme tu kwa ufupi kwamba huko Buchosa tunaona mambo yanaenda. Makao makuu yetu ya Halmashauri yanajengwa, Hospitali ya Jimbo au ya Halmashauri inajengwa na miradi mingine ya vituo vya afya na kadhalika inatekelezwa vizuri. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukurani hizi naomba niseme mambo ya jumla matatu au manne yafuatayo; moja, ni lile la uamuzi wa Serikali kuruhusu wananchi kuingia bandarini, kila anayeenda kutuma au kupokea mzigو. Hili jambo nimuombe sana Waziri wa Fedha alitazame upya. Huko nyuma bandari yetu iligubikwa na wizi, msongamano, urasimu, rushwa na kadhalika, kuna kitu kinaitwa *port community* wakakaa, wakafikia makubaliano kwamba watu wote wanaokuwa na mzigو ya kutuma au kupokea kuzagaa mle bandarini ni moja ya visababishi vya watu kuiba kuombaomba fedha zisizokuwa na utaratibu kwa sababu wengi wanakwenda kule hawaelewi hata *abc* za utoaji wa mzigو huko bandarini. Nafahamu jana aliongea kwa sauti sana Mheshimiwa Gulamali, lakini naomba tu niendelee kumshawishi Waziri kwamba hili jambo litazameni upya, sio kila mtu anaweza kufungua kompyuta akaona *TANC/S* inavyofanya kazi akaacha kupeleka usumbufu kwa maafisa wa bandari na *TRA* walioko kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo kuna ugumu sana wa watu kufungua kampuni hizi za *clearing and forwarding*, ni kama vile kuna kakundi kanajihakikishia *monopoly* ya hiyo kazi, lakini hizi kampuni zingekuwa nyingi

za kutosha wala hizo gharama Mheshimiwa Mpango unazozisema zisingekuwa kubwa hivyo kwa sababu *competition* ingekuwa kubwa ya kupata wateja and therefore bei za huduma ile zingeshuka.

Kwa hiyo, zitazame tena, tusirudi tena kule bandari yetu hiaminiki, mzigo ukaanza kuhama. Leo tuko kwenye ushindani mkubwa, tuko kwenye ushindani mkubwa na Msumbiji, Kenya, Angola na Namibia. Kwa hiyo tukifanya tu jambo lolote la kuifanya tena bandari yetu ionekane sio *competitive* tunakuwa tunajiharibia wenyewe. Tuyatazame vizuri haya maamuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niombe sana Serikali, nimesikiliza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wakiwasilisha bajeti sikuusikia uwanja wa ndege wa Mwanza ukizungumziwa. Halwezekani Jamani, illkuwa ujengwe wakati wa Mwандоса akiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, sijui kilichotokea, mimi sitaki kwenda huko, lakini ukajengwa wa Songwe, Mwanza tupo tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio kwamba ninakunanihii wewe, hapana, lakini ilikuwa ujengwe Mwanza ukajengwa Songwe tukakaa kimya, kote ni Tanzania. Sasa tunaomba na wa Mwanza ukamilike kwa sababu sio hela nydingi kihivyo kwamba Taifa litafilisika Mwanza tukiwa na *terminal* pale kama mahali pengine zilivyo. Ni mji mkubwa pili hapa nchini, kwa nini usipate sifa na heshima unaostahili?

MHE. FRANK. G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tizeba kuna Taarifa. Mheshimiwa Mwakajoka.

TAARIFA

MHE. FRANK. G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkumbushe tu kaka yangu Mheshimiwa Tizeba pale anazungumzia kwamba eti Songwe walikaa

kimya, lakini ukumbuke kwamba juzi tu Chato kuna uwanja mkubwa kabisa unajengwa pale, kwa hiyo mambo yanaenda vizuri si ndiyo? (*Kicheko*)

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, unajua Mwakajoka nakuheshimu kwa hiyo sitakujibu. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tizeba unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hiyo sijaipokea kwa sababu anajua sio Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa uamuzi wake kabisa na hapa shukurani za pekee ziende kwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wa kujenga daraja la kati ya Busisi na Kigongo. Huo utakuwa ukombozi mkubwa sana kwa watu wa Kanda ya Magharibi. Leo watu wakitoka Dar es Salaam wale wanaokwenda Kagera wanazalazimika kupitia Kahama na kwingineko, lakini lile daraja likikamilika ile njia itakuwa saa 24 watu wanasafiri, maisha yatakuwa murua. Tuombe Mungu tu kwamba daraja hili likamilike mambo ya Watanzania yaende kuwa, na nadhani litakuwa la kwanza la aina yake hapa Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru pia Serikali kwa uamuzi wa kujenga meli ndani ya Ziwa Victoria. Kimekuwa kilio cha watu wa Ziwa Victoria.

Ombi langu Mheshimiwa Kwandikwa, ile meli ikikamilika ile sijui mbili zile, zile ndogo ndogo zianze kuhudumia watu wa visiwani. Kuna visiwa vingi katika Jimbo la Buchosa, kuna visiwa vingi Jimbo la Geita, kuna visiwa vingi Jimbo la Muleba, kuna visiwa vingi Jimbo la Bukoba Vijijiini. Sasa hizi meli zilizopo leo, Butiama, Clarias na kadhalika tunaomba zianze kuhudumia hivyo visiwa, zisije tena na zenyewe zikabaki pale kwenda ile ile *route* ya Bukoba – Mwanza wakati kuna Watanzania chungu nzima kwenye visiwa kule wanasumbuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende jambo lingine la uvuvi. Asubuhi Mheshimiwa Serukamba amezungumza kidogo, naomba nisisitize hili jambo. Bado yako masharti magumu sana kuwafanya Watanzania wafuge samaki majini. Naomba *ni-declare interest* katika hili, ninafanya hiyo shughuli, kwa hiyo ninajua ugumu uliopo kwa mwananchi wa kawaida kufika mahali akapata leseni zote ili aweze kufanya ufugaji wa samaki majini. Masharti bado ni magumu sana. Vibali vya *NEMC* shilingi milioni 20, huyo Mtanzania wa kawaida ili apate kibali cha shilingi milioni 20 yuko wapi? Hujazungumzia kodi zilizoko katika vifaa vya kutengeneza *cage* zenyewe. (*Makofii*)

Kwa hiyo, niombe sana haya mambo yatazameni punguzeni hizi kodi, haya masharti, wezesheni wananchi wafanye shughuli za kujiletea kipato. Leo ziwani kule samaki wa kuzaana tu wenyewe hivi ni shida, Mheshimiwa Mabula amesema hapa viwanda vinafungwa kwa sababu uvuvi ule sio endelevu. Njia bora ya kuwa na uvuvi endelevu ni kufuga samaki. Vietnam na kadhalika wote wanafuga samaki na *wana-export* samaki kwa mabilioni ya dola na sisi tunaweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la jumla ni hili la madeni ya watumishi wa Serikali. Jamani jiwekeni kwenye miguu ya hao walimu, wahudumu, wakunga, sijui watu gani ambaye anadai shilingi 200,000 miaka mitatu au minne. Lakini hilo moja la watumishi, wako watumishi wa umma wa ngazi za vijiji, madiwani na vitongoji, hawa nao wanateseka sana, halmashauri hazina pesa za kukata hizo asilimia 10 kuwapeleka kule. Kwa nini inakuwa vigumu kufikiria kuwapa na wao kamshahara, mimi nakaita kamshahara vyovyote vile lakini ya uhakika. Kuna halmashauri leo Madiwani hawajalipwa posho zao zile za mwezi miezi 10. Wanapata wapi nguvu za kufanya kazi vizuri hawa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mambo ya Buchosa na hakika kama kumbukumbu yangu hainipotoshi ndiyo Halmashauri pekee isiyo na hata sentimeta moja ya lami. Kama yumo Mbunge mwingine humu Halmashauri yake

haina hata sentimeta moja ya lami anyooshe mkono. Acha bwana wewe, Mpanda Mjini imejaa, acha! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tena hili jambo la barabara ya Sengerema – Kahunda, nilongea wakati wa bajeti ya Ujenzi na Uchukuzi yameandikwa maneno sio sahihi, kitabu kile haijulikani kimerekebishwa, Mheshimiwa Kwandikwa namuona *Engineer Kamwelwe* hayupo. Fanyeni kila mnaloweza hili jambo likae sawasawa. Nikipinga bajeti sitakuwa nimekosea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kivuko...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na Mbunge anayefuata, kwa sababu kuna jina la kiongozi aliyeppita ametajwa hapa, nataka kumbukumbu za Bunge pia zikae vizuri. Serikali inapoleta mipango yake Bungeni, ikiwa ni pamoja na mipango ya miundombinu, inaleta bajeti ya kuendeleza maeneo mbalimbali. Hakuna kiongozi atakuja atabadilisha mwelekeo wa mipango ya Serikali kwa sababu yeye anatoka sehemu fulani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, lazima likae vizuri namna hiyo na ndiyo maana hata barabara kila Mbunge anapoomba hapa, hawasemi tutamaliza Wilaya moja ndiyo tuhamie Wilaya nyingine, ama tumalize barabara moja ndiyo tuhamie barabara nyingine na hata hii mipango mikubwa tunayoizungumza ya Serikali imepangwa yote kwa pamoja na inatekelezwa yote kwa pamoja kwa bajeti hiihii, siyo mradi mmoja halafu mwengine utafuata baadaye. Kwa namna hiyo hiyo, barabara zinapoendelezwa ni sawa tu na viwanja vyatia vinaendelezwa, maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Kwa hiyo, lazima kumbukumbu zetu zikae vizuri ili yule ambaye hana fursa ya kuweza kuja kujibu hapa ndani kwa hiyo hoja ya uwanja wa ndege wa Songwe, lazima kumbukumbu za Bunge zikae vizuri, lakini zikae vizuri kwa maeneo yote pamoja na viwanja viliviyotajwa. Unapoendelezwa Mwanza, unapojengwa Chato, unapojengwa Katavi, unapojengwa Katavi, unapojengwa Iringa, kila mahali ni Tanzania, kila mahali panahitaji maendeleo. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Sebastian Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, awali ya yote na mimi naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Nimshukuru Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote ndani ya wizara, lakini naomba naomba pia niseme mbele yako, mimi ni Katibu Mkuu wa Chama cha Kibunge cha Idadi ya Watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyakati tofauti ndani ya mwaka huu, nilikuwepo katika miji ya Kigali, Rwanda; nilikuwepo Accra, Ghana na hivi majuzi nilikuwa Vancouver huko Canada. Dunia kwa ujumla wake inaongelea suala zima la akina mama na watoto wa kike, kwa maana ya idadi yao. Tunaambiwa kuna takribani bilioni 1.7 akina mama na wasichana ambaeo huwezi ukawaacha kwenye uchumi wa dunia. Tukicheza nje ya watu hawa kwa wingi wao, akina mama ambaeo pamoja na kuzungumzia suala la *equality*, lakini ndiyo watu ambaeo tunaambiwa tukija kwenye masuala yanayogusa uchumi, ni watu makini, ni watu ambaeo uchumi wao, katika eneo la kada ya familia, ukikuta kuna baba, kuna mama, mama anaimarisha uchumi wa familia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mipango yetu na bajeti, bila kuwagusa hawa tunakuwa hatujawatendea haki. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, duniani huko, wanawaangalia kwenye sura hiyo na huwezi ukakimbia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa na mtaalam mmoja wa *IFAD*, anakwambia kuijenga dunia bila njaa, huwezi ukaacha akina mama. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na bado tunaambiwa wanakwenda kwa maana wanazalisha kati ya asilimia 20 mpaka 30, sasa nilitaka nianze kwa sura hiyo. Baada ya kulisema hilo, naomba pia Mheshimiwa Mpango, tunaambiwa hivi, tugsie *standard gauge*, tugsie mambo yote, bila kugusa afya ya msingi, kuna tatizo kubwa. Kwa hiyo, uwekezaji ambao hauendi kugusa afya, haya mengine yote hayana nafasi. Nalisema hilo kwa sababu walimu, wanafunzi, iwe ni askari, iwe watu wengine wote, nguvu kazi yenye afya ndiyo inaweza ikafanya mambo mengine yote. Kwa hiyo, naomba pia bajeti yetu ijikite pia katika *universal health coverage*, bila kusahau *primary health care*. Ni maeneo hayo ambayo tunaambiwa watu wetu wanakuwa kwa sababu ya kukosa afya na pia tunakwenda kwenye umaskini mkubwa kwa sababu ya gharama kubwa za afya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hayo tuyaaangalie kwa namna ya pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo naomba nigosie suala la reli, natoka Katavi, Mpanda, nilikuwa naomba na wazungumzaji wengine wameongea hapa, shirika hili bado linafanya mambo yake kizamani. Kwa mfano kule nyumbani, unaambiwa kwamba wateja ni wengi, mabehewa hayatoshi, hawaoni kwamba hilo ni soko, ni fursa ya kuchangamkia, kwamba kama wateja ni wengi, mabehewa machache, dawa ni kuongeza mabehewa, lakini utashangaa wamelalamika leo, wamelalamika kesho, watalalamika kesho kutwa, hatua hazichukuliwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama shirika linaona nivizuri kutofanya kwa, maana yake hata mashirika mengine, kwa mfano, mashirika ya ndege, hapa tumeona ikionekana wateja ni wengi Dodoma, wanaweza wakaongeza hata *trip* ya pilii, zikaja hata ndege mbili kwa wakati mmoja. Sasa kwa nini hawa hawaangalii katika sura ya kibiashara? Nilikuwa naomba hilo waliangalie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, eneo la kilimo, ni kweli na nakubali, tuseme yote tutakayoweza, bila kilimo, liko tatizo, lakini kilimo pekee cha kutufuta machozi ni kilimo cha umwagiliaji. Uzuri wa kilimo cha umwagiliaji, kwanza, wewe unakuwa na nafasi ya kuki-control,maji kidogo, maji zaidi na mwanga unakuwepo, lakini hiki kilimo cha kutegemea mvua za Mwenyezi Mungu, mara mafuriko na vitu vingine vyta namna hiyo. Kwa hiyo, tukijikita kwenye kilimo cha umwagiliaji, tukichanganya na hicho kingine cha kutegemea msaada wa Mwenyezi Mungu, tuna uwezo wa kuifanya nchi yetu ikawa ghala la chakula na kukasaidia watu wengine katika maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, suala la diplomasia ya uchumi, ndiyo maana tuna mabalozi nje ya nchi, tuna watu wengine wa namna hiyo. Inasikitisha kusikia ukilliona chungwa zuri, kama ni parachichi zuri, ni kwamba lilizalishwa Tanzania, limekwenda huko, halafu likapewa *label* ya nchi nyiningine, mabalozi wetu wako wapi! Suala zima la diplomasia ya uchumi iko wapi katika kuinusuru nchi katika mambo hayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na inasikitisha pia, ni kweli, hata mimi mara ya mwisho nilivyokuwa huko Canada nilisikia mtu mmoja akizungumza kabisa, kwa maana ya Mlima Kilimanjaro uko nchini kwao. Hasa mimi niendelee kusema, haya yote, kama mwenzako anafanya hivyo kwa *ku-take advantage* ya wewe, si na sisi tuna nafasi ya kulifanya hilo pia! Kwa hiyo, eneo hilo nilikuwanaomba sana, naomba sana tuliangalie katika sura hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la umeme ni kweli, nashukuru kasi inayoendelea, lakini kwa maeneo mengine kwa mfano hata kule kwangu Katavi, kasi si ile, najua hili Mheshimiwa Waziri husika atasikia pia kwa kupitia wewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, naomba niingie ene la madini, mara ya mwisho nilizungumza hapa, mimi ni mdau wa shughuli za uchimbaji madini, napata ugali

wangu wa siku kwa kupitia uchimbaji wa madini. Nilikuwa naomba niishauri nchi yangu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, pamoja na kuambiwa mchango wa uuzaaji dhahabu nje ya nchi umeongezeka kwa asilimia 0.7, tuache maeneo mengine ya utalii, fukwe na mambo mengine ya namna hiyo. Mimi naomba nijikite kwenye madini tu, tuna uwezo wa kuitoa nchi hii hapo ilipo ikaenda mbali zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokutana na Mheshimiwa Rais, kwanza chukulia niseme, kwa maana ya idadi ya wachimbaji, nichukulie hata kwa idadi kidogo ya 6,000, nitaje tu au milioni sita tufanye. Hebu chukulia kila huyo mmoja, akazalisha kilo moja tu ya dhahabu, ni *grams* ngapi, kilo ngapi za dhahabu zitapatikana katika nchi hii, lakini mambo ambayo tunatakiwa tuyafanye, mimi niseme nashukuru kwa hatua ambazo Serikali imeanza nazo, lakini tunatakiwa twende mbali zaidi! Tusifunge milango, tutoe nafasi, kwa mfano, kuna nchi hazina madini, lakini wazalishaji wazuri wa madini na wanaauza nje ya nchi. Tujilize wanafanyaje watu hawa! Kwa nini tusiige? Sisi kama nchi, kwanza madini tunayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme kwa mfano, leo pamoja na sheria hizi nyingine ambazo tunaziweka, bado wenzetu wa utafiti hawajafanya utafiti wa kutosha na ndiyo maana unaweza ukakuta ukilala, ukiamkia unasikia kuna *gold rush somewhere*, mtu alikuwa amekwenda tu kwa ajili ya kuchimba viazi, anaondoka na kipande cha dhahabu, mtu alikuwa ameenda kwa ajili ya kuchimba kisima, anaondoka na kipade cha dhahabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutengeneze sheria rafiki ambapo, kwa mfano, mimi nimekwenda peke yangu porini, nikakutana na kipande cha dhahabu cha size ya kiatu, wewe haupo, polisi hayupo, mwingine hayupo, unategemea mimi nifanyeje!

MBUNGE FULANI: Naondoka nacho.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: ...ndiyo maana katika mazingira hayo, tukitengeneza mazingira rafiki, mtu huyu awe tayari ku...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa, kengele ya pili ilishagonga.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Masoud Abdallah, kabla ya Mheshimiwa Frank Mwakajoka, kwa hiyo, atachangia kwanza Mheshimiwa Masoud Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nichukue fursa ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanah Wataalah* anijalie uzima na afya njema, kuchangia bajeti ya mwaka 2019/2020 na nianze na Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake katika ukurasa wa 95 akisema kuelekea uchaguzi za Serikali za Mitaa, mwaka huu Oktoba, 2019. Akataja sifa 10 na kuna baadhi ya sifa ambayo moja ilikuwa kidogo na ukakasi na Spika akarekebisha, labda niseme kuna baadhi ya sifa ambazo uliziacha, naomba nikukumbushe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganini mwa sifa ambazo tunataka kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuwachagua viongozi wanaofaa, awe anathamini utu wa binadamu, mionganini mwa atakayechaguliwa, lakini pia awe anatoka katika chama ambacho hakina tabia ya watendaji wake kuzikimbia fomu za wagombea wengine wanapopata fursa, akaingia mitini, hiyo ni sifa nyingine ambayo ya kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sifa nyingine ambayo itakuwa ni nzuri kuliko yote, awe anatoka katika chama ambacho kinakubali kushinda, chama ambacho anakubali kushindwa pale ambapo anaposhindwa, asiwe na tabia ya kung'ang'ania na kuandaa mazingira ya amani kutoweza, akishindwa akubali kushindwa, hizo ni sifa ambazo Mheshimiwa Mpango uliziacha. Tunaomba ukija hapa uzingize sifa hizo, kwamba tunataka uchaguzi Serikali za Mitaa, sifa hizo kuzitaja uliziacha, naomba uzikubali na ninafikiri kwa unavyocheka, sifa hizi umezikubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na bajeti sasa; bajeti hii ya mwaka huu haina uhalisia, bajeti hii ya mwaka huu inaonekana mnakwenda kutumia fedha nyingi zaidi kutokana na mchanganuo ambao umeleta, mapato/ makusanyo ya muda wa miaka miwili, tunakwenda kutumia ndani ya mwaka mmoja, yaani ukusanye fedha za miaka miwili, ambayo makusanyo yetu kwa mwaka ni triliioni 1.2, makusanyo yetu ni triliioni 1.2 kwa mwezi, lakini kwa jinsi ambavyo umetuletea matumizi yako, tunakwenda kutumia trioni 2.5 kwa mwezi, kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni lako la Taifa unasemani triliioni 9.7; ukiangalia mchananuo kama utagawa kwa mwezi, utakuta kwamba ni lazima upate bilioni 810. Ukienda kwenye mishahara triliioni 7.558; ukiangalia je, kwa mwezi utakuta kwamba unapata bilioni 629. Ukienda kwenye matumizi mengineyo (*OC*) triliioni 3.576; ukienda kwa mwezi utakuta kwamba kuna bilioni 298; ukienda kwenye fedha za maendeleo, ukiachia fedha za wahisani zile, triliioni mbili pointi; triliioni 9.73, nazo lazima ukusanye upate bilioni 811, hizo ni triliioni 2.5! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unashangaa leo Waziri unakuja na bajeti ya matumizi ya triliioni 2.5 zipatikane, lakini unasema na makusanyo yetu sisi ni triliioni 1.2, kwa mwezi! Hiyo ni bajeti ya kiini macho, kizungu mkuti, haifahamiki, funika kombe! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, tunataka bajeti ya uhalisia, siyo bajeti hii, hii bajeti haltekelezeki, tunakwenda kuumiza watanzania. Mimi halafu nashangaa, namshangaa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwamba hii bajeti, kweli haitoi jibu! Haitoi jibu kwa sababu gani, inaelekea moja kwa moja, utaratibu unaonekana, hata wafanyabishara wenyewe, kilio kila kona, maduka Kariakoo yamefungwa, uvuvi bahari kuu hauna jibu, hamkujipanga, ni kivutio kikubwa, lakini kila tukitoa ushauri kwetu sisi, mama ntilie nako ni kilio. Sasa hii ni bajeti ya aina gani mwaka huu! Bajeti hii ni kiini macho, kizungumkuti, haifahamiki. Naomba huwezi kuchukua trillioni 2.5 ambayo lazima uzipate, lakini makusanyo yako ni trillioni 1.2. nimshauri Mheshimiwa Waziri, bajeti hii ifumiliwe upya, haifai kabisaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, suala la wakulima; wakulima wamekuwa na malalamiko makubwa kila wakati. Suala la korosho limekuwa ni kubwa, mmeweza, mmechukua muda mrefu, wakulima wa korosho wanalamika, mara hii mmekwenda kuweza kuwakopa wakulima wa korosho, hamjawalipa, mmewalipa baadhi ya wakulima, baadhi ya wakulima wengine hamjawalipa na nini athari yake hii, athari yake wanashindwa kuandaa mashamba. Kama Serikali ni ya wanyonge, walipeni wanyonge wa korosho! Hata hawa wafanyakazi wa ngazi ya kat, walipeni fedha zao! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa sana, lakini kama mkiendelea kutowalipa fedha zao za korosho, basi kinachoonekana, morali inashuka, morali kwa wakulima wa korosho inashuka kila siku! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa mimi nawashangaa, mnasema Serikali hii ni ya wanyonge, wakulima, lakini nashangaa kwa nini hamsikii kilio tunacholia, Halmashauri zinakosa mapato!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri andaa mazingira, andaa mazingira kwamba ni jinsi gani mtaweza kulipa wakulima wa korosho na taarifa ambazo zipo, ambazo bado hazijathibitishwa, mna mpango wa kwenda kuwalipa

wakulima wa korosho kwenye mwezi wa nane na wa tisa, kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa iwe kama ni kampeni. Ndiyo taarifa zilizopo zinazozagaa, ni kawaida yenu hamuwalipi, mpaka karibu karibu ama kuna uchaguzi fulani ndiyo mnafanya ujanja ujanja, mnakwenda kuwalipa na amesema Mheshimiwa Bwege, mkiwalipa mtapigwa, hamkuwalipa mtapigwa. Kwa sababu wao wana macho wanajua wapi wanachagua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kwenye miradi ya maendeleo; kwenye miradi ya maendeleo, taarifa ya miradi ya maendeleo, kwa upande za Zanzibar. Kitabu kile hakionyeshio kabisa jinsi gani ambavyo mnakwenda kutekeleza miradi ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar, ni eneo dogo sana ambapo mmetaja. Ni sehemu moja tu ya ulinzi, kidogo tu, lakini kuna Mradi wa Mpigaduru kabisa hamkuutaja, kuna miradi kadhaa mlkwishaahidi zamani, kuna Bandari ya Wete, Bandari ya Mkoani, mliahidhi. Sasa nimshauri Mheshimiwa Waziri, katika miradi yote 552, lakini ukiachia miradi ile ambayo iko katika mambo ya Muungano, hata miradi ambayo ipo katika Ofisi ya Makamu wa Rais, mabadiliko ya tabianchi, mnakwenda kujenga kuta katika fukwe, hamkutaja hata mradi mmoja kutoka Zanzibar, kwa upande wa Unguja na Pemba, hili ni jambo ambalo linatumiza kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa, na Mheshimiwa Waziri January Makamba, wewe unafahamu jinsi tatizo la fukwe, wewe umefika Kisiwa Panza na maeneo mengine, kwa nini katika kitabu kile hamkuonesha utaratibu wa kwenda kujenga kuta katika fukwe katika mabadiliko ya tabianchi, mmewatenga Wazanzibari, hili lazima tuliseme, tatizo nini? Niwashauri mara nyingine mtakapoandaa taarifa, basi Zanzibar muweze kuihusisha vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo lingine ni hali ya uchumi unavyoendelea; katika hali ya uchumi unavyoendelea, kumekuwa na aina fulani ambayo inaonekana wazi wazi kwamba ni kwanini baadhi ya benki zinafungwa! Serikali imekaa tu, kuna benki ambazo

zimefungwa, unaifuata benki, imefungwa, kuna *Kagera Farmer Cooperative Bank*,imefungwa, Benki ya Wakulima imefungwa, lakini hata Benki ya Wanawake, nayo imefungwa! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sababu zipi za msingi ambazo zinaonekana kwamba kuna kuwa na m dororo huu wa uchumi! Moja ya sababu inaonekana Benki ya Wanawake kufungwa, taarifa ambazo tunazo ni kwamba Serikali iliahidi kuboresha Benki hii ya Wanawake, lakini fedha hamkupeleka! Sasa kwa nini msipeleke fedha na mnasema kwamba wanawake kwanza, tunawajali mama zetu, hawa ni wazee wetu, kwa nini basi mlipelekea mpaka Benki hizi, Benki hii ya Wanawake kufungwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Masoud, kwa hiyo hawezi kupewa tena taarifa maana muda wake umekwisha.

Mheshimiwa Amina Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Jaku Ayoub ajiandae.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Serikali kwa mwaka huu wa 2019/2020. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa vyote kwa kutuwezesha hatimae kuwa salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali na ninampongeza Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Mpango kwa mipango thabiti kutuletea bajeti hii ambayo ni bajeti ya wananchi. Nikupongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Ashatu Kijiji kwa ushauri mzuri ambao kwa pamoja na watumishi wote, Katibu Mkuu na pamoja na wafanyakazi

wote wa Wizara ya Fedha kwa ujumla kwa kweli kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Nampongeza kwa kiasi kikubwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa kwa moyo na uzalendo wake ambaa ameweza basi kuita watu mbalimbali na kufanya ikulu kuwa kweli ikulu ya wananchi na hasa kwa wafanyabiashara ambaa tumeona ni kwa kiasi gani wameweza kueleza changamoto mbalimbali zitakazoisaidia Serikali, nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza kama kiongozi wetu Bungeni, lakin pia kwa mipango thabiti ambayo kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli bajeti hii na hasa kilimo-biashara nina imani kabisa kwamba kazi inayofanywa kupitia Wizara ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemau basi tutaweza killimo kitakachofanywa na vijana pamoja na Wannachi wengine basi kitakwenda malighafi zile kutumika kwenye viwanda.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana na pia Katibu Mkuu na dada yangu Jenista Mhagama hongereni sana, pacha wangu pia Stella Ikupa ninakupongeza sana kwa ushauri mzuri unaompatia Waziri hatimae basi hata yale masuala ya watu wenye ulemau kwa kweli jitihada zako tunazona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia katika sekta ya viwanda; tunafahamu kwamba ajenda ya nchi hivi sasa ni viwanda na ili viwanda iweze kufanikiwa hapandipo tunapouona uwezo na nafasi kubwa ya Mheshimiwa Rais wetu kutohana na jitihada anazofanya basi tutaelekea uchumi wa kati kwa mwaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufanikiwa kwenye viwanda ni lazima tuzingatie uwepo wa malighafi na hizo malighafi viwanda vyetu vitakuwa na faida kubwa endapo malighafi hizo zitatumika za hapa hapa nchini na tunaona katika bajeti hii wameeleza kwamba malighafi zaidi zitakazotumika ni kutoka hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na mipango hii ya Mheshimiwa Mpango, Serikali tunaona kabsia kwamba ujenzi wa umeme wa *Stiegler's* pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, lakini pia ujenzi wa barabara vyote hivi vitasaidia kwa sababu mkulima atakaelima mazao yake, reli itakapokamilika ni dhahiri kabisa anaweza kufika katika soko la Kariakoo kwa muda mfupi ambapo atakwenda kuuza mazao yake, lakini wale wa vijiji pia ujenzi wa barabara ambako hivi sasa tumeunganishwa maeneo mengi bado Mkoa mmoja tu wa Kigoma na jitihada bado muda mfupi tu hatimae zile kilometa 300 zitakwisha, ninaamini kabisa dhamira hii ya Serikali ndiyo ambayo itakayotufikisha katika uchumi wa kati mwaka 2025. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kiwanda kiweze kufanikiwa ni lazima basi hizo malighafi kama nilivyoeleza, lakini je, katika hizi malighafi Serikali inajipanga vipli kuhakikisha kwamba upatikanaji wake, kilimo hiki kitakuwa ni kilimo chenye tija. Kwa mfano, katika kilimo cha sasa tunaona kabisa kwamba mabadiliko ya tabianchi ni tatizo pia. Katika haya mabadiliko ya tabianchi ni dhahiri kabisa kwamba mvua hizi ambazo tunategemea za msimu basi kama Serikali isipojipanga hatutaweza kufanikisha kwa zaidi, lakini ndipo hapo basi nikasema kwamba Ofisi hii ya Waziri Mkuu na hasa kuititia kilimo cha kisasa ambacho Serikali imejipanga ni dhahiri kabisa malighafi hizi zitakwenda kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mizuri kuititia kilimo cha kitalu nyumba ambacho ninaamini kabisa, kwa mfano, malighafi ambazo zitahitajika kwenye viwanda vya kutengeneza *tomato sauce*, nyanya zitapatikana kwa wingi lakini siyo hiyo na vingine vingi vitapatikana. Lakini tatizo kubwa ninaloliona na hapa napenda kuishauri Serikali yangu tukufu kwamba kuzingatia kwa mfano, malighafi ya ngozi hatuna wataalam wazuri wa kuweza ku-process hizo ngozi na hapa ndipo tunapoona umuhimu wa vyuo vya ufundi kama *VETA* kuona ni kwa jinsi gani vitawafundisha vijana wetu ili basi waweze kuajiriwa kwenye viwanda ambavyo ngozi zinapatikana kwa wingi hapa nchini kufanya basi kazi hiyo na hizo ngozi hata kama zitasafirishwa zisafirishwe zikiwa tayari

zimekwishaongezewa thamani kwa ule utaratibu wa kuweza kushughulikia hizo ngozi. (*Makofi*)

Mheshimo iwa Naibu Spika, lakinia malighafi nyingi vifungashio bado mni shida. Tunaona kwamba vifungashio vingi bado tunaagiza kwa nchi jirani na hasa wenzetu wa Kenya. Tunawaandaaje vijana wetu na hasa Chuo cha VETA kuona kwamba ni kwa jinsi gani kwa kushirikiana na SIDO ili basi waweze kuboresha zaidi vifungashio katika malighafi zitakazotengenezwa hapa nchini na kwa kutumia viwanda vyetu ili basi tuweze kila jambo liweze kufanyika hapa nchi tusafirishetiki na ubora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinia tunapozungumzia kwamba kilimo, kilimo hiki bado kina changamoto nyingi. Ninaiomba sana Serikali mbali ya kusema kwamba tutawashirikisha zaldii vijana katika Halmashauri zetu tuone tunawasaidiaje hasa wanawake kwasababu asilimia 80 ya wanawake ndiyo wanaofanyakazi zaidi na hasa kule mashambani. Mikopo ikiwepo na kuwawezesha Wanawake waweze kujilingiza kwenye kilimo chenye tija, basi ni dhahiri kabisa kwamba malighafi hizo zitaweza kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa utaratibu ambao sasa wameona ni vyema uamuzi wake wa kuwa na kitengo ambacho kitasikiliza kero mbalimbali za watu ambao kwa namna moja au nyingine wanashughulikiwa na TRA na hii itaweza kusaidia sana kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ukweli kutoka moyoni mwangu, TRA wametukwamisha na hapo ndipo ambapo tunaiomba kwa kweli Serikali iweze kuwabaini hawa baadhi ya watumishi wa TRA wasio waaminifu ambao wametufikisha hapa na ikibidi kwa kweli sheria ichukue mkondo wake kwa sababu hawa ni wahujumu uchumi. Tumesikia kero mbalimbali za wafanyabiashara ambazo zimedhihirisha, zimeeleza wazi, wakishughulikiwa hawa ninaamini kabisa nidhamu itakuwepo na kwa nini tusichukue hata ikibidi wakati mwingine kuweka jeshi mfano, kule

bandarini tukaweka jeshi ambalo litaweza kusimamia kwa ukamilifu kwa kushirikiana na wafanyakazi wa *TRA* mapato yakaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni soko la Kariakoo; tumeona ni kwa jinsi gani ambavyo wengine wameweza kuzungumzia soko hili la Kariakoo. Kilikuwa ni kitovu cha biashara, lakini leo hii siyo ile Kariakoo ya awali, wanasema kujikwaa ndipo ambapo unanyanya na kuangalia ni kitu gani kimesababisha wewe uanguke, kwa maana hiyo ninashauri sana Serikali kuona ni kwa jinsi gani tunairudisha Kariakoo, ile Kariakoo ya zamani ambayo ilikuwa ni kitovu cha biashara na hatimae wananchi turudishe imani kwa nchi ambazo zilikuwa zinakuja kununua biadhaa mbalimbali hapa nchini. Kwa mfano Uganda, sasa hivi wafanyabiashara wengi kwa kweli wanakwenda Uganda kwa ajili ya kununua malighafi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho kabisa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga hoja mkono, ninashukuru sana, naitakia kila la heri Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Frank Mwakajoka atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Ayoub, Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi niweze kuchangia bajeti hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kwanza kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya

Upinzani, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Kivuli kwa jinsi ambavyo ameandaa bajeti vizuri, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Chama Taifa, Kamanda wa anga ambaye kwa kweli ni kiongozi imara anayesababisha tufanyakazi vizuri na Watanzania waweze kutuamini na chama hiki kinaaminika kweli kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimekaa hapa nasikiliza michango mbalimbali ya wenzetu watu wa CCM na nilikuwa namsikia pia Mheshimiwa Amina Mollel hapa anazungumza kuhusiana na ukusanyaji wa mapato, anasema kwamba tungepeleka jeshi yaani mpaka leo Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Wabunge wake hawaelewi kwamba masuala ya fedha ni taaluma yaani wanaona jeshi pake yake tu kutumia nguvu, ndiyo kitu pekee ambacho kinaweza kikakusanya mapato katika Taifa hili yaani hapo ndipo milipofikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa nataka kuzungumzia jambo lingine; watu wengi wanasema sisi tunakataa *Stiegler's Gorge*, tunakataa *standard gauge* huu ni mtazamo wa hovyo kabisa. Sisi hata siku moja hatujakataa *standard gauge*, sisi hata siku moja hatujakataa *Stiegler's Gorge*, tulichokuwa tunasema sisi hapa tulikuwa tunatoa ushauri kutokana na matumizi makubwa ambayo yanakwenda kwenye miradi mikubwa miwili badala ya kuwahudumia Watanzania walio wengi, hicho ndicho ambacho tulikuwa tunajaribu kukizungumzia na siku zote tunaposema kwamba Serikali hii inakwenda kufanya shughuli za vitu, inaweka bajeti ya vitu badala ya bajeti inayowahusu wananchi tulikuwa tunamaanisha. Tunajaribu kuangalia ni namna gani bajeti zingine ambazo zimepewa fedha kidogo na hata hizo fedha kidogo ambazo zinakwenda kule hazipelekwi kabisa au zinapelekwa kidogo sana na ndiyo maana tunasema kwamba ni lazima mfike mahali mkubali. Tatizo kubwa CCM mnachokifiki ni kwamba vyote tunavyoviongea kama uoinzani ndani ya Bunge hili mnaona kama sisi tunapinga kila kitu na kwa sababu ya kiburi mlichonacho ndani ya mioyo yenu hamuwezi kutekeleza ule

ushauri ambao tunawapa, mnaendelea kubeza, lakini kesho mnarudi mnaanza kufanya hayo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais juzi amewaita wafanyabiashara Dar es Salaam, tuliyyozungumza mwaka 2016/2017 amekwenda kuyazungumza Mheshimiwa Rais hayo hayo na amefanya mabadiliko. Leo Mheshimiwa Mpango tulichozungumza kwamba mnaleta sheria ambazo ni kero kwa wafanyabiashara zitakazosababisha wafanyabiashara wasifanye biashara mka sema hapana hizi ndiyo sheria nzuri, leo Mheshimiwa Mpango karibu kodi 54 anakwenda kuziondoa. Sasa yote tuliyyazungumza yaani mpaka muue biashara mpaka mhakikishe kwamba biashara zinakwenda vibaya ndiyo mrudi nyuma muanze kufikiri kwamba sasa tumekosea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunaona sisi ni macho ambayo yanaona kila siku tunafanyakazi ya kuchanbua ni namna gani mambo yanavyokwenda...

MHE. AMINA S. MOLLEL: Taarifa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: ...tofauti na ninyi mnakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi...

MBUNGE FULANI: Tulieni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Frank Mwakajoka kuna taarifa. Mhehsimiwa Amina Mollel

TAARIFA

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Naomba nimpe taarifa mchangiaji anayezungumza kwamba anaposema waliishauri Serikali na hatimae leo hii ndiyo yanachukuliwa, naomba tu nimkumbushe kwamba

katika Bunge liliopita waliishauri sana Serikali kuhusiana na masuala ya madini na hatimae Serikali ikaonesha usikivu na ikaleta sheria hizo, lakini wale wale waliokuwa wanashauri hatimae ndio hao hao waliokuja kupinga sheria hiyo. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Frank Mwakajoka unaipokea taarifa hiyo?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ambayo anayafanya Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anatoa taarifa yaani hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo mnandelea kuwa dhaifu sisi kazi yetu ni kushauri na kama hamsikii mtaendelea kufanya hivyo na hamtaweza kupiga hatua na hamtaweza kufanya chochote kwa sababu hamuwezi mkasikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bunge la mwaka 2017/2018 tulizungumzia hapa, ilikuja taarifa hapa kwamba tunataka sasa fedha zote za Taasisi za Serikali ziondoke kwenye benki za kibashara ziweze kwenda *BOT*. Jambo hili tulilishauri sana na tukasema yaani sababu ni nini? Sababu waliyooita wakasema kwamba mabenki yanapata sana faida, lakini tukashangaa sana kwamba kazi ya benki za b Bashara katika nchi hii kazi yake zinaisaidia Serikali kuwakopesha wajasriamali wadogo wadogo na wafanyabiashara wakubwa kuhakikishawkamba wanafanya biashara na wanapata mitaji. Sasa mkapeleka hizo fedha *BOT* na sasa hivi hizo fedha zimekaa kule na *BOT* haikopeshi wajasriamali na benki imeshindwa kukopesha wafanya biashara wadogo wadogo na wajasriamali kwa hiyo mambo hayaendi. Yote haya najua baada ya mwaka huu mtakuja kesho kutwa mtaiondoa na kwasababu ndio kawaida yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nia yangu kubwa nilikuwa nataka kuzungumzia sana kwenye kilimo; lengo kubwa la Serikali wanasesha ni Serikali ya wanyonge na imekuja kuondoa umaskini kwa wanyonge, lakini nataka kuuliza wanyonge ni watu wa namna gani? Unapozungumzia

wakulima, wafugaji na wavuvi unazungumzia asilimia 65 mpaka 75 ya Watanzania wote. Kundi hili la Watanzania ambalo ni kubwa kabisa leo limesahaulika kabisa katika bajeti ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi hasa Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikukumbushe; mwaka 2016/2017 tulitenga fedha, tulipitisha fedha hapa shilingi bilioni 101; kati ya shilingi bilioni 101 fedha iliyokwenda kufanyakazi ya maendeleo kwenye kilimo ilipelekwa shilingi bilioni mbili peke yake, lakini mwaka 2017/2018 tulitenga fedha hapa shilingi bilioni 150 fedha iliyokwenda kufanyakazi ya kilimo ilipelekwa shilingi bilioni 16 peke yake, lakini mwaka jana tumetenga pia fedha imekwenda kupelekwa karibuni shilingi bilioni 46 peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo nashangaa na nasema kwamba jambo hili halihitaji hata kuwa profesa wala halihitaji kuwa daktari. Nazungumza hivi kwa sababu Watanzania asilimia 65 mpaka 75 tafsiri yake ni kwamba ndiyo wanunuzi wakubwa katika Taifa hili na ndiyo walipa kodi wakubwa. Ukitaka kujua kwa nini biashara zime-stuck katika mwaka 2018/2019 ni kwa sababu wakulima na wafanyabiashara wa mazao walishindwa kuuza mazao yao baada ya kukosa soko na ndiyo maana biashara zote zilisimama. Kwa hiyo, unapozungumzia biashara lazima uzungumzie kundi la watu asilimia 75 la wakulima, wafugaji na wavuvi. Usipozungumzia kundi hili ujue kabisa wanunuzi hawatakuwepo katika nchi hii kwa sababu wakikosa kipato hata wafanyabiashara wa maduka wanaofanya biashara za viwandani hawataweza kuuza kwa sababu watu wanaotegemewa sana ni wakulima, wafugaji na wavuvi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie mchango wa sekta ya kilimo katika nchi hii ni mkubwa sana. Ukienda kuangalia kwenye suala la ajira karibuni asilimia 65 ya Watanzania wote wanajajiri katika kilimo, ufugaji na uvuvi, lakini ukienda kwenye chakula karibuni asilimia 100 tunapata chakula kutokana na hao wakulima ambao ni wananchi

waliojajiri kwenye kilimo. Lakini ukienda pia kwenye pato la Taifa inachangia karibu asilimia 28 mpaka 30 lakini bado uwekezaji kwenye kilimo kwenye Serikali ya Awamu ya Tano iko chini ya asilimia mbili, sasa tusitegemee viwanda kwa sababu asilimia 65 ya malighafi ya viwandani yanategemea kilimo na kama yanategemea mazao ya kilimo tafsiri yake ni kwamba kama hatutawekeza kwenye kilimo tusitegemee kupata viwanda katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo mnasema kwamba hii ni Serikali ya viwanda halafu hamuwekezi kwenye viwanda mnapeleka kwenda kununua ndege, mnakwenda kujenga *Stiegler's Gorge*, mnakwenda kujenga *standard gauge* na manatumbia kwamba hii ni Serikali ya viwanda, hivyo viwanda vitakuja kwa namna gani? Kwa hiyo ni lazima tuhakikishe kwamba tunainua kilimo na ninataka kutoa mfano, kwamba Serikali hii kwa kweli imeshindwa kabisa kuhakikisha wkamba inawasaidia Watanzania wanyonge ambao ni wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004/2005 katika bajeti ya kipindi hicho yaani uwekezaji ulikuwa ni asilimia 4.7 ya bajeti yote; mwaka 2005/2006 ilikuwa aislimia 5.8 ya bajeti yote; mwaka 2006/2007 ilikuwa aislimia 5.8 na pia mwaka 2009/2010 ilikuwa asilimia 8.6 na walitenga fedha karibu shilingi bilioni 666.9; leo mnatenga shilingi bilioni 208 miaka mingapi imepita mnatenga shilingi bilioni 208 mnasema mnakwenda kuinua kilimo na mtapata viwanda katika Taifa hili, mnajidanganya. Ni lazima tufanye mageuzi ya kilimo kwanza ndiyo tutakwenda kwenye viwanda na kama mnaota viwanda wakati hamjafanya mageuzi ya kilimo mnajidanganya na Serikali yenu itakuwa ni Serikali ambayo inazungumza uongo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na uksoma llani ya Chama cha Mapinduzi utaona kabisa walikuwa wamekubalina kwamba ni lazima wawekeze kwenye kilimo, watainua kilimo kwa asilimia nane ndani ya miaka mitano, lakini leo kilimo hakijainuka na kilimo hapa kimekua kwa asilimia 5.3 peke yake. Sasa kwa hiyo mmewadanganya wananchi ambao

mlikwenda kuuza llani yenu illi mchaguliwe na mwongoze Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye llani yenu katika kifungu cha 27(n) mlisema kwamba mtanunua meli tano za uvuvi ilii kuhakikisha kwamba mnawainua wavuvi lakini pia mnahakikisha kwamba kinachangia pato la Taifa kwenye upande wa uvuvi. Lakini nakwambia mpaka sasa hakuna meli hata moja wala boti iliyonunuliwa kwenye bahari ya Hindi kwa ajili ya uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ilikuwa ni kwamba mnatengeneza na kwenda kuuza sera zenu kwa wananchi lakini hazitekelezeki. Kwa hiyo, sisi tunasema kwamba tunawakumbusha Watanzania waelewe kwamba yanayozungumzwa kwenye majukwaa, yaliyowekwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi hayatekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie tu ukweli Watanzania sio watu wajinga, leo wakulima wako kijiji wanalima kule, wanakosa masoko na hata wakipata masoko wanatafuta masoko yao tunakwenda kuzuia mipaka mnasema wasiondoke. Juzi Salum Sumri kule Sumbawanga aliamua kuacha mabasi akasema ngoja ajikite kwenye kilimo akagharamia vitu vingi sana kwa ajili ya kilimo, lakini cha kushangaza baada ya kugharamia haya amekwenda kulima amepata karibuni tani 47,000 lakini ameshindwa kuuza hayo mahindi yake yako ndani mpaka sasa hivi alipata soko Congo mkazuia mkasema asiende kuuza mkasema mtakula mahindi yote haya mnakulaje mahindi tani 40 na ngapi wakati fedha hamna za kununulia mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. GODWIN A. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imehagonga Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, huwa tunakumbushana mara nyingi, humu ndani kwa asilimia CCM wako kwa asilimia 72, wakiamua kuzomea CCM upande huu sijui kama kuna mtu atazungumza. Kwa hiyo, tuheshimiane anapozungumza mtu msikilize kama ambavyo ninyi mkisimama mnasikilizwa, sikilizeni wenzeni pia. Watu wote lazima tuheshimiane ndio maana kila mtu anaposimama anaita mwenzake Mheshimiwa, huo ndio utaratibu wa humu ndani. (*Makof!*)

Mheshimiwa sijampa yule taarifa kwa sababu muda wako umekwisha, kengele ya pili ilishagonga.

Waheshimiwa nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Jaku Ayoub atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Bobali ajiandae. (*Makof!*)

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza na mimi kukushukuru kuniruhusu kuchangia mjadala huu ambao ni muhimu na ndio afya ya Serikali yetu, bila ya fedha huwezi kufanya kitu. Nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake pamoja na Katibu Mkuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mchango wangu kwa Serikali zetu hizi mbili ni sikivu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bila kupoteza muda nianze na *TRA*, kwa kweli siku zote Mheshimiwa Rais kama hatukujipanga watendaji wa *TRA* nafikiri mko ndani mnasikiliza mchango huu, siku zote atabadilishwa Kamishina, itakuwa kama kubadilisha shati siku zote. Hapa pana uwajibikaji na utendaji, siku zote suala hili lina kazi. *TRA* mmekuwa midomoni mwa watu/wafanyabiashara sana lakini niwaombe panapo haki ya mtu jaribuni kuangalia haki ya mtu, tusifikie *TRA* kutumia nguvu za ziada kumlazimisha mtu, kuku anataga yai moja huwezi kumlazimisha kutaga mayai matatu utamkosa mpaka yule kuku, kwa hiyo hili mliangalie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Murad alizungumza sana kuhusu Kariakoo, sasa hivi haipo limebakii jina tu, kutengeneza jina kuna kazi kuchafua ni mara moja. Kwa hali ya Kariakoo haipo, kurejesha kuna kazi sasa hivi, wafanyabiashara wengi washafunga virago kutafuta maslahi kwengine. Hili mkae na mliangalie *TRA*, hali si nzuri, kodi hizi zinakusanywa kwa viwango vyake na utendaji wake, tusatike kumuonea mtu wakati hana hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wengine wanalazimishwa wasaini kabla hajaja kupelekwa mahakamani, kosa halijulikani, kuna mtu ana kesi ya mwaka 2010 mpaka leo, sheria ya *TRA* inasemaje miaka mingapi kufunga *file*?Tusifufue maiti wakati ilishaiza, hatuwezi kufika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu kubwa kuhusu Zanzibar kukopa hapa tutapiga kelele mpaka dakika ya mwisho Waheshimiwa Wabunge hasa kwa upande wetu wa Zanzibar. Kuna sheria ambayo ilipitishwa naomba kuinukuu ya tarehe 03 Machi, 2017; *The Written Law Miscellaneous Amendment Act 2017*; hii sheria kama Mwanasheria Mkuu yupo naomba akaialangalie haiko vizuri sana. Nasema kwa sababu zangu ninazozijua pamoja na kuwa na elimu yangu ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *amendment section two* “*The principal Act is amended in section 2, by (a) adding appropriate alphabetical order the following of definitions:*

“*Consolidated Fund*” means *Consolidated Fund of Government* referred to in the Constitution;

“*On-lending*” means an arrangement whereby the Government borrows from the external or domestic source and thereafter passes on the loan of another entity such as Revolutionary Government of Zanzibar, parastatal organizations, local Government of any other public body corporate.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sheria haiko vizuri kwa maslahi ya Zanzibar na imepitishwa hapa sijui tulikuwa wapi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii tuliangalie, maana yake kwa haraka SMT inaweza ikakopa SMZ kama ni mashirika au halmashauri za mjini kukopeshwa, kwa hiyo ile ndoto yetu ya Mpigaduri pana kazi kubwa sana, tuwe wa kweli wajumbe hii angalieni sheria hii ikoje? Mimi elimu yangu ni ndogo. Kwa hiyo, mkopo ule kujenga bandari ile pana kazi kubwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi nakwenda tena mbele; *The principal Act is amended by repealing section 12 and replacing for it the following; Revolutionary Government of Zanzibar may, where arrangement between the Government and the lender requires on-lending arrangement enter into on-lending arrangement with...*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili; *on-lending arrangement under subsection (1) shall be effected through on-lending agreement which shall, amongst other things, contain the terms and conditions of the primary kuna high and equally.* Hii sheria bado ina kazi kubwa, vinginevyo tutapata matatizo sana Serikali ya Mapinduzi kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda hautoshi lakini hii sheria ina mambo mengi huko mbele angekuwepo Mwanasheria Mkuu hapa ningemkabidhi hii ingekuwa vizuri, lakini huko mbele ina marekebisho mengine, lakini nitakuletea copy moja ili uione kuna nyingine za *Government, Loans, Guarantees and Grants Amendment Act* ya mwaka 2003 nayo haiko vizuri kama nitarhusiwa kuja na hoja binafsi nitakuja nayo na naomba kuinukuu; “*The Minister shall, within three months prior to the commencement of fiscal year other than the fiscal year in which this Act comes into operation, cause to be prepared for approval by the Government; an annual Debt Strategy and borrowing plain ambayo sheria hii ni ni mazonge matupu, kwa hii sheria naomba iangaliwe vizuri ili Zanzibar waanze kujikomboa na si vibaya Serikali ya Jamhuri*

Muungano kutokana na uwezo wako wakaifkiria Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikuwa na kilio tulipitisha sheria hapa ya *TASAC* (ya meli) lakini ninavyoju mimi mtu anapokamatwa, anatakiwa afuate sheria za sheria kama meli imekamatwa China itafuata sheria za nchi ya China, Zanzibar uchumi wake umekuwa mdogo, sasa *ZMA* imekuwa pale haina kazi kipindi hiki na usajili wa meli umeanza nafikiri Zanzibar kabla ya Tanzania Bara.

Kwa hiyo, mambo mengi narudia tena yale yale kwa Zanzibar imeanza mapema, kwa hiyo ifike pahali muangalie uchumi wa Zanzibar umekuwa ni mdogo, tufike pahali sheria tuiangalie *ZMA* imekwama kutokana na sheria ile, lakini sheria inasema meli inapokamatwa inahukumiwa na sheria za nchi, siwezi mtukakamatwa Oman akaletwa Tanzania akahukumiwa, anahukumiwa kule kule sheria na nchi hiyo, tufike pahali ili tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini njie na lingine niendelee kushukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondoa *VAT* na hatimaye kuwa sifuri na unaweza kuomba mambo mengi, lakini ukafanikiwa moja mengine yakaja baadae, niendelee kuomba tena umeme ule walionunua *Tanga Cement*, *Twiga Cement* na baadhi ya kampuni nyingine na bei niliyonunua Zanzibar karibu *almost* sawa, ukizingatia Zanzibar miundombinu ni yake mwenyewe ya baharini na ikaharibika anatengeneza kwa pesa zake. Kwa hiyo, hilo nalo mlifikirie na mllichukue, huwezi kuomba mambo yote kwa mpigo ukaja ukafanikiwa kwa wakati mmoja, hili mkae na mlifikirie, hali iko mashaka na duniani kote kuna bei ya rejareja na jumla kwa hiyo hili nalo mlizingatie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini njie kwenye suala la bidhaa za Zanzibar kuingia katika soko la Tanzania Bara; imekuwa kizungumkuti cha muda mrefu tufike pahali, hapa rafiki yangu Mheshimiwa Mwijage alipokuwa Waziri wa

Viwanda na Biashara tulikuwa tukipigana vikumbo sana, leo tufikieni sukari ile ya Zanzibar pamoja na udogo wake kwani kuleta hapa kuna tatizo gani? Leo bidhaa za Zanzibar zimeingia kule hakuna *question mark* yoyote, leo bidhaa zinatoka Uganda, zinatoka Congo, zinatoka Zaire zinaingia bila vikwazo vyovyote. Zanzibar inategemea biashara tufike pahali napo hili mlizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kw nye suala la ajira za Muungano; hapa nilikuwa nikiomba kidogo papangwe *formula* maalum kuhusu ajira kwa sekta za Muungano, hiki ni kilio cha muda mrefu hakujawa na *formula* maalum mpaka muda huu. Kama ipo nafahamishwa ipo, kwa hiyo naomba nifute kauli yangu hiyo naambiwa ip, kwa hiyo ipo naomba kufuta kauli yangu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mgao wa mashirika ya Muungano iiwepo *TCRA*, Posta, benki *NBC* na kadhalika nyingine mpaka muda huu hayo mashirika hayajatoa gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizi nije kwenye suala la Zanzibar inategemea zaidi uchumi wake karafuu, Mungu ajalie ziweze kuzaa, lakini kukikosekana karafuu ni utalii; sasa hivi utalii umekuwa ukigwaya gwaya maana yake, ikiwemo sheria ya Wizara ya Fedha za Tanzania sheria mnazozitunga Tanzania Bara baadhi ya sheria muwashirikishe ndugu zetu wa Zanzibar, kuna sehemu zinawagusa, haziko sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele yako imelia, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daimu Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo na mimi kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali.

Kwanza niipongeze Serikali yetu kwa mambo makubwa ambayo imeyafanya, lakini nitatoa pongezi za kipekee kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunduru kwa ujumla kwa Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutuokoa katika janga la korosho. Nitashukuru kwa sababu wakulima karibu asilimia 80 wamelipwa wamebaki asilimia 20; lakini nilitegemea katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wakati amekuja angalau angezungumza jambo kidogo kuhusu suala la korosho, lakini bahati mbaya sikuona, naomba nimkumbushe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, korosho ni zao la biashara upande wa Kanda ya Kusini, lakini ndio tegemeo kubwa kwa wananchi wa Kusini, nilikuwa naomba kati ya tozo ambazo umeziona zitolewe ningeomba na *export levy* kwenye korosho nayo iondolewe ili iweze kusaidia wakulima kwa sababu kwa sasa imeonekana *export levy* ni gharama kwa mnunuzi halafu ni mzigo kwa mkulima ambapo bei yake ya korosho inapungua. Tukiangalia kwa sasa hali tuliyokuwa nayo korosho kuwepo maghalani madhara ya kuwepo maghalani hapo mbele itakuwa ni makubwa, lakini kama tungeweza kutoa *export levy* ninaamini kuna wanunuzi ambao wangeweza kujitokeza kuweza kununua korosho zile kwa bei ambayo ingeweza kusaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa gharama zetu ni kubwa ukiongeza mzigo wa *export levy* korosho zile mpaka sasa hivi wanunuzi waliokuwa wengi wanaziogopa na athari zake zitakuwa ni kubwa kwa sababu msimu ujao wa korosho unakaribia kuanza hapo mwezi wa nane jambo ambalo kutakuwa na madhara makuu mawili. La kwanza tutakosa mahala pa kuhifadhi korosho kwa sababu korosho nyingi zimejaa kwenye maghala ambayo ndio tunayoyategemea, kwa hiyo nilidhani katika mkakati wa Serikali wa awamu ijayo, moja ya mkakati ingekuwa ni kuongeza maghala katika maeneo ambayo yanazalisha korosho; lakini madhara ya pili wanunuzi wetu ni wale wa kila siku ambao ni Wahindi wa Vietnam ukweli wanajua tuna tani 224,000 kwenye maghala yetu, kwa hiyo, wataogopa kuja katika msimu ujao kununua korosho zetu kwa sababu

wanajua kwamba korosho zikikaa zaidi ya miezi sita ubora unaendelea kushuka siku hadi siku. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba naongea hili kwa uzoefu nimekuwa *General Manager* zaidi ya miaka nane kwenye sekta ya korosho. Ninajua korosho, naombeni sana Serikali kwa kuangalia hali ilivyo sasa basi tukubali bei itakayojitokeza tuuze zile korosho isije yakatokea yaliyotokea mwaka 2013/2014; jambo hili lilijitokeza na korosho tuliuza nusu bei, naomba sana Serikali iliangularie hili kwa kuangalia gharama zake ambazo zitasaidia korosho zile ziuzwe ili kunusuru msimu ujao korosho ziuzike kwa urahisi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nilikuwa ninaomba kuna wananchi ambao wanadai mpaka leo, waliobaki walio wengi ni wale ambao ni wakulima wakubwa vijijini kwetu, hawana namna ya kuhudumia mikorosho, hawana namna ya kupulizia, basi kwa kuwa wanadai na Bodi ya Korosho wana pembejeo ambazo zipo kwenye maghala basi uwekwe utaratibu wa kuwakopesha wale wananchi pembejeo pindi Serikali itakapopata fedha basi waje kupunguza kwenye hayo mapato yao ili na wao waweze kuhudumia mashamba yao ili angalau mwakani nao waweze kuvuna zaidi. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu hawana namna kilio kimekuwa ni kikubwa sana, naomba sana Mheshimiwa Waziri uliangularie hili kwa upande wa huruma sana wale wakulima hawana namna yoyote ya kuweza kuwasaidia zaidi ya kuwakopesha pembejeo ili waweze kupalilia na kupulizia mikorosho yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine napenda niishukuru sana Serikali na kuipongeza kwa sheria ile ya mwaka 2005 ya mfumo wa stakabadhi gharani na ndio iliyoifanya korosho iongezeke uzalishaji mpaka mwaka 2017/2018 ukafikisha tani 3,13,000; lakini bahati mbaya yale yaliyojitokeza mwaka jana ambayo tuliyayalamikia kwa muda mrefu uzalishaji umeshuka mpaka tani 224,000 na hii ilitokana na namna ambavyo tuli-handle pembejeo kwa wakulima wetu ambazo jambo tulilokuwa tumelilalamikia kwa muda mrefu, lakini halikutilia maanani.

Kwa hiyo, ninaomba sana ili kuongeza uzalishaji basi tupunguze gharama na miaka ya nyuma Serikali ilikuwa inatoa ruzuku kwenye pembejeo, nimesema nimekuwa kwenye korosho miaka nane, miaka ile Serikali ilikuwa inatoa ruzuku kwenye *sulphur*, ilikuwa inatoa ruzuku kwenye mbolea, lakini jambo lile limesitishwa naomba ile ruzuku irudie tena kwa wakulima ili waweze kununua pembejeo kwa bei rahisi na waweze kununua kwa wingi waweze kuzalisha zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mfumo ule wa Stakabadhi gharani tulisema tunaanza kwa mfano katika kanda ya korosho mafanikio yameonekana na hata sasa hivi upande ule tumeamua ufutwe kutumia mfumo wa stakabadhi gharani. Matokeo yake yamekuwa mazuri, bei imikuwa nzuri. naomba Serikali kwa kuwahurumia wakulima wa Tanzania ule mfumo ni mzuri uendelee kwenye maeneo mengine ya kahawa, pamba na tumbaku ili wakulima waweze kufaidika kama wenzao wa ufuta na korosho walivyoweza kufaidika miaka miwili, mitatu iliyopita. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Augustino Holle Vuma ajiandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwanza ningependa kuchangia kwenye suala la korso ambalo mzungumzaji aliyepita amezungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa korosho walikuwa wanategemea pamoja na mambo mengine tungeona maelezo ya Serikali juu ya utaratibu upi utatumika

kuziondosha korosho zilizo kwenye maghala kule Lindi, Mtwara na Ruvuma. Korosho zimejaa kwenye maghala, hata sasa hivi kuna ununuzi wa ufuta, ufuta ule hausafirishwi kupelekwa kwenye yale maghala makubwa kule mikoani kwa sababu hamna nafasi, msimu wa korosho umeanza. Tunaposema sasa hivi maeneo yale ya ukanda wa pwani kama Jimboni kwangu pale Mchinga, Kilwa na kwa Mheshimiwa Nape pale Mtama tayari zimeanza na mwezi wa saba tutaanza kuokota/ kuzikusanya, mwezi wa nane/tisa zinakuwa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hebu tuelezeni mtatumia utaratibu gani kuziondosha zile korosho zilizopo maghalani ili matajiri watakaokuja kununua mwaka huu wawe *assured* kwamba hawatachanganyiwa korosho za mwaka jana na mwaka huu. Inafahamika kwamba ubora wa korosho za mwaka jana hauwezi kufanana na za mwaka huu. Kwa hiyo, kama kuna mpango wowote Serikali mnaweza mkaufanya *either* kuziuza hata kwa *undergrade* ili muweze kuziondoa ama vinginevyo basi zitaifisheni ili ziondoke ili sisi baadae hizi tunazozalisha mwaka huu, tuweze kupata bei tunayostahiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taarifa tumezisikia na tunaendelea kuzifutilia kwamba *World Trade Organization (WTO)* wameanza mchakato wa kufutililia mfumo wa ununuzi wa korosho Tanzania kwamba isije wanunuzi mwaka huu wakaja kupata hasara, kuna uwezekano mkubwa wanunuzi wakubwa wasije kwa sababu ya kuhofia korosho za mwaka jana zikachanganywa na za mwaka huu. Fuartilieni watu wa Serikali kwa sababu mpo nadhani mtakuwa mnalijua vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wowote wa nchi lazima uwe jumuishi, kusipatikane watu wakaachwa, wengine wakaendelea sana na wengine wakawa maskini sana, tutasababisha migogoro na migogoro mingi katika mataifa ya Afrika ni kwa sababu ya *distribution of resources*, watu wakihisi kwamba sisi tumeachwa, wengine wameondoka, kunaleta matatizo na wakati mwingine kunakuwa na fujo katika nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara unategemea gesi, korosho na uvuvi, ni jambo muhimu sana. Nitatoa mfano, wakulima wa korosho ndiyo kama nilivyozungumza, waliobakia ni wavuvi; leo dagaa hawa wanaopatikana pale Kilwa wanatozwa ushuru wa dola 1.5 kwenye kila kilo, ni zaidi ya shilingi 3,000 na; lakini dagaa hawahawa ambao wanasafirishwa kupelekwa Congo wote wanaotoka kwenye maziwa kwa mfano Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ushuru wake ni dola 0.16, *this is quiet unfair*. Hatuwezi kuwa na uchumi ambao bidhaa moja aina inayofanana huku inatozwa kodi kubwa, huku inatozwa kodi ndogo kwa lengo gani? Uchumi wa namna hii utapelekea...

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: ...kutuacha wengine wawe wameendelea sana, wengine tuendelee kuwa maskini.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika,...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali kuna taarifa. Mheshimiwa Peter Serukamba.

T A A R I F A

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa taarifa mse maji, mimi natoka Kigoma, Kigoma pia dagaa wale wanaosafirishwa kilo moja wanatozwa dola 1.5 siyo 0.1.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali unaipokea taarifa hiyo?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Taarifa yake nimeipokea lakini maelezo ya Waziri wa Uvuvi wakati anazungumza na hili jambo tumelifuatilia

sana, tulipewa maelezo humu ndani ya Bunge kwamba dagaa wa Pwani wanatozwa dola 1.5 na dagaa wanaotoka kwenye maziwa wanatozwa dola 0.16, maji baridi maana yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa kama hilo na wenyewe wamekuwa *introduced* huko, ninachozungumza kwanza hii tozo yenyewe ni kubwa sana. Kilo moja ya dagaa unapotoza dola 1.5 zaidi ya shilingi 4,000 au 3,000 tuseme ili hawa dagaa wenyewe wauzwe kwa bei gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi napendekeza hii tozo iweze kushushwa badala ya kuwa dola 1.5 walau ishushwe iwe dola moja ama chini ya dola moja ili hawa wavuvi wa dagaa waweze kupata fedha stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia uchumi jumuishi. Kwenye llani ya CCM iliwekwa kitu kimoja kizuri sana na kama kingetekelawa kingewafanya Watanzania waendelee kuwa na imani sana na Chama cha Mapinduzi, kupeleka shilingi milioni 50 kwenye kila kijiji/mtaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namna pekee ya kusaidia watu maskini ambao hawawezi kufanya biashara, wameminywa kwenye kilimo ni kuwasaidia moja kwa moja kwa kupeleka fedha kwenye maeneo yao kuwe na mtiririko wa fedha watu waweze kutumia zile fedha kwenye biashara na mambo mengine. Mngekuja na maelezo, leo kwenye bajeti ya nne hii Serikali ya Awamu ya Tano mmeshindwa kabisa hii shilingi milioni 50 kwenye kila kijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama wawakilishi tunapokwenda Majimboni tunaulizwa na hakuna tamko rasi la Serikali mlilolitoa kwamba imeshindikana shilingi milioni 50 kila kijiji, shilingi milioni 50 kila mtaa. Semeni ndani ya Bunge ili na sisi tukienda tukaseme hili limeshindikana jipangeni na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nasema kwa sababu kuna wakati kule Jimboni kwangu kuna watu walikwenda wakawatapel i watu, wakawaambia leteni elfu kumikumi, zile shilingi milioni 50 zinakuja na bahati mbaya sana waliovatapeli wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwamba utaletewa na hizi fedha zikija nyie ndiyo mtapewa kipaumbele. Kwa hiyo, yanetoka maelezo ya kina juu ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa gesi; uchumi wa gesi ni uchumi ambao mimi nadhani ungeweza kusaidia Mikoa ya Lindi na Mtwara lakini pia ungeweza kusaidia kama taifa. Upo mradi wa *LNG* ambao *financiers* watu wanaotaka kutoa fedha siyo Serikali, Serikali kazi yao ni kufanya *regulation* na kuangalia manufaa ambayo sisi tutakuja kuyapata. Wawekezaji wapo tayari na mwezi uliopita tulikutana nao pale Lindi, tulikwenda *Wabunge* wote wa Mkoa wa Lindi, wanaonesha *commitment* kwamba wapo tayari, hatuoni *progress* yoyote ya Mradi wa *LNG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza wakati nachangia Wizara ya Nishati hapa, *LNG* kwa Tanzania siyo mradi wa kwanza Afrika. Kama kuna mambo mnahitaji *ku-study* kwa nini msiende kwenye nchi ambazo tayari hii miradi inatekelezwa? Kwa nini msiwende Angola, Msumbiji, Algeria na maeneo mengine mkaenda *mka-study* wenzetu walifanyaje, mnanufaikaje. Huu ni mradi ambao ungeweza kusaidia sana pato la Taifa kwa *ku-create* ajira lakini pia mngeweza kuinua uchumi wa Watanzania hususan wa Mikoa ya Lindi na Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali upande wa Mkoa wa Lindi eneo limetengwa, wananchi wapo tayari kuhama na wameshafanyiwa tathmini ya malipo, leo huu mwaka wa nne watu wamezuiwa wasiendeleze maeneo yao, mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, na lenyewe hili kwa sababu ni mradi wa kimkakati, mradi ambao ulikuwa unakuja kuwekezwa zaidi ya shilingi trillioni 59, ni mradi mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iseme mradi huu umeishia wapi, kama hautakuwepo tena basi kila mtu aweze kujua ili wale wananchi tuweze kuwaambia kwamba haya maeneo yenu limeni ufuta na karanga, hii habari ya *LNG* imeishia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mchache uliopita nilikuwa na kikao hapo na Profesa Lipumba, Mwenyekiti wetu wa Chama ambaye pia ye ye ameniambia kwamba ye ye ni mwalimu wa Dkt. Mpango, amemfundisha uchumi Chuo Kikuu.

Sasa ukiangalia kwenye takwimu za Umoja wa Mataifa, takwimu ya mwisho iliyotolewa mwezi wa tatu ya hali ya furaha ya wananchi katika ulimwengu, Tanzania tupo nchi ya 153 kati ya mataifa yote ya ulimwengu. Maana yake inaonesha kwamba wananchi wa Tanzania wengi hawana furaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mpango unaweza kujiuliza kwa nini watu hawana furaha na hata ndani ya Bunge inaonekana, wakati unasoma bajeti yako mwaka jana hapa, palikuwa na vigelegele na makofi, humu ndani tuliambiwa hii ni bajeti ya kihistoria haijawahi kutokea, uliposoma mwaka huu umeyaona yale? Kwa sababu huko nje watu hawana furaha na takwimu za mwezi wa tatu mwaka huu, Tanzania tunatajwa tupo wa 153 kwa kiwango cha furaha. Sisi katika Afrika Mashariki tunawazidi Burundi na jirani zetu hapa kidogo wa Somalia, kwisha habari. hata wenzetu Kenya na Rwanda wametuzidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali/mazingira ya biashara, Tanzania tupo 144 Rwanda wapo nchi ya 29, Kenya wapo nchi ya 40, mazingira ya biashara mnakuja kutuambia uchumi unakua, kweli Mheshimiwa Mpango? Na swalii moja mimi nilimuuliza Mheshimiwa Profesa Lipumba, huyu si ndiyo mwanafunzi wako, inawezekanaje haya mbona humuelezi haya maana yake anakuja kutueleza hapa. Akasema sasa wakati mwingine unapotoa ushauri usipofanyiwa kazi unaachana nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Mpango kiukweli kabisa vyuma vimekaza, hali ni mbaya. Hata takwimu zako wewe mwenyewe, ukisoma kitabu hiki cha hali ya uchumi. Nasikitika hiki kitabu tungekuwa tunakipata wakati ule wa kusoma randama zile kwenye bajeti za kisekta kwa sababu ingweza kutusaidia pia kuchangia kwenye sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho; ukiangalia kitabu cha hali ya uchumi, inaonesha kilimo kinachangia asilimia 28 ya Pato la Taifa, lakini kwenye bajeti yako Mheshimiwa Mpango mmepeleka asilimia 1.2. Sasa huyu ni ng'ombe gani wa maziwa ambaye unataka akupe lita 20 kwa siku halafu haumlishi yaani yeche ambaye anakupa asilimia kubwa ya pato la Taifa unamtengea asilimia 1.2. Mheshimiwa Waziri hatuwezi kwenda na kwenye uchumi wa viwanda kama kilimo hakiko vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, tutamalizia na Profesa Jumanne Kishimba.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye mapendekezo ya bajeti ya 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mpango pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema ukweli, bajeti hii iliyosomwa safari hii, mimi nimefanya utafiti huko nje, nimeongea na watu na wasomi na kila mmoja, bajeti hii wameipenda vizuri sana. Wanasesma hawajawahi kuona bajeti nzuri kama ya safari hii, Mheshimiwa Waziri songa mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi nzuri mnayoifanya, bajeti hii wameipenda, imegusa kila mmoja, wanasema ni bajeti nzuri mbayo hawajawahi kuionna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kuipongeza Serikali kwa kufanya uhakiki na kulipa madeni ya wazabuni pamoja na watoa huduma, mmeefanya kazi nzuri, bado mnahakiki. Licha ya hivyo naomba kukwambia kuwa kuna baadhi ya vyuo ambavyo ni vya kilimo, baadhi ya shule za sekondari kwenye Mkoa wangu wa Morogoro ambaao bado hawajalipwa kama MATI Ilonga kuna na sekondari ya Morogoro kuna wanaodai. Naomba waifanyie kazi na ninavyosema hivi, bila shaka kuna na mikoa mingine kuna wazabuni na wakandarasi ambaao hawajalipwa naomba waendelee kuhakiki Serikali iweze kuwalipa kama ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuongelea mambo ya vipaumbele kwenye bajeti hii na nianze kwa viwanda pamoja na kilimo. Ili viwanda viweze kuendelea lazima tuangalie kilimo, kilimo ndiyo kinacholeta malighafi kwenye viwanda na ninaposema kilimo hapa namaanisha kilimo mazao, uvuvi na mifugo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo asilimia 65.5 ya wananchi wanategemea kilimo na hasa huko vijiji na asilimia ya chakula asilimia 70 ni wanawake wanaozalisha chakula hiki. Kwa hiyo, naomba tunavyoongelea kilimo tuwape kipaumbele wanawake na hasa kuangalia kwenye upande wa mikopo na kuangalia jinsi watakavyoendeleza kilimo hiki. Hakuna kilimo/chakula bila ya kumuangalia mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ila kuna changamoto kidogo kwenye upande wa kilimo, bado tunatumia kilimo cha jembe sana sana ingawa naipongeza Serikali kwa upande wa matrekta yameongezeka, lakini unakuta bado tuna matatizo tunatumia kilimo cha mvua, bado ni kilimo cha

mvua kinashamiri. Kwa hiyo nilikuwa naiangalia na kuiomba Serikali yangu iangalie kilimo cha umwagiliaji. Tukifanya kilimo cha umwagiliaji, tutaweza kusonga mbele na tutaweza kupata malighafi ya kutosha kwenye mazao yote ambayo tunalima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jambo lingine kubwa sana kwenye matatizo ya kilimo ni mbegu. Mbegu hapa nchini tunazalisha asilimia 21 tu, mbegu nyingine zinatoka nje, tatizo ni nini? Tatizo ni ASA ambao ndiyo wanadhibiti na wazalisha mbegu, ASA hawana bajeti ya kutosha. Mheshimiwa Waziri naomba ASA wapate bajeti hiyo waliyoomba fedha ziweze kupitishwa zote kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzalisha hizo mbegu, wanaodhibiti hizo mbegu ni *TOSCI*, *TOSCI* na wenyewe hawana fedha, naomba na wenyewe waweze kupewa fedha za kutosha kusudi tuweze kupata mbegu za kutosha. Huko ni kwa upande wa mazao hasa nafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye mbogamboga (*horticulture*) pamoja na matunda ni asilimia moja tu ya mbegu tunazalisha hapa nchini na sanasana ni vitunguu. Kwa hiyo, naomba sana kwa sababu mbegu nyingi zinatoka nje, je, tatizo ni nini? Naomba sana na yenewe ni ASA hawana fedha za kutosha, naomba muwapatie fedha za kutosha, huo ndiyo ushauri wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mbolea; tunategemea mbolea kutoka nje. Tuna kiwanda kimoja cha Minjingu, Minjingu nayo haipendwi sana hapa nchini, kwa nini, ni baadhi ya wachache wanaipenda. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali yangu na hapa wanaohusika watuambie Kiwanda cha Mbolea cha Lindi ni lini kitaanza kuzalisha mbolea? Kwa sababu tukipata mbolea yetu, naamini tutaweza kulima na kuzalisha vizuri sana kwa sababu mbolea pamoja na mbegu bora tutaweza kupata mazao bora ambayo yanaweza kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hii programu ya *SAGGOT* pamoja na *ASDP*, Serikali wamepanga mkakati mzuri kwenye upande wa kilimo, naomba hela zote zilizopangwa kwenye mkakati huo ziweze kutoka na zikitoka tutaweza kupata mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko yanaenda pamoja na mazao na viwanda. Nashukuru kuona viwanda vimeanza kujengwa, kuna viwanda vya korosho viro, naipongeza Serikali wanajitahidi kwenye kuangalia na kuangalia wakulima wa korosho wawasaidiaje, siyo kusema wamewaachia wanawasaidia kadri wanavyoweza na najua kila kitu kitakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazao ya mikunde tumeweza kupata kiwanda hata Morogoro tuna kiwanda kimejengwa ambapo tutaweza kununua mbaazi, karanga na maharage. Kwa hiyo, hata matatizo yaliyokuwepo kwa upande wa mbaazi yatakwisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema kilimo inakwenda na miundombinu/barabara; kuna barabara za mashambani, barabara za mashambani zingine zimesahaulika, naomba sana ziangaliwe. Kuna barabara za uchumi; nikisema barabara za uchumi kwa upande wa Morogoro kuna barabara ya kutoka Kidatu – Lupilo – Malinyi – Songea, Namtumbo. Tumetengewa hela kidogo, naomba Mheshimiwa Waziri hela hizo zilizotoka ziweze kutolewa na zenyewe ni za ukarabati. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, iweze kujengwa kwa lami kwa hiyo ndiyo hivyo uchumi utaendelea na kwa sababu inaunganisha mikoa miwili; Mkoa wa Ruvuma pamoja na Mkoa wa Morogoro iweze kuangaliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwa upande wa mifugo, mifugo tuweze kufuga mifugo ya tija. Kwa upande wa mifugo waangalie sana kuhusu malisho. Naomba bajeti yote iliypangwa kwenye malisho iweze kutoka pamoja na matumizi bora ya ardhi. Tulisema kuwa ardhi iweze kupimwa,

ikipimwa hakutakuwepo matatizo yoyote na wafugaji wataweza kufuga vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi; uvuvi wa bahari kuu bado hatujautendea haki. Naomba sana Serikali yetu iangalie uvuvi wa bahari kuu, maziwa, mito na uvuvi ambao tunasema ni wa mabwawa. Ili tupate samaki wengi, lazima wananchi wahamasishwe kufuga kwenye mabwawa na hii itasadida hasa na kwenye utapiamlo kwenye mambo ya lishe. Fedha zote zilizotengwa kwenye mambo ya lishe ziweze kutolewa na ziweze kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa uchumi kwa maendeleo; naomba kuongelea kuhusu *Stiegler's Gorge*. *Stiegler's Gorge* tunaifurahia sana na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kulona hili na kulendeze na tunaamini haturudi nyuma, tunasonga mbele pamoja na umeme huu wa *Stiegler's Gorge* na ninaamini tutapata umeme mwingi na tutaweza kuzalisha kwenye viwanda vyetu na tunaweza kufanya mambo mengine kuhusu huu umeme. Pamoja na hii *Stiegler's Gorge* kuna mambo ya umwagiliaji pamoja na barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Miradi yote iliyolala iweze kukamilika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. Ahsanteni sana, nashukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Augustine Holle Vuma tutamalizia na Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni ya leo ambayo nimepata na mimi kuungana na wenzangu kwenye kuchangia bajeti hii ambayo ni bajeti inayoonekana inakwenda kumkomboa Mtanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mambo matatu; jambo la kwanza, nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya bila kuchoka kuweka mikakati vizuri kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii kwa ujumla. Dhamana aliyopewa ni kubwa na sisi tunamuombea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpungeza Mheshimiwa Rais kwa kumkaribisha Ikulu pacha wangu, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Papa Félix Tshisekedi. Sisi watu wa Kigoma uchumi wetu kama Mkoa una mashirikiano makubwa sana na nchi ya Kongo. Kwa hiyo Rais alivyomuita Rais mwenzake wa Kongo kumkaribisha Ikulu tunaamini kwamba wamezungumza mambo makubwa na mazuri ambayo yatapunguza baadhi ya vikwazo mpakani pale na hatimaye tutaendelea kupokea Wakongomani wengi Kigoma kwa ajili ya kufanya nao biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye bajeti; nipende kushauri yafuatayo, jambo la kwanza, upande wa mawakala hawa wa kutoa mizigo bandarini. Kaka yangu Dkt. Mpango, mimi hili sjalielewa vizuri, ninapenda Serikali ije na maelezo mazuri na ya kina tuweze kuelewa kwa sababu tunaamini *clearing and forwarding* ni *profession* ya watu ambao wamesoma vyuoni wamemaliza na wana-practice vizuri ili kuweka waraka wa kufanya shughuli hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa anapokuja mtu wa kawaida tu ambaye hana *knowledge* hiyo wala haelewi hicho kitu, tunapaswa kujua lakini tuelewe hatma ya makampuni haya ya watu ambao wanafanya *clearing and forwarding*, tuweze kujua kwa sababu kuna ajira nydingi ambazo ziko huko. Mimi nadhani kama kungekuwa kuna matatizo kwa hao ma-agent ilikuwa ni busara zaidi

kuwafanya *vetting* na kuwaondoa wale ambao hawastahili kuliko kusema kwamba kila mtu aweze kufanya *clearing and forwarding* ya mzigo wake. Sina maana ya kupinga hili, lakini nataka Serikali ije kunishawishi, iweze kutueleza tuweze kufahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mifugo; mimi nipende kushauri jambo moja, nchi hii imekuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji kila siku. Bunge lililopita niliuliza mkakati wa Serikali kupunguza mifugo labda ili kuweza kupunguza migogoro hii katika wakulima na wafugaji, lakini nikaona kwamba kupunguza mifugo kwa kweli ni jambo ambalo ni gumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninashauri jambo moja kwamba Serikali nadhani inapaswa kutenga vijiji vya ufugaji ambavyo vitakuwa havina wakulima. Yapo maeneo ambayo Mheshimiwa Rais anasema kwamba yamepoteza sifa za uhifadhi, nadhani tutenge vijiji vya ufugaji ambapo wafugaji wote tutawaambia waende kule na watakuwa hawakutani na wakulima. Hii itaweza kupunguza migogoro katika wakulima na wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya Utalii; watu wengi ambao wamewekeza kwenye sekta hii wanalamika kwamba vibali vya uwindaji ambavyo wanapewa ni vifupi. Kwa hiyo, wanashindwa kufanya uwekezaji wa muda mrefu kwa sababu wanapewa vibali vya mwaka mmoja. Kwa hiyo, nashauri Serikali ilitazame hili, itoe vibali vya muda mrefu ili wawekezaji hawa waweze kutoa hela zao mfukoni kufanya uwekezaji kwenye maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sisi pale Kagerankanda tuna mwekezaji wa kitalu cha uwindaji, alitaka atujengee mabwawa ya samaki kwa ajili ya ile jamii inayozunguka, lakini mradi ule unaenda miaka miwili na ana kibali cha mwaka mmoja kutoka Serikalini. Kwa hiyo amesitisha kwa sababu inawezekana akianza kujenga ule mradi kibali chake kiki-expire basi asiweze kuongezewa na hatimaye akapewa mtu mwingine kwa hiyo inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kushauri ni kwenye upande wa hawa...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Taarifa, taarifa.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: ...upande wa elimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuma, kuna Taarifa. Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa.

T A A R I F A

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba katika jambo analolisema kwamba wawindaji wanapewa vitalu muda mfupi, ninataka nimuongezee taarifa kwamba kwa kweli limekuwa ni tatizo na hivi sasa Wizara ilitoa mpango wa mnada, mnada umeshindikana, kwa hiyo hivi vitalu kuna uwezekano wa kuvipoteza na tukapunguza mapato kwenye mpango wako Mpango kwa sababu mpango huu wa kunadisha vitalu karibu 90 vimekosa wateja, ni mipango mibovu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimpe taarifa tu katika hili analolisema.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuma, unapokea taarifa hiyo?

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa naipokea na Serikali ije kutoa majibu hapa wakati wa majumuisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye upande wa elimu hakuna...

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa elimu napenda kushauri jambo moja...

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuma kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nimheshimu sana Mheshimiwa mchangiaji, lakini ninataka tu niweke kumbukumbu sawa. Mnada ambao unaendelea sasa wa vitalu haujafungwa na mnada huo umepandisha thamani ya kitalu kutoka dola 60,000 kwenda dola 150,000 na ninataka kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika marekebisho yetu ya Kanuni suala la mwaka mmoja halipo, tulikuwa na miaka mitano tunakwenda miaka kumi. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Augustine Holle Vuma unapokea Taarifa hiyo?

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa na ninawatakitia utekelezaji mzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Nabu Spika, niseme kwenye suala la elimu; hili nashauri kitu kimoja; hapa mtaani kuna vijana wengi ambaao tumewakopesha fedha nyingi sana ambaao wamemaliza vyuo, sisi tunawadai pesa, lakini wao wanaidai Serikali ajira na wakati huo huo Serikali haina watumishi wa kutosha kwenye idara za walimu, katika hospitali na sekta zingine. Sasa nikasema, kwa nini hawa vijana ambaao wanamaliza shahada zao ambaao wana mikopo, kwa nini tusiwape mikataba mifupi ambayo tutakuwa tunawapa hela za kujikumu na hatimaye waende kufundisha au kufanya kazi katika hospitali huko na kwenye sekta mbalimbali huku wakiwa wanalipa madeni ambayo wanadaiwa na Bodi ya Mikopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wale vijana tunawadai pesa, wao wanatudai ajira na hatuna watumishi. Sasa tuangalie sehemu ambayo tutakutana hapo katikati; vijana hawa wakimaliza wakienda kufanya kazi kwanza watakuwa wanalipa madeni yao, lakini pia watakuwa wanapata uzoefu. Kwa sababu vijana wengi wako mtaani, lakini uzoefu wa kufanya kazi hawana mpaka wanashindwa kupata kazi kwenye sekta binafsi kwa sababu hawana uzoefu, kwa hiyo tutawapa uzoefu lakini pia watakuwa wanalipa madeni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali barabara ya kutoka Buhingwe – Kasulu – Nyakanazi, naomba sana utekelezaji wake. Lakini pia naomba barabara ya kutoka Kasulu kwenda mpaka Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niweze kuja kwenye suala la *SGR*; nimemsikia ndugu yangu, kaka yangu hapa, Mheshimiwa Mwakajoka anasema kwamba wao hawapingi miradi ya *SGRna Stiegler's Gorge* lakini hawataki fedha nyngi ziende kwenye miradi ile; kituko kabisa hiki, hiki ni kituko, yaani miradi unaitaka lakini hutaki fedha nyngi ziende kwenye miradi ile kwa sababu miradi ya matrillioni inatengewa mabilioni...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: ...kila mwaka wewe hautaki hela ziende kule ila miradi unaitaka...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: ...yaani unajitekenya halafu unacheka mwenyewe. Sasa hili ni jambo ambalo ni la kusta... (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuma, kuna taarifa. Waheshimiwa Wabunge, hii ni taarifa ya mwisho kwa

Mheshimiwa Vuma kwa sababu hii ni taarifa ya tatu tayari.
Mheshimiwa Mwakajoka.

TAARIFA

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kumpa taarifa mzungumzaji, siyo kwamba tumesema kwamba hatupingi halafu fedha nyingi zimekwenda kule. Tulichokizungumza hapa ni kwamba maeneo ambayo wananchi wengi wanatakiwa kupata huduma fedha hazijapelekwa.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaishauri Serikali muda wote na tumeishauri Serikali muda wote kwamba fedha zipelekwe katika maeneo hayo; ndege, umeme, kila kitu tunakihitaji, lakini fedha ni nyingi mno ndiyo maana tumesema tunahitaji mgawanyo ambao uko sawa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni kwamba haja...

NAIBU SPIKA: Taarifa ni moja Mheshimiwa Mwakajoka. Mheshimiwa Augustine Holle Vuma unapokea taarifa hiyo?

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, hii taarifa siipokei kwa sababu huyu mtu anajichanganya na niseme, unajua sisi Mkoa wa Kigoma unapozungumza reli ni *identity* yetu, ni utambulisho wetu, ndiyo maana Mkoa wa Kigoma umekuwa unaitwa kwamba ni mwisho wa reli. Kwa hiyo, sisi Kigoma tunahitaji reli kwa gharama yoyote ile na ninaishauri Serikali iendelee kupeleka pesa kwenye *SGR* ili tupate reli, *SGR* ifike Kigoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua kuna watu hapa ambao kwao wanakotoka maeneo yao hakuna shida za usafiri, wao zimeshaisha. Sasa Kigoma unapokwenda kupinga reli tunakuita ni msaliti wa Mkoa wa Kigoma, kwa hiyo sisi tunaiunga mkono kabisa Serikali, tunahitaji *SGR* Mkoa wa Kigoma kwa sababu tunaamini itakuwa ni mkombozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tunaamini kwamba *SGR* hii ina faida za muda mfupi katika ujenzi wake lakini na faida za muda mrefu. Faida za muda mfupi, jambo la kwanza *SGR* hii *Lot One* *Lot Two* inayoendelea kujengwa imeajiri sasa hivi mpaka leo tunavyozungumza Watanzania 17,000 wamepata ajira kwenye *SGR*. Lakini kama haitoshi kumejengwa kiwanda cha mataruma kwa hiyo unavyozungumza ujenzi wa *SGR* hauzungumzii vile vyuma kutandikwa peke yake, kuna *element* ya viwanda kwenye ujenzi wa *SGR*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi kuna kuchochaea uchumi ndani ya *SGR*; niseme tu kuna watu wengi sana wanafanya shughuli za kimaendeleo wakati mradi ule unajengwa. Ukiangalia kwa mfano vifaa ambavyo mradi ule unatumia ukianzia na *cement*, inakadiriwa kwamba *Lot One* na *Lot Two* itatumia mifuko millioni 9.2 ya *cement* ambayo yote inanunuliwa hapa Tanzania; lakini itatumia nondo kilo zaidi ya millioni 100, yote inanunuliwa Kamal hapa hapa Tanzania. Sasa ukiangalia haya yanaendeelea kuchochaea uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia bodaboda, mama lishe ukienda kwenye mradi huu wamejaa wanafanya shughuli zao za kiuchumi, huku ni kuchochaea uchumi. Kwa hiyo, unavyoangalia reli, ujenzi wa *SGR* usi-focus kwenye kutandika vyuma tu, kuna vitu vingi viko ndani yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nadhani kuna suala la uelewa; watu wengi huu mradi hawauelewii vizuri, wanausoma na kusikia tu michango ya Bungeni, wanasoma kwenye *whatsApp* na wapi, wanapaswa waende kutembelea mradi huu waweze kuona au ije *presentation* Bungeni hapa watu waweze kupewa shule juu ya Mradi wa *SGR* ili waweze kuelewa kilichopo ndani yake, ule ni zaidi ya mradi wa reli kuna vitu vingi vilivyopo ndani yake; hizo ndiyo faida za muda mfupi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo za muda mrefu; tunaamini kwamba Mradi wa *SGR*, reli ikikamilika itakwenda

kuongeza thamani ya mazao katika nchi yetu. Kwa sababu tunaamini, kwa mfano Mchima amekuja akatangaza soko la muhogo, Kigoma tunalima muhogo lakini gharama za kusafirisha muhogo kutoka Kigoma kuupeleka mpaka bandarini uende China ni *very expensive*. *SGR* itakapokuwa imekamilika tunaamini muhogo utatoka Kigoma mpaka Dar es Salaam kwa muda mfupi na gharma zitakuwa chini. Na *study* inaonesha *SGR* itapunguza gharama za usafiri kwa asilimia 40; nani anapinga *SGR* na kwa nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi, tunaamini kwamba itaweza kulinda barabara zetu ambazo tumezijenga kwa gharama kubwa. Mizigo mingi mikubwa itakuwa inapitia kwenye reli hii ambapo itaweza kulinda barabara zetu kwa sababu barabara zitabaki zinatumwiwa na magari machache, mizigo yote itakuwa inasafirishwa kwenye treni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nipende kuwaomba kwamba wajitahidi kusoma huu mradi wa *SGR*. *Na niseme; hizi bajeti mbadala hizi ambazo zinakuja na vijembe, zinapingga miradi mikubwa kama SGR ni za kuchana hizi, hakuna kitu.* Lazima tuwe *serious* katika mambo kama *haya ili watu waweze kuelewa kwamba...* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

(*Hapa Mhe. Augustine V. Holle alichana kitabu cha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: ...hili jambo ni jambo ambalo sisi watu wa Kigoma tunahitaji lifanyike. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof!*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakajoka umesimama na Mheshimiwa Esther Matiko amesimama na mnazungumzia utaratibu. Mheshimiwa Mwakajoka.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuna mambo ambayo yanafanyika ndani ya Bunge...

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu, natumia Kanuni ya 64; mambo ambayo hayakubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji aliyekuwa anachangia sasa hivi amesimama hapa amechana hotuba ya Upinzani ndani ya Bunge hili. Ninafikiri jambo hili ni dharau kubwa lakini pia ni kutokjielewa kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba yuko humu kwa sababu gani na hajui kwa nini hiki kitabu amepewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba meza yako iweze kutoa sababu na ni namna gani huyu Mheshimiwa Mbunge asiyejielewa achukuliwe hatua ili kidogo akili yake ikae sawasawa maana yake tumemuona kama kichaa fulani hivi ndani ya Bunge. Ahsante sana. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

Amesimama Mheshimiwa Mwakajoka akaitaja Kanuni ya 64 kwamba ndiyo ambayo imemfanya asimame japokuwa ufanuzi wake haukuwa hasa kwenye kifungu kipi cha Kanuni ambacho anaona kimevunjwa. Lakini Kanuni hii ya 64 Waheshimiwa Wabunge, yako mambo mbalimbali ambayo yanakatazwa na inazungumzia kwa ujumla wake

mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Sasa ukisoma Kanuni hiyo ya 64(1)...

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, huwa napenda kusikilizwa na kwa mujibu wa Kanuni zetu nikiwa nimesimama mnapaswa kunyamaza ili mjue nasema nini.

Kanuni ya 64(1) ukiisoma (g) inazungumza kuhusu kutokutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine. Kwa hiyo kwa mchango wa Mheshimiwa Vuma, hoja iliyopo itakuwa si kuchana kitabu maana amezungumza wakati akichana kitabu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Vuma kwa muktadha wa Kanuni hii ya 64(2) ukizisoma zote kwa pamoja, Mheshimiwa Vuma maneno ya kuhusu kukichana kitabu hicho nitakupa fursa ili uweze kuyafuta na jambo hilli Waheshimiwa Wabunge lisirudiwe wakati mwингine.

Mheshimiwa Vuma.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Naibu Spika, napokea busara za Kiti, nafuta maneno yale. Lakini ilikuwa ni kuonesha namna gani ambavyo hotuba hii haina maslahi kwa umma. Ahsante sana.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa Esther Matiko.

Waheshimiwa Wabunge..., Mheshimiwa Heche naomba ukae nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana huwa nasisitiza anapozungumza mmoja wetu ni muhimu sana kumsikiliza. Mheshimiwa Vuma ameonesha kitendo ambacho mimi nimeshakitolea utaratibu na wakati akafanya hivyo amesema kwamba kitabu hiki kinapaswa kichanwe.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Tusikilizane, Kanuni hii...

Waheshimiwa Wabunge, tusifikishane mahali ambapo ninyi mnataka kufika.

Mheshimiwa Vuma ameshaambiwa afute hayo maneno kwa Kanuni...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge sikilizeni, kwa sababu Kanuni aliyoitumia Mheshimiwa huyu inahusu nini; kuna kitendo cha kuchana kitabu hapa? Tusikilizane vizuri Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane vizuri; Kanuni ya 64 utaratibu nimeshautoa kwa mujibu wa Kanuni ya 72, kama mtu hakubaliani na...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Naomba tusikilizane, nimesimama. Nimesimama naomba mnisikilize.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Nazungumza mara ya mwisho, nimesimama naomba mnisikilize.

Tokeni nje. Nendeni, tokeni nje. Kwa sababu hatusikilizani, naomba muende.

Mheshimiwa Esther Matiko, naomba utoke, wote nendeni.

Naomba uende Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Matiko naomba mtoke, hatuwezi kubishana humu ndani. *Sergeant-At-Arms.*

Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Heche, naomba mtoke nje.

Mheshimiwa Esther Matiko, naomba usimame uende nje.

(Hapa Mhe. Esther N. Matiko na Mhe. John W. Heche walitoka Ukumbini)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kishimba.

MHE.JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Sware naomba utoke nje.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Kwa kuomba muongozo?

NAIBU SPIKA: Eee naomba utoke nje tafadhalii. *(Kicheko)*

(Hapa Mhe. Dkt. Immaculate S. Semesi alitoka Ukumbini)

Mheshimiwa Jumanne Kishimba

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwanza na mimi naungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake nzima kwa bajeti hii aliyoletetea. *(Makofi)*

Mimi nina suala moja tu la afya; ugonjwa siyo kitu ambacho unaweza kuchagua wala kupanga muda wa kuugua wala uwe na pesa kiasi gani au uwe maskini. Ni kweli kabisa napongeza Serikali hasa vijiji dawa ni nyingi sana sana kwa mara ya kwanza toka mwaka 1980 kumeonekana dawa nyingi sana sana hospitalini hata mimi mwenyewe nashangaa na tunashukuru sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana aliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya bado kuna matatizo mawili au matatu; tatizo la kwanza sisi tunaotoka mikoa ya Kanda ya Ziwa ambako wenyeji wa maeneo yale aidha, hawataki kukata bima kwa ajili ya *tradition* yao kwamba watakuwa wanajitabiria kifo au kujitabiria ugonjwa, tunaomba Wizara ya Afya au TAMISEMI wawaruhusu wanakijiji wetu anapokuwa ameugua kama ana mbuzi au kuku hospitali au zahanati zetu zipokee atibiwe ili asubuhi au mchana ziuzwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi mtu ameugua mchana au usiku yeye hana pesa lakini anatakiwa aende hospitali na bima hana na leo kuuza mfugo ni kazi lakini kama atapokelewa mfugo au mahindi, atapata matibabu na kesho yake vitu hivyo vitauzwa, hakuna daktari ambaye hajui kuku wala nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu ni maskini, sasa hivi kumezuka kwenye hospitali za Serikali na za Misheni kitu cha kusikitisha sana. Mtu anapokufa kwanza unapewa *bill*/ya marehemu ukiwa huna pesa wanakatalia maiti na maiti ile wanaenda kuizika kama wanatupa mbwa, ni kitu kibaya sana na humu ndani nashangaa Mheshimiwa Waziri Mpango sisi wote ni maiti watarajiwa, Bunge zima.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kishimba naomba ukae kidogo, Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) naongeza muda wa nusu saa ili Mheshimiwa Kishimba aweze kumaliza mchango wake. (*Makofi*)

MHE.JUMANNE K. KISHIMBA:Ahsante sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kwamba humu ndani wote Waheshimiwa Wabunge sisi ni maiti watarajiwa kasoro itakuwa muda, tarehe na wakati. Ni kweli ukiangalia kwenye bajeti yetu tumesamehe unga wa keki, lakini tunatoza tozo la maiti kwenye *mortuary* nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha au Naibu Waziri wa Fedha hebu rudisha hiyo kodi ya unga wa keki ili tufute tozo la maiti kwenye *mortuary*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 95 ya vifo vinatokana na kuumwa na kuumwa kwenye mara nyingi ni kwa muda mrefu, kunapokuwa kwa muda mrefu huyu mtu anakuwa amedhoofika kiuchumi, amedhoofika kiafya sasa leo anafariki ni kweli hospitali inampa bili ya shillingi 500,000 anazipata wapi ameshakufa na huyu mtu wachangiaji wengi humu wamesema Watanzania woote wanalipa kodi wanavuta sigara, wanakunywa bia, wanafanya shughuli zote, sasa kwa nini Serikali isimsamehe mtu aliyefariki imsamehe bili halafu hizo pesa tuzipeleke kwenye keki ni hatari sana watengeneza bajeti najua ni vijana wetu wa Oysterbay ambao nafikiri walijua keki ni kitu cha muhimu sana ndio maana wakashindwa kuelewa kwamba kuna shida nyingi sana kule kwetu vijijini. (*Klcheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ulikuwa Kahama juzi nashukuru sana umepita mle njiani zile nyumba unaziona mle za nyasi ni waganga wa kienyeji. Waganga wa kienyeji ukipeleka mgonjwa bahati mbaya akafariki hawaombi pesa badala yake wanakusaidia na sanda, inawezekanaje sisi Serikali tumdai mtu aliyefariki halafu tukatalie maiti, halafu maiti tukaizike kwa kutupa kwa gharama na bahati nzuri Mheshimiwa Msigwa ni Mchungaji na Mama Lwakatare wangetusaidia sana maana yake turuhusiwe basi watu wakafanye maombi kule kwenye makaburi ya Serikali wajue na kaburi ya ndugu yao ili baadaye baada ya miaka 10 watoto wakipata hela wakachukue mifupa ya baba yao au mzazi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu ambacho kweli ni vizuri tukiangularie sana kama watakubali ni vizuri sana warudishe kodi ya keki maana yake hapo wamefuta kodi ya unga wa keki wanasema unga wa ngano ambaao unatengeneza vyakula, vyakula gani ni keki na biskuti. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la pili hapa sasa hivi kumezuka mtindo huu wa *x-ray* na *dialysis* ya figo. Daladala inauzwa shilingi milioni 50 mpaka shilingi milioni 100 kwa siku inaleta shilingi 50,000 mashine ya *x-ray* inauzwa shilingi milioni 40 mpaka shilingi millioni 100 na yenyewe mashine zote hizi, kwa nini hii inafanya shilingi 200,000 au shilingi 40,000 kwa mtu mmoja kwa nini Serikali isiruhusu watu wanunue *x-ray* wazipeleke hospitali ili bei ya hizi *x-ray* ipungue? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wataalamu wataleta maneno mengi sana ambayo yanahuusu afya, yanahuusu nini lakini ni uongo, ni uongo kwa sababu waganga wa kienyeji wanapewa kibali na Wizara ya Afya kuendesha shughuli zao na waganga wa kienyeji hawana elimu yoyote ya hospitali, kule kwetu Kanda ya Ziwa mgonjwa mahututi ndiyo anapelekwa kwa mganga wa kienyeji ambako hakuna choo, hakuna kitu chochote, ni vipi Serikali ikatae leo kuwa watu wanunue wapeleke hizo *x-ray* kwenye hospitali ili bei hii ipungue? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa watu wetu ambaao ni wa mjini ambaao hawana pesa, nchi nyingi sasa hivi duniani bili yako ya maji na bili ya umeme inakudhamini hospitali. Anapofika mtu akatibiwa ikija *bill* ni shilingi 24,000 mnakaa na hospitali mna-*bargain* kwamba utalipa shilingi 4,000, 4,000 wanakwambia lete *bill* yako ya maji au *bill* ya umeme wanaingiza shilingi 4,000, 4,000 mle kwa kuwa *TANESCO* na Idara ya Maji ni taasisi za Serikali, wakichukua ile shilingi 4,000 wataipelekea hospitali, lakini mtu wetu anakuwa amepona kuliko sasa hivi kama huna pesa ni tatizo sana sana, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangularie sana suala hili ili kusudi itusaidie sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea suala zima la biashara; juzi kwenye mkutano wa Mheshimiwa Rais suala walilokuwa wanalalamika karibu wafanyabiashara wote lilikuwa ni suala la *investigation* baada ya kuwa mtu umemaliza kulipa kodi. Suala la kutafuta watu watakatifu mimi siliamini maana yake dini ina zaidi ya miaka 2000 toka Bwana Yesu aje, lakini mpaka leo watu hawajashika dini, dawa ya kumaliza mgogoro ni kuondoa zile sheria ambazo zinatusababishia mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* wanayo sheria inayoruhusu mtu ambaye hakufanya hesabu *wam-charge* kwa *percent* ya mauzo, lakini sheria ile inawaruhusu wao kumu-*investigate* yeye, lakini sheria ile iliachwa na mkoloni na ilikuwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba kama mtu hana vitabu atalipa 2% ya mauzo yake, lakini na yeye asilete gharama zake, kwa hiyo kama mtu ameuza shillingi billioni moja, analipa shillingi 20,000,000 na yeye hawezi kuleta hesabu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu asilimia 90 ya wafanyabiashara wa Tanzania elimu yetu ni darasa la saba, wengine hawakusoma kabisa. Sasa inakupa kazi ngumu sana utunze *store* ya mali, utunze na *stoo* ya karatasi na bado karatasi hizo ukizipeleka unaambiwa hazifai lazima utatoa hela. Lakini kama wao *TRA* walishamfanya *investigation* mtu zaidi ya miaka mitano, wakajua huyu mtu *sells* zake huwa ni hizi na tulikusanya hela hizi kwa nini wasichukue *formula* ile ile wakaigawa ikaenda kwenye *sells* ya mauzo ambayo itamaliza kabisa ule ugomvi wote uliokuwepo siku ile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la Kariakoo; ni kweli Kariakoo imekufa, lakini Kariakoo imeuwawa na vitu viwili. Wataalamu wetu nafikiri hawajui kitu gani kinauzwa Kariakoo. Kariakoo haiuzi soda, haiuzi *diesel*, haiuzi vitu hivi ambavyo kwenye *tarrif* za *TRA* zinahesabiwa kwa tani na lita. Vitu vinavyouzwa Kariakoo ni vitu hivi vidogo vidogo. Nitatoa mfano uki-*import glass* Sheria ya *TRA* ina kitu kinaitwa *tariff*, *tariffya glass* inaitwa *glassware*,

lakini kuna *glassya* shilingi 800 na kuna *glassya* shilingi 10,000; *TRA* kwa kuwa anataka pesa atachukua *glassya* shilingi 1,000 kwenda kui-charge 5,000 akikuwekea kwenye shilingi 5,000 hautauza na watu wote Watanzania, wa Malawi na wa Kongo wanafata hii *glass ya shilingi* 1,000 hawa watu wa Samora ndiyo wanafanya glasi ya shilingi 10,000. (*Makofi*)

Kwahiyu nafikiri *TRA* waangalie *tariffni* kitu ambacho tuliki-*download* sisi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, ni vizuri *TRA* wachukue vitu waviainische ili mtu alipie kwa kitu alicheleta, watu wote watarudi kama wenyewe watakubali watu walipie kwa kile kitu alicheleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukileta kontena moja la *glass hutalilipia* hapa, lazima ulipeleke Mutukula ukalipie Mutukula ili watu wachukue polepole na baskeli kuleta au ulipeleke mpaka Tunduma ili watu waanze kulileta kwa sababu watu wale kule Wazambia wanakubali ulipie kwa *item* uliyoleta, huku unatakiwa ulipie kwa *tariff*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukileta nguo zinazouzwa Kariakoo ambazo ni *t-shirt*, *t-shirt* ziko za shilingi 3,000, iko *t-shirtya* shilingi 20,000. Kwenye hesabu ya *tariffunalipa excise duty*, unalipa VAT halafu unaenda kwenye *weight* (kwenye uzito) na nguo nzito ni ile ya bei rahisi nguo nyepesi ndiyo ya bei ghali. Sasa haitawezekana ile nguo kuiiza ndiyo maana inakwenda nje halafu inarudi huku, nafikiri wataalamu wetu wa *TRA*... (*Makofi*)

MHE.SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Turkey anayezungumza hapo ni Profesa sasa...

MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY: Taarifa ninayompa maneno anayozungumza ni sahihi kabisa na ukienda kuangalia chupi ile ya kamba ndiyo ghali zaidi kuliko chupi nzima, ahsante sana. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kishimba unaipokea taarifa hiyo?

MHE.JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wataalamu wetu wa *TRA* ni vizuri kabisa wakubaliane na wafanyabiashara, ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha awaite wafanyabiashara wakiwa wametulia ili apate kabisa *data* ili turudishe soko letu la Kariakoo. Ni kweli kabisa wachangiaji wote wanaliongea hili na kwenye Kamati ya Bajeti tumejaribu sana kuliongea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa Benki Kuu ya Tanzania nafikiri wakati wowote itatangaza utaratibu mpya wa namna ya ku-*import* mali. Utaratibu uliopo unaotarajiwa ni kwamba mtu lazima atume pesa kwa *TT* kwenda kwenye *source* ya kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba wataalamu wote kabla hawajafanya kitulabda na wao watoe watu wao waende kule Dubai na China waone mali inanunuliwa namna gani. Kule China na Dubai hakuna mahala unaweza kumtumia mtu hela ukazikuta hizo hela, watu wanarusiwa kule wakiwa na hela *cash* kwa sababu hata mali aliyokuuzia anaweza akakuletea *fake* na ukirudi kwenye lile duka limekuwa *saloon*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama utatumia hela toka hapa, utamtumia nani kule China au Dubai, haiwezekani, ndiyo maana tunaomba wataalam wetu basi labda wachanganye changanye na watu wa biashara kidogo ili wanachotengeneza kionekane cha Tanzania maana yake inaonekana kinachotengenezwa hata wananchi wanatucheka kwamba hivi hata ninyi Wabunge mnafanya nini huko maana yake kinachotoka ni kama kimetoka London. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo yote nashukuru naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji wetu kwa jioni na naamini kwamba wote mtakubaliana na Mheshimiwa Spika alivyomtunukia uprofesa, Profesa Jummane Kishimba. Huyu anatoka sehemu ya madini na anatema madini. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambaao hawakupata fursa ya kuingia asubuhi; tunao wageni saba wa Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvvi ambao ni wakulima kutoka Jimboni kwake Mkuranga, Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani Abdul Zombe, karibuni sana, bila shaka hawa ndio walioleta ng'ombe waliokuwa wanaoneshwa kule Nanenane, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wengine ambaao wamekuja kwa ajili ya mafunzo nao ni wageni 90 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosoma *Business Studies and Law* wakiongozwa na Ndugu Kigoma Marwa, karibuni sana, karibuni sana wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa siku yetu ya leo, kwa hiyo, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.58 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 19 Juni, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*